**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |

| | |
|---|---|
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |

| | |
|---|---|
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |

| | |
|---|---|
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| **Ndugu Yahya Khamis Hamad** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi** |

**Kikao cha Nne – Tarehe 20 Mei, 2015**

*(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)*

**Dua**

*Mhe. Spika,(Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, noamba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa mwaka 2015/2016. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Naomba kuwasilisha hati mezani ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti, kuhusu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 42**

**Usafi wa Mji wa Zanzibar Wakati wa Ujio wa Rais wa Ujerumani**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kuuliza swali langu namba 42, naomba uniruhusu dakika moja tu nitowe utangulizi. Kabla sijajibiwa swali langu Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri, wasinione mtu wa ajabu kuuliza swali hili karibu kila kikao. Moyo wangu Mhe. Spika, unaniuma sana na suala hili na ukizingatia wageni wanaoingia kutoka mataifa mbali mbali katikati ya nchi yetu na kuona kwenye mlango ule kuwekwa mambo ya ajabu. Hasa ndugu zetu wa Muungano wa kudumu Tanganyika wanapokuja kutembelea Zanzibar na kuona hali kama ile. Ni kitu cha kusikitisha na ni cha kutia huruma sana.

Kwa hivyo, naiomba serikali wasinione mtu wa ajabu kwa kurudia kuuliza swali hili karibu kila kikao, ni suala ambalo halipendezi na linachafua mandhari yetu. Naomba kujibiwa swali langu Mhe. Spika.

Ziara ya Rais wa Ujerumani tumeshuhudia mambo mengi ikiwemo usafi uliofanyika katika Mji Mkongwe na usafi wa kusafisha fukwe katika ukanda wa Forodhani na Malindi pamoja na kuondolewa mawe au makalbi katika eneo ya Bandari ya Malindi, usafi huo ulikuwa wa kudumu au wa muda.

(a) Kwa kuwa kero ya wananchi wengi ni suala zima la usafi. Je, Serikali inawaahidi nini wananchi baada ya kushuhudia kuwa inauwezo wa kusimamia na kuweka Mji safi kama ilivyoonekana katika ziara hiyo.

(b) Hatua ya kuondoa makalbi katika eneo la Bandari ya Malindi kuelekea Forodhani imeleta mandhari nzuri na kupunguza msongamano; Je, hatua hiyo ya kufanya usafi itakuwa ya kudumu au ya muda.

(c) Serikali imetumia kiasi gani cha gharama za kuweka safi Mji Mkongwe baada ya kukabiliwa na mgeni na hatua kama hizi zichukuliwe katika maeneo mengine ya Manispaa na Halmashauri zake na ni kitengo gani kilichofanyakazi ile, Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini, Mji Mkongwe au Baraza la Manispaa.

**Mhe. Spika:** Lijibiwe au lisijibiwe? Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa heshima ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inayowajali wananchi wake wa Zanzibar, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.42 lenye kifungu (a), (b) na (c), kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi swali lake, naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, Serikali inakubaliana na wewe kuwa usafi wa mji ni muhimu sana kwa wakaazi na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla.Kwa hivyo, serikali inaendelea na juhudi mbali mbali hivi sasa, katika kuhakikisha suala la usafi wa mji unaimarishwa, licha ya kupatikana kwa vifaa muhimu kupitia mradi unaoendelea wa uimarishaji wa huduma mijini (*ZUSP*), kama magari ya kusombea taka na makontena yakutosha katika maeneo mbali mbali ya mji wetu.

Mhe. Spika, katika kuendeleza huduma za usafi wa miji na kuwa endelevu, serikali kupitia Baraza la Manispaa imejifunza mengi wakati wa kipindi cha

maandalizi ya ziara ya Mhe. Rais wa Ujerumani, na jambo kubwa tulilojifunza ni kuwa na mashirikiano na uwajibikaji wa kila mmoja ni muhimu sana katika kuhakikisha usafi wa mji wetu unaimarika. Vile vile, tumejifunza kuwa na mashirikiano ya pamoja kwa kila taasisi kuwajibika kwa upande wake tunaweza kuhakikisha mji wetu kuwa msafi kwa gharama ndogo zaidi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, naomba kutoa wito kwa kila mmoja wetu kuanzia mwananchi, Sheha, Mhe. Diwani, Mhe. Mbunge, Mhe. Mwakilishi, Taasisi za Serikali na za binafsi kuwajibika ipasavyo katika kuimarisha usafi wa mji wetu, ili udumu na uwe kuliko kipindi cha ziara ya Mhe. Rais wa Ujerumani.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 42 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa uzoefu tuliojifunza katika maandalizi ya ziara ya Mhe. Rais wa Ujerumani, serikali inakusudia kuimarisha zaidi huduma za usafi wa mji kwa kuvishirikisha vikundi vya jamii na Mazingira (*CBOs* na *NGOs*) na Taasisi za Serikali na binafsi na kuwahamasisha zaidi wananchi katika kushiriki, kutunza na kuchangia gharama za usimamiaji huduma za usafi wa mji kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Manispaa.

(b) Serikali imeweka makalbi katika eneo la Bandari ya Malindi kuelekea Forodhani, kwa lengo la kupunguza msongamano wa gari kwa kuheshimu taratibu za urithi wa Mji Mkongwe, na hasa wakati wa abiria kushuka na kupanda nyakati za usafiri wa meli na boti. Serikali iliondoa makalbi wakati wa ziara kwa sababu za kiusalama na sio vyenginevyo.

(c) Baada ya kukabiliwa na mgeni Baraza la Manispaa ilipokea TZS. 2,500,000/= kutoka Serikali Kuu kupitia Kamati ya Kitaifa ya Sherehe na Mapambo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Fedha hizi zilitolewa kwa nia ya kulisaidia Baraza katika masuala ya usafi. Shughuli hii ya usafi iliwashirikisha wafanyakazi wa Baraza la Manispaa, vikundi vya kijamii pamoja na kujumuisha wadau na Taasisi mbali mbali za serikali wakiwemo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mamlaka ya Bandari, Mji Mkongwe na Idara ya *UUB*.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu marefu ya Mhe. Waziri ambaye namuheshimu sana rafiki yangu, kutokujibu majibu ya swali ya msingi. Mhe. Spika, mimi nimezaliwa shamba, nimekuwa shamba, nimesoma shamba na kwa hivi sasa naishi mjini. Mhe. Waziri ananiambia amepunguza msongamano, makalbi yaliyokwenda kuwekwa pale sasa hivi

hayapungui kutoka pale mpaka hapa, tunapunguza au tunazidisha. Sisi sote tuna macho na tunaona Mhe. Waziri, tumepunguza au tumezidisha.

Mhe. Spika, pamoja na majibu alipokuja wakati wa Rais makalbi yameondoshwa na kuleta mandhari nzuri ya bandari na kuonekana mji kuwa safi, leo tumeshuhudia kurudishwa. Mhe. Spika, tarehe 30/05/2014 niliuliza swali hili. Naomba kunukuu *Hansard* zake, Mhe. Naibu Waziri alijibu:

"Mhe. Spika, ni kwamba serikali haijaachia suala hili na bado tunaendelea kulifanyia kazi ili kuona usumbufu huo unaondoka."

Serikali imekiri kwa kupitia chombo hiki cha wananchi kuwa usumbufu huo upo, sio maneno yangu haya ni maneno ya Mhe. Naibu Waziri. Tena nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa umakini wake.

Baada ya hapo, suala la pili ni kweli *concrete slabs* zilizokuwa zimewekwa Forodha Mchanga zilikuwa zimewekwa zimezuwia barabara kwamba usipite *concrete slabs* zilizowekwa kwa sasa katika eneo hilo la bandari, zimejaribu kufanya *partition* kwa ajili ya kugawa barabara wanaopita kwenda mjini waende na wanaotoka mjini waweze kupita.

Kwa hivyo, mimi naamini pamoja na makoseo. Narudia tena Kiswahili Mhe. Spika, pamoja na makoseo ya kuweka *slabs* zile, lakini maudhui ni mazuri, tunachoweza kukifanya sisi ni kutafuta namna nzuri ya kuweza kugawa barabara ile, ikiwa aidha kuweka rangi kama inavyokubalika katika viwango vya kimataifa, au kuweka mawe maalum yale madogo yenye ishara ya kuleta *reflector*, kwa ajili ya kuongoza watu viziri, ziaidi hasa nyakati za usiku. Tunatambua jiwe lile lililowekwa ukifika wakati wa usiku taa zinapiga hazina *reflector* ni hatari anaweza kuvamia, haya sio maneno yangu.

Niendelee kumshukuru Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, alipouliza swali la nyongeza. Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kuongeza mawe yale huoni unaendelea kuwa hii barabara unaifanya zaidi iwe nyembamba.

**Mhe. Spika:** Mhe. Jaku Hashim, swali lako ni nini?

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Suala bado tunaongeza msongamano na hivi sasa cha kusikitisha kuna ujenzi unaendelea na msongomano utazidi kuwa mrefu. Pamegaiwa njia pale sasa hivi ya kupita miguu mbali na ya kupita gari. Serikali imekiri kuwa imefanya kosa kwa suala hili, kwa nini tusikubali makosa yetu. Hilo la kwanza Mhe. Spika, bado la pili.

Mhe. Spika, kwa nini serikali imeshindwa kuweka michoro ya kutenganisha barabara zile, japo kuweka chokaa kama rangi itakuwa ghali. Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi namsubiri zaidi kwenye bajeti Mhe. Waziri, naomba kuweka *Hansard* sawa. Hii ni *try,* mchezo bado. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, swali la nyongeza la Mhe. Mjumbe, lina maelezo mengi ya *Hansard* ya Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, kwa bahati mbaya *Hansard* hiyo pamoja na kwamba serikali inawajibika kwa pamoja, haikuahidiwa na wizara yangu ambayo yeye ameielekeza swali lake. Sasa mimi naomba nichukuwe nafasi hii kujibu maswali yake mawili kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe, alipoanza kuuliza swali la msingi, alianza na maelezo na akasema wageni wanaokuja nchini kwetu wanatushangaa sana, kwa serikali kuweka makalbi katika barabara ile. Lakini wageni wanaokuja nchini kwetu hawatushangai tu kwa kuwekwa makalbi, wanatushangaa kwa mambo mengi ambayo wakija kwetu wanayaona ni mambo ambayo hayastahiki kufanywa kutokana na usugu wa wananchi wetu na watu wanaotumia barabara.

Kamati ya Usalama Barabarani ilipokea malalamiko ya usumbufu na msongamano uliopo katika bandari ya abiria. Kamati hii ambayo inaongozwa na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, ilipeleka suala hili serikalini kuanzia ngazi ya Mkoa wakalijadili. Walipoona hawawezi kulipatia ufumbuzi, wakalipeleka katika ngazi ya Mkoa. Katika ngazi ya Mkoa lilijadiliwa suala hili ambapo liliwashirikisha wataalamu wengi wa serikali, wakiwemo wa Miundombinu na Mawasiliano, wataalamu wa Manispaa, wataalamu wa Mji Mkongwe, wataalamu wa Bandari na wengineo. Wakaona ili kupunguza msongamano wa madereva kufanya vurugu wakati wa meli kuondoka na kuingia bandarini kwa kugombaniana abiria, ni vizuri madereva wakapangiwa utaratibu wa kutokuzungusha gari katika maeneo ambayo wanashuka abiria, ndipo ulipotoka uamuzi wa kuweka makalbi.

Mhe. Spika, serikali inapoona kadhia inawapata wananchi, basi inayo haki ya kuweza kuwatafutia ufumbuzi ili waondokane na kadhia hiyo. Sasa kama lilivyokuja, kwa sababu suala hili limeulizwa kwenye wizara yangu, basi mimi nitawaambia waliokaa kwenye vikao halali kwa kuwashirikisha wataalamu wote waliangalie upya suala hili, kama bado wakiondosha makalbi, tatizo la kuvunjwa sheria ambako kunapelekea kutokuwa na usalama mdogo pale bandarini suala hilo litaondoka. Kama wakihisi wao kwa tathmini yao, kwamba wakifanya hivyo vurugu litaendelea makalbi yataendelea kuwepo.

Kwa sababu jambo hili haliamuliwi na mtu mmoja, serikali inapofanya kazi zake inafanya kwa mujibu wa taratibu. Kamati ya usalama barabarani kwa mujibu wa sheria wanayo haki ya kuona kama kuna matatizo na kuweza kuyatafutia ufumbuzi.

Swali la mwisho ambalo ameuliza Mhe. Jaku Hashim, hivi sasa ni suala la muda kutokana na ujenzi unaoendele wa *Sea wall*, likimalizika hilo basi ule usumbufu ambao umeongezeka, na huu usumbufu unatokea wakati wa kuingia meli na kuondoka meli, sio wakati wote. Hapa nataka aamini Mhe. Jaku Hashim, kama alivyosema yeye ni rafiki yangu, ni rafiki yangu kweli. Lakini kwa hili, mimi nitaendelea kusimamia taratibu, kanuni na sheria kama nilivyoapa kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar, sitalifanya hivi kwa sababu ya urafiki wetu mimi na wewe. Nitalijibu kwa mujibu wa utaratibu, katiba na sheria ambayo mimi imenipa mamlaka kuweza kusimamia shughuli za serikali katika sekta zangu ambazo nimekabidhiwa na Mhe. Rais. Ahsante sana.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Spika. Wakati Mhe. Waziri akijibu swali la msingi nambari 42 lilikuwa lina vifungu vitatu vidogo (a),(b) na (c). Mimi nilitaka nimuulize swali la nyongeza katika swali hili namba 42(c), ambalo lilizungumzia suala zima la usafi na wakati Mhe. Waziri akijibu alitaja mpaka na gharama ambazo zilitumika katika suala la usafi katika maeneo ya Mji Mkongwe.

Swali langu Mhe. Spika, ni kama ifuatavyo. Mimi nataka nikubaliane na Mhe. Waziri katika jitihada hizi na nilipongeze Baraza la Manispaa kwa usafi mzuri, ambao umeonekana hivi karibuni baada ya kupata magari ya *ZUSP*. Swali langu liko hapa Mhe. Waziri, baada ya mazingira kuwa mazuri katika Manispaa ya Zanzibar katika suala zima la usafi, kumejitokeza kero jengine katika suala zima la usafishaji huu, nalo ni magari mapya kukimbia kwa kasi na kuanza kuhatarisha usalama wa wananchi katika barabara ya Kwerekwe hadi jaa kubwa la Kibele.

Je, Mhe. Waziri huoni kuna haja ya usafi huo wa Manispaa ya Zanzibar kufanywa nyakati za usiku ili kuja kuepusha ajali za barabarani.

**Mhe. Spika:** Mhe. Ali Salum Haji, hili ni swali la Usalama wa Barabarani moja kwa moja halihusiani na usafi. Hebu fanya utaratibu wa kuiandikia wizara inayohusika juu ya jambo hili. Tunaendelea.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi asubuhi hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika majibu yake mama Mhe. Waziri, alisema kwamba walifanya mashirikiano makubwa sana kwa ujaji wa Rais kutoka Ujerumani kwa kufanya usafi katika Mji.

Lakini je, nimuulize Mhe. Waziri, huoni kutokufanya mashirikiano ya usafi kabla hajafika Rais kutoka nje, huoni huku ni kumdhalilisha Rais wetu aliyekuwepo hapa Zanzibar na viongozi wengine. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kabla sijamjibu naomba nimpongeze sana kwa hatua za awali za mchakato ndani ya Chama chake.

Mhe. Spika, mashirikiano tuliyoyafanya katika eneo dogo la Mjimkongwe wakati wa ziara ya Mhe. Rais wa Ujerumani hayamdhalilishi Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, yamemjengea heshima kwamba Rais yule amekuja nchini salama na ameondoka salama na kwa utashi wake ameweza kutembea katika eneo ambalo ameshuka Bandarini mpaka katika hoteli ya Serena na akaona linaridhisha. Kwa hivyo, zaidi limemjengea heshima na mashirikiano haya tunayaendeleza kwa kushirikiana na vikundi mbali mbali katika maeneo yote ya Mji wetu wa Zanzibar kutokana na usafi unaoendelea hivi sasa. Ahsante sana.

**Nam. 50**

**Kufukuzwa Kazi Wafanyakazi wa *ZRB* Pemba**

**Mhe. Muhammed Mbwana Hamad (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) -** Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni kunataarifa kuwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) Kisiwani Pemba imewafukuza kazini wafanyakazi wake wawili, kwa madai ya kukosa umakini katika kufanyakazi zao na hivyo kuipunguzia mapato Serikali kwa kiasi kikubwa.

(a) Je, taarifa hizi ni za kweli.

(b) Kama ni za kweli ni sababu gani za msingi zilizopelekea wafanyakazi hao watimuliwe kazini.

**Mhe. Waziri wa Fedha -** Alijibu:-

Mhe. Spika, heshima kubwa naomba kujibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 50 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli tokea tarehe 25/3/2015, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) imewafukuza kazi wafanyakazi wake wawili kituo cha Pemba.

(b) Mhe.Spika, sababu za msingi zilizopelekea wafanyakazi hao wawili wafukuzwe kazi ni kutokana na kutiwa hatiani na Mahakama ya Chake Chake Pemba kwa makosa yafuatayo:-

i) Kuiba Tshs. 19.2 milioni mali ya Shirika la Umeme, kinyume na kifungu cha 274 (4) cha Sheria Nam. 6 ya mwaka 2004 ya Sheria ya Zanzibar.

ii) Kula njama ya kutenda kosa kinyume na Sheria Nam. 6 ya mwaka 2004 ya Sheria ya Zanzibar.

iii) Kutengeneza hati ya uongo kinyume na kifungu cha 340 (d)(1) na kifungu cha 342 (2) ya Sheria Namba 6 ya mwaka 2004, Sheria ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Mahakama ya Chake Chake Pemba imewatia hatiani wafanyakazi hao na kutakiwa kulipa fedha hizo pamoja na faini ndani ya kipindi cha miezi miwili. Uongozi wa *ZRB* umeawafukuza kazi wafanyakazi hao baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la jinai (wizi) kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni za Utumishi za *ZRB* za mwaka 2002 kifungu cha 69 (3).

**Mhe. Muhammed Mbwana Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kumuuliza Mhe. Waziri, swali la nyongeza.

Kwanza naipongeza serikali kwa hatua waliyoichukua kuwafukuza kazi wabadhilifu hawa wa mali ya umma. Kwa kuwa watendaji wengi wa serikali wanaosimamia matumizi ya serikali kama Wahasibu wanakuwa na mapungufu mbali mbali, wanakwenda kinyume na Sheria ya Manunuzi ya Zanzibar. Na kwa kuwa ripoti mbali mbali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinaonyesha mapungufu ya watendaji hawa na zinaibua fedha nyingi ambazo zinatumika bila ya kufuata taratibu za kiserikali.

Je, Mhe. Wizara, yako na serikali kwa jumla ina mpango gani ya kuwachukulia hatua muwafaka kama hawa waliochukuliwa hatua watendaji wanaosimamia fedha ambao wanakwenda kinyume na taratibu za serikali. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, nimekuwa nikieleza na nitaendelea kueleza hakuna mfanyakazi atakaehukumiwa au kudhulumiwa au kudhaniwa au kushtakiwa bila ya kufuata utaratibu na utaratibu upo. Ripoti za *CAG* zinaelezea mapungufu ya matumizi. Mapungufu hayo yanafanyiwa kazi lakini haimaanishi kwamba kuna wafanyakazi kwamba wamehukumiwa kutokana na ripoti ile. Ili

wafanyakazi waweze kuhukumiwa lazima tufuate utaratibu, kwanza kumsimamisha kazi, baadae kufungua mashataka na baadae kumpeleka Mahakamani na Mahakama ndio ithibitishe kwamba mfanyakazi huyu kweli ametiwa hatiani, itakapothibitishwa kwa mfanyakazi yeyote yule sheria zitafuata mkondo wake na Kanuni za Utumishi zinaeleza kwamba afukuzwe kazi.

Kwa hilo ikithibitisha Mahakama kwamba ana kosa atafukuzwa kazi tu.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi hii kuweza kumuuliza Mhe. Waziri maswali ya nyongeza yenye (a) na (b).

Mhe. Waziri, jana mimi nilitoa hoja hiyo na kwa kuwa nilianza kutafuta uchochezi wa kutambua njia ya kuweza kutumiwa ili watu hawa kuweza kutiwa hatiyani.

a) Mhe. Waziri kwa kuwa Mahakama imeamuru hawa watu walipe hizi fedha, je, tangu kipindi hicho mpaka hivi leo kwanza fedha zimeshalipwa.

b) Pili, kuwa hili suala leo ni *example* kwa hawa watu wawili, je, serikali ina mkakati gani wa endelevu na hasa kutokana na masuala kama hayo ya mabadiliko ya fedha na mkaweza mkatupa taarifa kwenye chombo hichi.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa taarifa ambazo nimezipata, kwa sababu kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi hizo fesha hazikuwa fedha za *ZRB* zilikuwa ni fedha za Shirika la Umeme. Kama nilivyoeleza baada ya kufatilia kwa karibu zaidi taarifa ambazo nimezipata wafanyakazi hao wameanza kulipa na kuna muelekeo kwamba wameshakamilisha malipo yao kwa sababu Mahakama imewapa miezi miwili tu walipe fedha hizo shilingi milioni 19.

Mhe. Spika, suala la pili, huu ni utaratibu mzuri na huu utaratibu unapaswa kuendelezwa. Lakini kama ninavyosema kwamba tusimuhukumu mtu kwa shutma. Lazima tufuate taratibu, taratibu zake kwanza ukisikia au ukipata taarifa ni kumsimamisha kazi na baadae kumfungulia mashtaka halafu mashtaka yale yapelekwe Mahakamani na Mahakama ndiyo ithibitishe.

Mimi nataka nimuombe tu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwamba serikali kwa ujumla tusimamie utaratibu huu na pale itakapothibitishwa kwamba wafanyakazi hawa na hawa na hawa Mahakama imewatia hatiani na serikali imewafukuza kazi, basi tuje tutoe taarifa hapa Barazani. Huo ndio uwazi, hatuwezi tukafuga wafanyakazi wanaoiibia serikali. Jana nilisema hapa, haya mapato jamani ni kodi za wananchi na kodi za wananchi zinapaswa kurudi kwa wananchi, sasa kama

kuna wafanyakazi wanaiibia serikali na sisi tunakaa kimya tu. Mimi nasema kwamba utaratibu huu tuuendeleze na tuje tutoe taarifa Barazani.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana, naomba nimuulize Mhe. Waziri wa Fedha swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri kwa sababu amekiri kwamba kuna wafanyakazi wawili waliiba kiasi cha fedha milioni 19 na niipongeze serikali kwa kuchukua hatua ya kuwafukuza kazi na hatimaye kupewa kazi ya kulipa fedha hizo. Je, swali langu baada ya kuwafukuza kazi na kulipa fedha hizo ndio adhabu imetosha au tunawapa mwanya kama mtu anaweza akaiba halafu akalipa.

**Mhe. Waziri wa Fedha:**Mhe. Spika, nataka nieleze kwamba Mahakama ya Chake Chake Pemba imewatia hatiani hawa vijana wawili na kuamuru kwamba vijana hawa walipe fedha zile pamoja na fidia. Hiyo ndiyo hukumu ya Mahakama, lakini sisi kama serikali tuna Kanuni na Sheria za Utumishi. Na sisi kama *ZRB* tuna Kanuni za Utumishi, tumeangalia Kanuni zetu zinatutaka tufanye nini baada ya kutiwa hatiani mfanyakazi wa serikali.

Mhe. Spika, Kanuni zinasema kwamba mfanyakazi yeyote wa serikali ambaye ametiwa hatiani na Mahakama kwa kosa la jinai, kosa kama hili la wizi anapaswa afukuzwe kazi. Kwa hivyo, sisi kwa upande wetu tumeangalia Kanuni inavyotuelekeza na tumechukua hatua kulingana na Kanuni inavyotuelekeza. Kanuni haituelekezi vyengine katika kosa kama hili. Kwa hivyo, sisi tunafuata Kanuni. Kanuni haijatuelekeza kwamba tumfunge na wala Mahakama haikusema kwamba afungwe, Mahakama imesema hivyo na sisi tumefuata amri ya Mahakama na tumefuata amri ya Kanuni zetu.

Kwa hivyo, kwa utaratibu huu utakuwa humuonei yule mfanyakazi yeyote utakuwa humuonei kwa sababu kanuni ndivyo zilivyoelekeza. Kwa hivyo, na sisi tumefuata Kanuni zilivyotuelekeza na tumeshawafukuza kazi.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri tunakushukuru na tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nichukue nafasi hii kwa heshima nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

**Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, naomba kutoa Hoja kwamba Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili lipokee, lijadili na hatimae liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuendelea kuijaalia nchi yetu amani na utulivu na kutuwezesha kufanyakazi zetu kwa mafanikio. Vile vile, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuliendesha Baraza letu kwa amani na salama na ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, kwa aina ya kipekee namshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake mahiri na usimamizi mzuri wa shughuli za Serikali unaozingatia Katiba na Sheria za nchi. Mhe.Rais amekuwa mstahamilivu mkubwa, asiyetetereka na kuwa mstari wa mbele katika kuhimiza uwajibikaji na uadilifu katika utendaji wa shughuli za Serikali. Chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, nchi yetu imepiga hatua kubwa za maendeleo katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa kiongozi wetu huyu afya njema na umri mrefu, yeye na familia yake na amzidishie hekima na busara ili aendelee kuiongoza vyema nchi yetu.

Mhe. Spika, aidha, namshukuru Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuendelea kumshauri vizuri na kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya masuala mbali mbali yanayohusu maendeleo ya nchi yetu. Pia, namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mashirikiano yake makubwa kwa Ofisi yangu.

Mhe. Spika, pia, napenda kuwapongeza kwa dhati Naibu Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini. Vile vile, nawashukuru Wenyeviti wa Baraza, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi wa Viti Maalum na Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa namna wanavyokusaidia katika kuliendesha Baraza letu hili.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza lako Tukufu kwa kusimamia vyema utendaji katika Taasisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, natoa shukrani maalum kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura, Makamu Mwenyekiti Mhe. Saleh Nassor Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Wawi na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

ya mwaka 2015/2016 na kutupa ushauri utakaotuongoza katika utekelezaji wa malengo na majukumu ya Ofisi yetu.

Mhe. Spika, pia, nawapongeza Wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu kwa kuipitisha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2015/2016 iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Fedha, tarehe 13/05/2015.Bajeti hiyo ndiyo itakayoiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa malengo iliyojiwekea katika shughuli za kuwaletea maendeleo wananchi.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa naomba nichukue fursa hii kumkumbuka ndugu yetu na mwenzetu Marehemu Salmin Awadh Salmin alietutoka ghafla tarehe 19 Februari, 2015. Marehemu Salmin alikuwa kiongozi shupavu, hodari na wakati wote alikuwa mstari wa mbele kutetea wananchi na kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Kuondoka kwake kumeacha pengo kubwa na daima tutamkumbuka kwa mchango wake kwa jamii na nchi yetu. Mungu ailaze roho ya Marehemu peponi, *Amin*. Aidha, natoa pole kwa wale wote waliopoteza ndugu na jamaa zao katika maafa yaliyotokea tarehe 3 Mei, 2015 yaliyotokana na mafuriko kutokana na mvua kubwa za masika na waliopata hasara ya kupotelewa na kuharibikiwa na mali zao. Serikali inachukuwa hatua zinazostahiki kuona kwamba wale wote waliofikwa na maafa hayo wanarudi katika hali ya maisha yao ya kawaida.

**HALI YA KISIASA:**

Mhe. Spika, naomba nizungumze kidogo kuhusu hali ya siasa nchini. Hali ya Kisiasa Zanzibar inaendelea kuwa ya shwari, amani na utulivu, hali ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta maendeleo kwa kutoa fursa za uwekezaji, kufanyika kwa shughuli za biashara na kutoa nafasi nzuri kwa wananchi kufanya shughuli zao za kimaisha bila ya wasi wasi. Hata hivyo, kunahitajika mashirikiano kwa viongozi na wananchi wote ili kuhakikisha amani na utulivu unazidi kuimarika katika nchi yetu, rasilimali kubwa katika nchi yetu ni umoja, amani na utulivu, kwa hali yeyote lazima tuilinde rasilimali hii.

Mhe. Spika, mwaka huu nchi yetu inakabiliwa na mambo mawili makubwa na muhimu, ambayo ni Kura ya Maoni kwa Katiba Inayopendekezwa ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Uchaguzi Mkuu. Kwa upande wa Kura ya Maoni, baada ya kupatikana kwa Katiba Inayopendekezwa, wananchi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla watapata fursa ya kuipigia kura ya maoni Katiba hiyo katika tarehe itakayotangazwa hapo baadae na Tume ya Uchaguzi. Napenda kuchukua nafasi hii kwa mara nyengine tena kuwanasihi wananchi kuisoma na kuielewa Katiba hiyo ili hatimae waweze kutoa maamuzi sahihi wakati wa

kuipigia kura.

Kwa upande wake Serikali imechukuwa juhudi ya kugawa nakala za Katiba Inayopendekezwa kwa wananchi Unguja na Pemba. Ni imani yangu kuwa wananchi wote wenye sifa za kupiga kura wataitumia fursa hii adhimu ya kuitumia haki yao ya kidemokrasia kwa kwenda kupiga kura ya maoni.

Mhe. Spika, kwa upande wa Uchaguzi Mkuu, wananchi watapata fursa ya kuchagua viongozi wao wakiwemo Rais wa Zanzibar, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wabunge, na Madiwani ambao watawatumikia katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Katika kufanikisha zoezi hilo, nawaomba wananchi ambao bado hawajajiandikisha na wanazo sifa za kufanya hivyo waende kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kujitokeza kwa wingi kwenda kupiga kura muda utakapowadia.

Mhe. Spika, kwa upande wa maandalizi ya uchaguzi huo, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inaendelea vyema na matayarisho ikiwemo uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kutoa Elimu ya Wapiga Kura na upatikanaji wa vifaa mbali mbali vya upigaji kura. Serikali kwa upande wake itahakikisha kwamba, Uchaguzi Mkuu huo utakuwa wa haki na utafanyika katika hali ya utulivu, usalama na amani. Hivyo tunaomba wanasiasa wote wasiwe chanzo cha kuharibu amani na upendo uliopo bali wawe chanzo cha kuimairisha amani, umoja na upendo.

## HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

Mhe. Spika, kuhusu hali ya Uchumi wa Zanzibar kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora wakati akiwasilisha hali ya uchumi kwa mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/2016 katika Baraza lako Tukufu, uchumi wa Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2010/2014 umeonesha mwenendo mzuri na umekua kwa kiwango cha kuridhisha cha wastani wa asilimia 6.5. Ukuaji huo wa uchumi ulitokana na kuimarika kwa sekta ndogo za Ujenzi, Fedha na Bima, Usafiri, Habari na Mawasiliano na Sekta ndogo ya Utawala wa Umma.

Mhe. Spika, kwa upande wa Pato la Taifa kwa mwaka 2014, Pato halisi lilikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 7.0 ikilinganishwa na wastani wa 7.2 mwaka 2013. Kuongezeka kwa pato la Taifa kumechangiwa na mambo makuu yafuatayo:-

i. Kuimarika kwa sekta ya huduma ambayo imekuwa kutoka asilimia 4.6 mwaka 2013 hadi asilimia 9.8 mwaka 2014;

ii. Kuimarika kwa sekta ya viwanda ambayo imekuwa kutoka asilimia 3.5 mwaka 2013 hadi asilimia 6.0 mwaka 2014;

iii. Kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini kutoka watalii 181,301 mwaka 2013 hadi kufikia watalii 311,891 mwaka 2014 sawa na ongezeko la asilimia 72; na

iv. Kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini.

Mhe. Spika, kuendelea kukuwa kwa uchumi wa Zanzibar kunatokana na juhudi za Serikali za kukuza uchumi kwa kutekeleza mipango, mikakati na sera mbali mbali za kiuchumi. Juhudi ambazo zitaendelezwa ili kuimarisha hali ya ustawi wa wananchi wa Zanzibar. Kama ilivyokwisha elezwa na Mhe. Waziri wa Fedha kwa mwaka ujao maeneo muhimu yatakayopewa kipaumbele na Serikali ni miundombinu na mawasiliano, huduma za kielimu, afya na pensheni kwa wazee waliofikia miaka 70 na zaidi.

**HUDUMA ZA JAMII**

Mhe. Spika, kuhusu huduma za jamii katika Awamu hii ya Saba, Serikali imechukua hatua mbali mbali za kuimarisha huduma za elimu, afya, maji safi na salama pamoja na makaazi ili kuleta ustawi mzuri kwa jamii. Kwa upande wa Sekta ya Elimu, Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuiimarisha na kuiendeleza elimu. Hatua hizo ni pamoja na ujenzi wa skuli na madarasa mapya kwa skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari, ununuzi wa samani pamoja na vitabu vya kiada, ziada na vya maktaba kwa skuli mbali mbali za Unguja na Pemba. Aidha, Serikali imeendelea kuwajengea uwezo walimu kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa lengo la kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa.

Mhe. Spika, hivi karibuni Serikali imetangaza rasmi kufuta michango yote iliyokuwa ikitolewa na wananchi kwa ajili ya elimu ya msingi ya watoto wao na kuondosha ada za mitihani kwa elimu ya sekondari. Uamuzi huu wa Serikali una lengo la kuwaondoshea wananchi hasa wa kipato cha chini mzigo wa kugharamia elimu ya watoto wao na kutoa fursa zaidi kwa watoto wetu kupata elimu na kujenga Taifa la watu walioelimika. Tunamshukuru Mhe. Rais kwa uamuzi huu wa Serikali yake ambao unawajali sana wananchi.

Mhe. Spika, Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha wanafunzi kujiunga na kuendelea na masomo ya elimu ya juu katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi kwa kuwapatia mikopo wale wote wanaokidhi vigezo

vya kupatiwa mikopo hiyo. Serikali itaendelea kutoa huduma hii ya mikopo ya elimu ya juu ili kufikia lengo la kuwa na wataalamu wazalendo katika fani mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za kinga na tiba katika hospitali na vituo vya afya pamoja na kutoa elimu ya afya kwa wananchi ili kujikinga na maradhi ya kuambukiza na yasio ya kuambukiza. Aidha, Serikali imezifanyia matengenezo makubwa hospitali na vituo vya afya na kujenga majengo mengine mapya Unguja na Pemba, ikiwemo wodi ya wagonjwa mahatuti *(ICU)* na kitengo cha huduma ya upasuaji vichwa na uti wa mgongo *(Neuro Surgical Unit)* katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, Serikali pia imechukua hatua za kuongeza madaktari na wahudumu wengine wa afya kwa kuwasomesha na kuwapatia uzoefu. Hivi sasa nchi yetu ina madaktari wazalendo wapatao 44 na madaktari bingwa wazalendo 13. Hii ni hatua kubwa sana kufikiwa na nchi yetu. Aidha, Serikali inawaendeleza madaktari 14 kuwa madaktari bingwa wa saratani, maradhi ya watoto, maradhi ya kina mama, upasuaji wa uti wa mgongo, maradhi ya mifupa na maradhi ya macho. Vile vile, kwa kushirikiana na nchi marafiki, Serikali imepatiwa madaktari bingwa wa maradhi mbali mbali kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Maji, Serikali imeendelea na juhudi zake za kuwapatia wananchi huduma bora ya maji safi na salama. Katika kutimiza lengo hilo, Serikali inaendelea kutekeleza programu na miradi mbali mbali ikiwemo uchimbaji wa visima, ujenzi wa matangi ya maji na uwekaji wa pampu na mota. Pia, kufanya matengenezo makubwa katika miundombinu ya usambazaji maji katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Serikali itaendelea kuwaelimisha wananchi athari ya kuviharibu na kuviziba vianzio vya maji ambavyo huweza kusababisha upungufu mkubwa wa maji nchini.

Mhe. Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa makaazi bora kwa wananchi wetu imeandaa Sheria ya *Condominium* ili kuwawezesha wananchi kumiliki sehemu ya majengo katika nyumba za maendeleo na kuunda bodi ya kusimamia utekelezaji wa Sheria hiyo. Aidha, Serikali imeandaa Sheria ya Shirika la Nyumba la Zanzibar ya mwaka 2014 ili kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba. Pia, Serikali inaufanyia mapitio Mpango Mkuu wa Mji wa Zanzibar na kutenga maeneo maalum ya ujenzi wa nyumba za ghorofa kwa lengo la kupunguza matumizi ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

## MASUALA MTAMBUKA

### Mazingira

Mhe. Spika, niseme kuhusu masuala ya MTAMBUKA. Kwanza mazingira, Mhe. Spika, utunzaji wa mazingira ni suala muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Nchi zote duniani zinatoa kipaumbele katika suala hili kwa maendeleo endelevu na kupunguza umasikini. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imekua ikihimiza wananchi kupanda miti kwa wingi na kuachana na tabia ya kukata miti ovyo na uchimbaji wa rasilimali zisizorejesheka kiholela. Aidha, wananchi wanaelimishwa kuachana na matumizi ya mifuko ya plastiki na kusafisha mazingira katika maeneo yao. Athari ya mafuriko yanayoikumba nchi yetu mara kwa mara kwa kiasi kikubwa yanatokana na uharibifu wa mazingira ikiwemo; uchimbaji wa mchanga kiholela, ujenzi wa nyumba katika maeneo ya mabondeni, kwenye njia za maji ya mvua na utupaji wa taka kiholela katika mitaro ya maji machafu.

### Mapambano Dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia

Mhe. Spika, tatizo la ukatili na udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto bado linaendelea kushamiri katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu licha ya jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kupambana na tatizo hilo. Katika jitihada za kuendelea na mapambano hayo, Serikali imeanzisha kamati za kupambana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia katika ngazi ya taifa hadi shehia pamoja na kuzijengea uwezo kamati hizo. Serikali pia inashirikiana na Asasi za Kiraia na Viongozi wa Dini katika mapambano hayo.

Kwa kutambua uzito wa tatizo hili, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein mnamo tarehe 6 Disemba, 2014, alizindua rasmi Kampeni ya Kitaifa ya "Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto Zanzibar Sasa Basi". Lengo la Kampeni hii ni kuona kwamba hakuna tukio lolote la ukatili la udhalilishaji wa wanawake na watoto litakalovumiliwa katika nchi yetu. Nachukua nafasi hii kuwaomba viongozi na wananchi wote kuwafichua wanaofanya maovu haya na kuyapiga vita kwa nguvu zetu zote.

### Mapambano dhidi ya Rushwa

Mhe. Spika, rushwa imekuwa donda ndugu na  ni adui mkubwa kwa maendeleo ya nchi yetu na ustawi wa jamii. Serikali inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti vitendo vya kutoa na kupokea rushwa kwa kuielimisha jamii kujua madhara ya rushwa na haja ya kuichukia na kuikataa rushwa. Aidha, Serikali imetunga Sheria ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi ya mwaka 2012 na kuanzisha

Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi. Serikali inaendelea kuijengea uwezo taasisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**Malengo na Utekelezaji wa Kazi za Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Miezi Tisa (Julai-Machi) 2014/2015**

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi) cha mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake imechukua juhudi kubwa katika kutekeleza malengo iliyojipangia na kufanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

**Ofisi ya Faragha**

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha kwa mwaka 2014/2015 imepanga na kutekeleza yafuatayo:-

## Malengo

- Kuimarisha Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais;
- Kuimarisha makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa kuzifanyia matengenezo nyumba za Mazizini, Dar-es-Salam na Dodoma;
- Kuratibu ziara 20 za ndani ya nchi na mbili (2) nje ya nchi za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais;
- Kuwajengea uwezo wafanyakazi wawili (2) wa Idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi pamoja na kulipia stahiki za likizo kwa wafanyakazi wanne (4); na
- Kuimarisha uhusiano na ushirikiano na nchi na Taasisi mbali mbali za ndani, Kikanda na Kimataifa.

**Utekelezaji**

- Ofisi ya Faragha imeratibu mikutano baina ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Mabalozi, Wanadiplomasia na Wageni mbali mbali kutoka nchi za nje na Mashirika ya Kimataifa. Mikutano hiyo imezidi kuimarisha uhusiano uliopo baina ya Zanzibar na nchi wanazotoka Wanadiplomasia na Wageni hao.

- Ofisi imeratibu vikao vya mazungumzo ya upatanishi na utatuzi wa migogoro mbali mbali ya ardhi. Vikao hivyo vimefanikisha kumaliza mgogoro wa wananchi wa Kiombamvua na Hoteli ya *Seacliff.*

- Ofisi ya Faragha imeratibu ziara 33 za ndani za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Ziara 29 zilihusisha Mikoa yote ya Zanzibar na ziara nne (4) kwa Mikoa ya Tanzania Bara. Madhumuni makuu ya ziara hizo yalikuwa ni kuonana na wananchi, kusikiliza matatizo yao na kukagua shughuli zao za maendeleo. Aidha, Ofisi imeratibu ziara mbili (2) za nje ya nchi, ziara hizo zilikuwa katika nchi za China na Zambia.

- Ofisi imeratibu ahadi 23 zilizotolewa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika mambo mbali mbali, kati ya hizo ahadi tisa (9) tayari zimetekelezwa. Ahadi zilizokuwa hazijatekelezwa zinaendelea kufanyiwa kazi na Taasisi mbali mbali zinazohusika.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 483,116,224 kwa Ofisi ya Faragha. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya shilingi 449,644,209 zimepatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 93.

**Idara ya Uendeshaji na Utumishi**

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka 2014/2015 imepanga na kutekeleza yafuatayo:-

**Malengo**

- Kuweka mazingira mazuri ya kazi za Idara kwa ununuzi wa vifaa vya ofisi, samani pamoja na kulipia gharama za umeme na mawasiliano na utunzaji wa majengo.

- Kuufanyia mapitio Mpango wa Mafunzo ya wafanyakazi pamoja kuandaa utaratibu wa kutathmini utendaji kazi (*Staff Appraisal System*) na upandishaji vyeo wafanyakazi kwa kufuata Muundo wa Utumishi (*Scheme of Service*).

- Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.
- Kusimamiamatumizi bora ya fedha na vifaa vya ofisi kwa kuandaa vikao vinne (4) vya Kamati ya Uongozi, Vikao vinne (4) vya Bodi ya Zabuni, vikao vinne vya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani na kulifanyia mapitio Daftari la Mali za Serikali (*Asset Registry).*

**Utekelezaji wa Malengo Hayo:**

- Jumla ya wafanyakazi 38 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika fani mbali mbali ndani na nje ya nchi ili kuwaongezea ujuzi na maarifa ya kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

- Idara imenunua vifaa na vitendea kazi mbali mbali kwa matumizi ya ofisi pamoja na kulipia gharama za uendeshaji wa ofisi kama vile maji, umeme na mawasiliano ya simu na *internet*.

- Idara imesimamia kwa mafanikio makubwa matumizi bora ya fedha na rasilimali kwa kuandaa vikao vitatu (3) vya Kamati ya Uongozi, vikao vinne (4) vya Bodi ya Zabuni, vikao vitatu (3) vya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani na kulifanyia mapitio Daftari la Mali za Serikali (*Asset Registry*).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 704,166,316 kwa Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya shilingi 584,539,975 zimepatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 83.

**Idara ya Mipango, Sera na Utafiti**

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka 2014/2015 imepanga na kutekeleza yafuatayo:-

**Malengo:**

- Kuratibu vikao 12 vya Kamati ya Kisekta ya kuidhinisha tafiti mbali mbali na vikao vinne (4) vya Kamati ya Taifa ya Kutafiti Rasilimali za Asili.

- Kuratibu utekelezaji wa Miradi ya Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria kupitia Mfuko wa Dunia (*Global Fund).*

- Kuandaa bajeti nakutayarisha Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kufanya ziara nne (4) za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu/ Miradi ya Maendeleo.

- Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati (*SP*) 2012-2014 wa Ofisi Makamu wa Pili wa Rais.

- Kuwajengea uwezo wafanyakazi 11 wa idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi watatu (3) muda mrefu na kulipa stahiki za likizo za wafanyakazi watatu (3).

- Kwa kushirikiana na *COSTECH* kuwajengea uwezo watafiti wa Wizara za SMZ kwa kuandaa warsha mbili (2) pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa utoaji wa vibali vya utafiti.

**Utekelezaji**

- Idara imeandaa mafunzo ya bajeti inayozingatia programu (*PBB*) yaliyowashirikisha Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Maafisa Mipango na Wahasibu wa Ofisi/Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

- Idara imefanya vikao vitatu vya Kamati ya Utafiti ya Kisekta, vikao hivyo vilipokea na kupitisha maombi 10 ya utafiti.

- Idara ilifanya semina huko Pemba, semina hiyo ilihusu masuala ya utafiti na iliwashirikisha maofisa utafiti, maafisa Mipango wa Wizara, wakuu wa vituo vya utafiti, *NGO*'s zinazojishughulisha na masuala ya utafiti na vyuo vilivyopo Pemba.

- Idara imeandaa Taarifa za Utekelezaji kwa kipindi cha miezi sita (6) Julai - Disemba na taarifa ya Utekelezaji miezi mitatu (Oktoba – Disemba) pamoja na kutayarisha Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (*MTEF*) wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

- Idara imeufanyia mapitio Mpango Mkakati (*SP*) wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 184,007,400 kwa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya shilingi 134,207,903 zimepatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 73.

**Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali**

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015 imepanga na kutekeleza yafuatayo:-

**Malengo**

- Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanyakazi wanne (4) pamoja na kulipia stahiki za likizo kwa wafanyakazi saba (7).

- Kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na kuandaa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia Oktoba, 2010 – Mei, 2015.

- Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo katika majimbo 50 ya Unguja na Pemba ambayo yamepatiwa fedha.

- Kusimamia utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) Awamu ya Tatu kuhusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kwa Unguja na Pemba.

- Kushughulikia malalamiko na migogoro ya wananchi kwa kushirikiana na sekta husika.

- Kuratibu masuala ya Muungano.

- Kuimarisha Kitengo cha *ICE* kwa ununuzi wa vifaa kutoa mafunzo kwa watendaji na kusimamia Tovuti ya Serikali.

- Kufuatilia mijadala na utekelezaji wa ahadi za serikali zinazotolewa katika vikao vya Baraza la Wawakilishi.

- Kuratibu vikao saba (7) vya mashirikiano na vikao vinne (4) vya Mawaziri na Makatibu Wakuu wa SMZ na SMT na vikao vinne (4) vya Sekreterieti ya Kamati ya Pamoja ya Mambo ya Muungano.

**Utekelezaji wa Malengo hayo**

- Mhe. Spika, idara imeandaa Rasimu ya Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kipindi cha miaka mitano (2010-2015).

- Idara imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi midogo midogo ya wananchi kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo

katika Majimbo 32 ya Unguja na kukagua usahihi wa akaunti za mfuko huo katika Majimbo kumi (10) kati ya 18 ya Pemba. Aidha, idara imefuatilia marejesho ya matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa mwaka 2013/2014. Kufuatia ufuatiliaji huo, jumla ya Majimbo manane (8) yamefanya marejesho hadi kufikia Machi, 2015. Majimbo hayo ni Donge, Kitope, Matemwe, Dimani, Makunduchi, Mtoni, Koani kwa Unguja na Chambani kwa Pemba.

- Kuhusu masuala ya Muungano, Idara imeratibu vikao vitano (5) vya mashirikiano baina ya Wizara za SMZ na SMT. Vikao hivyo ni baina ya Kamati ya Wanasheria Wakuu wa SMT na SMZ; Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati SMZ na Wizara ya Nishati na Madini SMT; Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma SMZ na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma SMT; Wizara ya Mifugo na Uvuvi SMZ na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi SMT; na Wizara za Fedha za SMZ na SMT. Aidha, Ofisi imeratibu vikao vinne (4) vya Sekretarieti ya mambo ya Muungano.

- Idara imesimamia utekelezaji wa Mpango wa *TASAF III* kwa Kunusuru Kaya Masikini. Mpango huo umefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

    i. Imefanikisha zoezi la kuibua miradi ya kutoa ajira ya muda kwa Kaya maskini na kuanza utekelezaji wa miradi hiyo katika Shehia 40 za awali kwa Unguja na Pemba.

    ii. Imeandaa mikutano kwa wajumbe 76 wa Kamati za Uongozi na Kamati za Usimamizi wa Mpango wa *TASAF III* kwa Unguja na Pemba kwa lengo la kuwapatia uelewa wajumbe hao kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini pamoja na taarifa za Mpango Kazi zilizoandaliwa.

    iii. Usanifu wa miradi ya kutoa ajira ya muda kwa kaya masikini umefanyika. Jumla ya miradi 77 (Unguja 33 na Pemba 44) imefanyiwa usanifu na imetekelezwa katika siku 60 za mwaka wa kwanza. Miradi hiyo inahusiana na vitalu vya miti ya matunda na misitu, upandaji wa miti ya mikoko, barabara za ndani, usafi wa mazingira na ujenzi wa tuta la kuzuwia maji ya bahari. Jumla ya shilingi 649,735,200

(Unguja 228,224,400 na Pemba 421,510,800) zimelipwa kwa kaya masikini 6,598 (Unguja 2,432 na Pemba 4,166) kwa miezi mitatu ya Disemba, Januari na Febuari. Aidha, kaya hizo masikini zimelipwa ruzuku ya msingi na masharti ya jumla ya shilingi 1,115,393,537 (Unguja 404,863,884 na Pemba 710,529,653) katika kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi).

iv. Uibuaji wa Kaya masikini katika Shehia 90 (Unguja 58 na Pemba 32) kwa ajili ya kufanyiwa Tathmini ya Matokeo (*Impact Evaluation*) chini ya Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini umefanyika. Tathmini hiyo inafanyika kwa mashirikiano baina ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na *TASAF* Makao Makuu.

v. Uandikishaji wa Kaya Masikini katika Shehia 51 mpya (Unguja Shehia 31 na Pemba Shehia 17) umefanyika. Jumla ya Shehia 103 mpya (Unguja 68 na Pemba 35) zinatarajiwa kuingizwa katika Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kuanzia mwaka huu wa 2015.

- Idara ya Uratibu, imekiimarisha Kitengo cha Habari, Mawasiliano na Elimu (*ICE*) kwa kuwapatia mafunzo maafisa wanne wa kitengo hicho na kupatiwa vifaa, ikiwemo kompyuta. Hili limefanyika kwa mashirikiano na *UNDP* kupitia Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi za Viongozi Wakuu wa SMZ.

- Idara imeendelea kuratibu utekelezaji wa ahadi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa zilizotolewa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba wakati wa ziara zilizofanywa na viongozi hao. Jumla ya ahadi 14 zimeratibiwa. Kati ya hizo, ahadi nane (8) zimeshatekelezwa na sita (6) zinaendelea na hatua ya kutekelezwa.

- Idara imeshughulikia jumla ya malalamiko26 kwa kushirikiana na sekta husika. Malalamiko hayo yanahusiana na ardhi (15) na mambo mengine (11).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 344,638,000 kwa Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya shilingi 231,909,954 zimepatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 67.

**Idara ya Uratibu Dar es Salaam**

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu Dar es Salaam kwa mwaka 2014/2015 imepanga na kutekeleza yafuatayo:-

**Malengo**

- Kuweka mazingira mazuri ya kazi za Idara kwa ununuzi wa vifaa vya ofisi na samani.
- Kuwapatia mafunzo wafanyakazi watatu (3) wa Idara pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi tisa (9).
- Kuandaa muundo mpya wa kitaasisi wa kiutumishi wa Idara utakaoleta ufanisi na tija.
- Kuimarisha mashirikiano baina ya Idara na Taasisi za SMZ na za SMT, Ofisi za Kibalozi na Taasisi za Kimataifa

**Utekelezaji**

- Idara imeshiriki mkutano wa wadau wa uhamasishaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Viwanda vya Madawa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- Idara imeshiriki katika kikao cha maandalizi ya majadiliano baina ya Serikali ya Tanzania na Japan kuhusu ufadhili wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/2016.
- Idara imeanza maandalizi ya kuandaa muundo mpya wa Kitaasisi na Kiutumishi wa Idara.
- Idara imenunua vifaa vya kutendea kazi, kulipia huduma za ofisi (maji, umeme, mawasiliano) na kulipia stahiki za likizo za wafanyakazi tisa (9).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 353,178,160 kwa Idara ya Uratibu, Dar es Salaam. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya shilingi 181,504,731 zimepatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 51.

**Idara ya Kukabiliana na Maafa**

Mhe. Spika, Idara ya Kukabiliana na Maafa kwa mwaka 2014/2015 imepanga na kutekeleza yafuatayo:-

**Malengo**

- Kujenga uwezo kwa jamii katika kukabiliana na majanga na maafa kwa shehia 10.

- Kuyafanyia matengenezo maghala mawili (2) na kununua vifaa vya kukabiliana na maafa Unguja na Pemba.

- Kukamilisha Sheria ya Kukabiliana na Maafa.

- Idara kwa Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo (*USAFRICOM*, Benki ya Dunia na Kamisheni ya Bahari ya Hindi) itaendesha mafunzo mbali mbali ya kukabiliana na maafa kwa watendaji na wadau pamoja na kuendesha mazoezi mawili (2) (*Simulation Exercise*) ya kukabiliana na maafa.

- Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanyakazi wanne (4) na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi sita (6).

**Utekelezaji**

- Idara imeendesha zoezi la Kimataifa la Kukabiliana na Maafa (*Simulation Exercise*) lililoshirikisha wadau mbali mbali ambapo jumla ya watu 100 wameshiriki katika zoezi hilo.

- Pia, idara imejenga uwezo kwa jamii katika kukabiliana na maafa na namna ya kupunguza athari zake kwa kutoa mafunzo kwa Shehia 30 kwa Wilaya za Mjini, Magharibi, na Kaskazini “A” kwa Unguja na Wilaya ya Chake Chake kwa Pemba. Aidha, Idara imetoa elimu kupitia vipindi vya redio katika Shirika la Utangazaji Zanzibar na kuunda Kamati za Maafa kwa Shehia zilizopatiwa mafunzo.

- Idara imetoa mafunzo ya kujikinga na Kukabiliana na Maafa kwa walimu 265 wa Skuli za Serikali na Binafsi wa Wilaya za

Mjini, Magharibi na Kaskazini ‘A’ kwa Unguja na Wilaya ya Wete na Micheweni kwa Pemba.

- Idara imefanya tathmini na uchambuzi wa awali kwa hali ya maafa kwa Shehia 30 katika Wilaya za Kaskazini ‘B’ na Kati kwa Unguja na Wilaya za Chake Chake na Wete kwa Pemba.

- Idara imeendesha semina ya siku moja ya Kujikinga na kukabiliana na maafa kwa Viongozi 50 wa Vyama vya Siasa 22 vilivyosajiliwa.

- Idara imesambaza Kitabu cha Nyenzo za Usimamiaji na Ufuatiliaji wa Sera ya Kukabiliana na Maafa kwa wadau mbali mbali wa Maafa kwa Unguja na Pemba.

- Idara imezifanyia matengenezo makubwa ghala ya kuhifadhia vifaa vya Kukabiliana na Maafa Unguja na Pemba.

- Idara imesambaza Mkakati wa Ufuatiliaji Rasilimali za Kukabiliana na Maafa kwa wadau mbali mbali wa Maafa Unguja na Pemba.

- Idara imefanya mkutano wa Kitaifa(*Platform*) uliowashirikisha wadau mbali mbali wa maafa.

- Idara imekamilisha utayarishaji wa Sheria mpya ya Kukabiliana na Maafa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi 298,447,800 kwa Idara ya Kukabiliana na Maafa. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya Shilingi 196,518,500 zimepatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 66.

**Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa**

Mhe. Spika, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kwa mwaka 2014/2015 imepanga na kutekeleza yafuatayo:-

**Malengo**

- Kuratibu na kusimamia Sherehe za Miaka 51 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

- Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanyakazi wawili pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi wawili (2).

- Kuratibu Sherehe za Miaka 51 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na ushiriki wa viongozi na wananchi wa Zanzibar katika Sherehe za Miaka 53 za Uhuru wa Tanganyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu.

- Kuifanyia mapitio Sheria namba 10 ya 2002 ya kuwaenzi viongozi pamoja na mambo yanayohusiana nayo.

- Kuendelea kukusanya na kutunza kumbukumbu za Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume.

- Kuratibu Hitma na Dua ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume (Siku ya Mashujaa).

**Utekelezaji**

- Idara imeratibu Sherehe za Miaka 51 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa mafanikio makubwa. Aidha, Ofisi imesimamia kilele cha Sherehe hizo zilizofanyika tarehe 12 Januari, 2015, Uwanja wa Amaan.

- Idara kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania imeanza maandalizi ya kujenga kaburi la Marehemu Sheikh Idrisa Abdulwakil huko Makunduchi na kufanya matengenezo ya kaburi la Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume hapo Kisiwandui.

- Idara imeratibu maandalizi ya Sherehe za miaka 51 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar za tarehe 26 Aprili, 2015, Dar es Salaam.

- Idara imeratibu maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Mashujaa Zanzibar (*Karume Day*) ya tarehe 7 Aprili, 2015.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 871,615,500 kwa Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya Shilingi 1,358,989,717 zimepatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 156.

**Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali**

Mhe. Spika, Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa mwaka 2014/2015 imepanga na kutekeleza yafuatayo:-

**Malengo**

- Kuweka mazingira mazuri ya kazi za idarakwa ununuzi wa vifaa vya ofisi na samani.
- Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi wafanyakazi watano (5) na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi saba (7).
- Kutoa huduma za uchapishaji nyaraka na sheria za serikali.
- Kutangaza huduma za kiwanda kwa ajili ya kuongeza idadi ya wateja na mapato.
- Kukamilisha utaratibu wa kuanzisha Bohari Kuu ya Serikali ya vifaa vya ofisi.

**Utekelezaji**

- Idara imetayarisha Rasimu ya Sheria inayokipa mamlaka Kiwanda cha Upigaji chapa iwe taasisi inayojitegemea.
- Idara imenunua vitendeakazi na kulipia huduma za ofisi zikiwemo maji, umeme, mawasiliano na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi saba (7).
- Idara kupitia Kiwanda cha Upigaji Chapa imefanikiwa kuchapisha nyaraka na machapisho mbali mbali ya serikali kama vile Gazeti Rasmi la Serikali, Miswaada ya Sheria, Sheria na machapisho mengine yaliyowasilishwa kiwandani kwa mujibu wa mahitaji ya taasisi husika.
- Idara imeendelea na zoezi la kuzihamisha nyaraka zilizoko Saateni katika jengo la zamani la Kiwanda cha Uchapaji na kuzipeleka Maruhubi. Nyaraka zote zimehifadhiwa vizuri na ziko salama.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 482,066,600 kwa Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu

wa Serikali. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya Shilingi 392,018,845 zimepatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 81.

**Baraza la Wawakilishi**

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2014/2015 limepanga na kutekeleza yafuatayo:-

**Malengo**

- Kujenga mazingira mazuri kwa kuwezesha kufanyika kwa mikutano minne (4) ya Baraza la Wawakilishi pamoja na kazi za Kamati katika kufuatilia shughuli za serikali na kusimamia uwajibikaji wake.

- Kutoa mafunzo na kuongeza uwezo wa kitaalamu kwa Wajumbe na wafanyakazi wa Baraza.

- Kutoa taaluma kwa wananchi kuhusu utendaji wa shughuli za Baraza kupitia Vyombo vya Habari.

- Kuimarisha mahusiano kati ya Baraza na Mabunge mengine ya Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola.

**Utekelezaji**

- Baraza la Wawakilishi limefanya mikutano mitatu ambayo ni mkutano wa 17, 18 na 19. Katika mikutano hiyo jumla ya Miswada 12 iliwasilishwa, kujadiliwa na kupitishwa. Jumla ya maswali ya misingi 169 na nyongeza 398 yaliulizwa na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri.

- Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilifanya kazi zake za kuisimamia serikali na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za serikali na kuwasilisha ripoti zao katika Mkutano wa 19 wa Baraza la Wawakilishi ambapo zilipokelewa na kujadiliwa. Aidha, serikali kupitia kila wizara iliwasilisha ripoti za utekelezaji wa maagizo ya Kamati za Baraza yaliyotokana na ripoti za Kamati za Kudumu za mwaka 2013/2014.

- Baraza lilipokea ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka za Serikali ambayo ilijadiliwa na Baraza kutoa ushauri na maagizo kwa serikali.

- Ofisi ya Baraza imefanya semina kwa asasi za kiraia, waandishi wa habari pamoja na wafanyakazi wa Baraza juu ya taratibu za ushirikishwaji wa wadau katika kazi za Kamati za Baraza.

- Wanasheria saba (7) wa Baraza wamepatiwa mafunzo ya siku tano (5) kuhusu uandishi na kutafsiri sheria. Mafunzo hayo yalitolewa kupitia Taasisi ya Sheria ya Kimataifa ya Uganda.

- Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji Zanzibar (Redio na *TV*) linaendelea kurusha moja kwa moja (*alive*) vikao vya Baraza la Wawakilishi. Aidha, Baraza limekuwa likitoa taaluma kwa umma kupitia kipindi chake cha LIJUE BARAZA LA WAWAKILISHI kipindi ambacho pia hurushwa kupitia Shirika hilo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 14,564,000,000 kwa Baraza la Wawakilishi. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya Shilingi 13,954,901,100 zimepatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 95.

**Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar**

Mhe. Spika, Aidha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mwaka 2014/2015 imepanga na kutekeleza yafuatayo:-

**Malengo**

- Kuweka mazingira mazuri ya kazi za Tume kwa ununuzi wa vifaa vya Ofisi na samani.

- Kuwajengea uwezo wafanyakazi watatu (3) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 15 mafunzo ya muda mfupi pamoja na kulipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi sita.

- Kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

- Kufanya uchunguzi wa idadi, majina na mipaka kwa Majimbo yote 50 ya Uchaguzi.

- Kusimamia na kuendesha Kura ya Maoni ya Kuthibitisha Katiba Inayopendekezwa.

- Kufanya matayarisho ya jumla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

**Utekelezaji**

- Tume ya Uchaguzi, imefanya matengenezo makubwa ya Ofisi ya Wilaya ya Mjini kwa kuweka ukuta wa kizuizi na matengenezo ya ukumbi wa mkutano. Kwa upande wa Pemba, Tume imefanya matengenezo makubwa ya Ofisi ya Wilaya ya Wete pamoja na kununua vifaa na samani kwa ajili ya ofisi zote mbili.

- Tume ya Uchaguzi imefanya mapitio ya Kanuni, miongozo na maadili mbali mbali ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za uchaguzi. Miongozo hiyo ni kama vile; Maadili ya Vyama vya Siasa, Maadili ya Waangalizi wa Uchaguzi na Muongozo wa Uteuzi kwa Wagombea.

- Tume ya Uchaguzi inaendelea na kazi za matayarisho ya vielelezo vya kutoa elimu ya wapiga kura. Aidha, Tume imekamilisha muongozo kwa ajili ya kutoa elimu ya Wapiga Kura kwa Asasi na Taasisi ambazo zinataka kutoa elimu hiyo.

- Tume ya Uchaguzi inaendelea na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015. Katika maandalizi hayo Tume ilikutana na Vyama vya Siasa na wadau wa uchaguzi Unguja na Pemba. Katika mikutano hiyo, mambo mbali mbali kuhusu Uchaguzi Mkuu yalijadiliwa. Pia, Tume ilitangaza rasmi ratiba ya Uchaguzi Mkuu.

- Tume ya Uchaguzi inaendelea na kazi ya mapitio ya idadi, mipaka na majina ya majimbo ya uchaguzi na inatarajia kutangaza majina na mipaka mipya ya majimbo hayo baada ya kazi hiyo kukamilika.

- Tume ya Uchaguzi imekamilisha Kanuni za Kura ya Maoni na miongozo ya utoaji wa elimu ya uraia na elimu ya Wapiga Kura. Aidha, Tume imetoa vibali kwa asasi za kiraia 61 kati ya asasi 75 zilizoomba kutoa elimu ya uraia kwa Zanzibar.

- Tume ya Uchaguzi imekamilisha uandaaji wa Mpango wa Manunuzi ya Vifaa (*Procurement Plan*) kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu. Tume inatarajia kutangaza zabuni ya ununuzi wa vifaa hivyo katika Mwezi wa Mei, 2015.

- Tume ya Uchaguzi imefanya mapitio ya Sheria ya Kura ya Maoni ya mwaka 2010 ili kurahisisha utekelezaji wake.

- Tume kwa kushirikiana na *“UN Women”,* imeandaa Rasimu ya Sera ya Ushirikishwaji wa Makundi Maalum katika Uchaguzi (*Gender Mainstreaming and Social Inclusion Policy).*

- Tume imefanya uchambuzi yakinifu wa mifumo yauandikishaji wa Wapiga Kura pamoja na vifaa vya uandikishaji wa wapiga kura.

- Tume imeandaa mpango wa utekelezaji, ratiba ya uchaguzi pamoja na bajeti kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

- Tume imewapatia watendaji wake sita (6) ziara ya mafunzo ya siku tatu (3) nchini Kenya kwa ajili ya kujifunza masuala ya uendeshaji wa uchaguzi.

- Tume ya Uchaguzi imewapatia mafunzo watendaji wa Kitengo cha *IT* ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma kitaalamu. Aidha, maandalizi yameanza ya kutengeneza upya Tovuti ya Tume pamoja na kuweka taarifa mbali mbali zinazohusiana na uchaguzi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi 1,314,100,000 kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Hadi kufikia Machi, 2015 jumla ya Shilingi 1,229,926,569 zimepatikana na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 94.

**Utekelezaji wa Kifedha**

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi 2014/2015), Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilipanga kutumia jumla ya Shilingi 4,110,200,000 kwa kazi za kawaida. Fedha zilizopatikana na kutumika ni shilingi 3,801,401,484 sawa na asilimia 92. **Angalia Kiambatisho Nam.1.** Aidha, kwa upande wa Miradi ya maendeleo Ofisi ilipanga kutumia jumla ya Shilingi 90,000,000 na hadi kufikia mwezi Machi jumla ya Shilingi 45,000,000 zimepatikana na kutumika sawa na asilimia 50 ya fedha zilizopangwa. **Angalia Kiambatisho Nam. 2.**

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi katika kipindi hicho ilipanga kutumia Shilingi 14,564,000,000 kwa kazi za kawaida na fedha zilizopatikana ni Shilingi 13,954,901,100 sawa na asilimia 96. **Angalia Kiambatisho Nam. 1.**

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi Zanzibar katika kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi) 2014/2015 ilipanga kutumia Shilingi 1,314,100,000 kwa kazi za kawaida na fedha zilizopatikana ni Shilingi 1,229,926,569 sawa na asilimia 94. **Angalia Kiambatisho Nam. 1.**

**Ukusanyaji wa mapato**

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais  inakusanya mapato kutoka katika Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Katika kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi 2014/2015), Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 450,000,000. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2014 ofisi imekusanya jumla ya Shilingi 295,903,000 sawa na asilimia 66 ya lengo.

Aidha, kwa upande wa Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 2,250,000. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2015 imekusanya Shillingi 11,940,000 sawa na asilimia 530. Kwa upande wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilipangiwa kukusanya Shilingi 3,750,000 ikiwa ni makusanyo ya kodi ya ukumbi wa jengo la zamani la Baraza la Wawakilishi. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2015, hakukuwa na fedha yoyote iliyokusanywa. Hali hii imetokana na ukumbi huo kukosa kukodishwa kwa vile uko katika hali isiyoridhisha na unahitaji matengenezo makubwa na kuwekwa vifaa vya kisasa. **Angalia Kiambatisho Nam. 3.**

**BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

Mhe. Spika, serikali inaendelea kufanya mageuzi ya bajeti ikiwa ni sehemu ya mageuzi ya utawala na udhibiti wa fedha za umma. Kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016 serikali imetoka katika mfumo wa bajeti unaotumia vifungu (*line item*) na kwenda katika mfumo wa bajeti unaotumia *program.*

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake ina programu nane (8) na programu ndogo 13 zinazohusisha malengo, na matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika *program* na *program* ndogo kama ifuatavyo:-

**Programu ya Kwanza (C011): Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais.**

Mhe. Spika, lengo la programu hii ni kuimarisha utendaji wa kazi kwa Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais. Matokeo yanayotarajiwa ni kuimarika kwa ofisi hii na kutoa huduma bora kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Huduma

inayotolewa katika Ofisi ya Faragha ni kuratibu kazi mbali mbali za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais ikiwemo ziara za ndani na nje ya nchi, mikutano na Mabalozi wa nchi mbali mbali, Wawakilishi wa Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa na mikutano mbali mbali na wananchi kusikiliza kero na malalamiko yao. Programu hii inatekeleza lengo la tatu katika *klasta* ya tatu ya MKUZA II inayohakikisha ushirikishwaji wa wananchi katika Utawala wa Kidemokrasia. Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais.

**Programu ya Pili (C012): Uratibu wa shughuli za serikali.**

Mhe. Spika, programu hii lengo lake kubwa ni kuweka mfumo imara na endelevu kwa Uratibu wa Shughuli za Serikali. Programu hii inatekeleza lengo la tatu katika *klasta* ya tatu ya MKUZA II la kuhakikisha ushirikishwaji wa wananchi katika utawala wa kidemokrasia. Aidha, Programu hii ina programu ndogo tatu zifuatazo:-

i. **Programu Ndogo (C0121): Uratibu wa Shughuli za Kukabiliana na Maafa.**

Mhe. Spika, Programu hii ndogo lengo lake kuu ni kujenga uhimili kwa jamii katika kukabiliana na maafa. Matokeo yanayotarajiwa ni kutoa huduma bora kabla, wakati na baada ya maafa. Huduma inayotolewa ni Uratibu wa Shughuli mbali mbali za kukabiliana na maafa ikiwemo kutoa mafunzo kwa jamii, kuwahudumia waathirika wa majanga na maafa na kuandaa na kutoa miongozo mbali mbali inayosimamia utekelezaji wa kazi za maafa. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Kukabiliana na Maafa.

ii. **Programu Ndogo (C0122): Uratibu wa Shughuli za Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa.**

Mhe. Spika, Programu hii ndogo lengo lake ni kuwa na sherehe zenye hadhi na kudumisha historia na kumbukumbu za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Matokeo yanayotarajiwa ni ubora na ufanisi wa sherehe na maadhimisho ya kitaifa na kuwa na kumbukumbu zenye kuelezea historia za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Huduma inayotolewa ni Uratibu wa shughuli za Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa.

iii. **Programu ndogo (C0123): Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).**

Mhe. Spika,  lengo kuu la Programu hii ndogo ni kuimarika kwa utekelezaji wa shuguli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mambo ya Muungano na Uratibu wa Shughuli za Serikali, Dar es Salaam kupitia sekta mbali mbali. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwa na utekelezaji wa ufanisi kwa malengo ya Serikali. Huduma inayotolewa ni Uratibu wa Shughuli za Serikali (SMZ) ikiwemo kukusanya taarifa za utekelezaji wa shughuli za Serikali. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali Zanzibar na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali Dar es Salaam.

**Programu ya Tatu (C013): Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa.**

Mhe. Spika,  lengo kuu la Progrmu hii ni kuimarisha huduma za upigaji chapa. Matokeo yanayotarajiwa ni kutoa machapisho bora na kwa wakati. Kiwanda cha Upigaji Chapa kinatoa huduma za kuchapisha nyaraka mbalimbali za Serikali zikiwemo Hotuba za Bajeti za Wizara mbali mbali, vyeti vya kuzaliwa, Gazeti Rasmi la Serikali, Miswada ya Sheria na Sheria na Machapisho mengine. Programu hii inatekeleza lengo la Tatu katika klasta ya Tatu ya MKUZA II la kuhakikisha uimarishaji wa Demokrasia na Utawala bora. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

**Programu ya Nne (C014): Mipango na Utawala.**

Mhe. Spika,  lengo la Programu hii ni kuimarisha mazingira bora ya wafanyakazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi. Matokeo yake ni kuimarika kwa utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wafanyakazi na wadau mbali mbali wa Ofisi hii. Programu hii itatekeleza lengo la tatu katika klasta ya tatu ya MKUZA II la kuimarisha utawala wa sheria wenye kuheshimu haki za binaadamu na upatikanaji wa haki za sheria. Programu hii ina Programu ndogo tatu (3) zifuatazo:-

**i. Programu ndogo (C0141): Uongozi na Utawala.**

Mhe. Spika,  Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha na kusimamia utendaji kazi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Matokeo yanayotarajiwa ni matumizi bora ya rasilimali, wafanyakazi wenye ujuzi na uzoefu na ufanisi katika utendaji kazi.  Huduma zinazotolewa ni kutoa huduma za Utumishi na Uendeshaji, ikiwemo stahiki mbali mbali na kuwapatia mafunzo na vitendea kazi wafanyakazi. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

**ii. Programu ndogo (C0142): Mipango, Sera na Utafiti.**

Mhe. Spika, Programu hii ndogo ina lengo la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango na Bajeti na kufuatilia utekelezaji wa *Program*/Miradi ya Maendeleo

ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwa na mipango endelevu na yenye kuleta maendeleo. Huduma inayotolewa ni kuratibu uandaaji na kusimamia utekelezaji wa mipango, sera na bajeti. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

**iii. Programu ndogo (C0143): Ofisi Kuu Pemba.**

Mhe. Spika, lengo kuu la Program hii ndogo ni kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba. Matokeo yanayotarajiwa ni utendaji na utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba kwa ufanisi. Huduma inayotolewa ni kuratibu kazi zote za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba.

Mhe. Spika, vile vile, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inaratibu shughuli za Baraza la Wawakilishi na Tume ya Uchaguzi ambazo nazo zina Programu Kuu na Programu Ndogo kama ifuatavyo:-

**Baraza la Wawakilishi:**

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi lina Program mbili (2)

**Programu ya kwanza (C021): Kutunga Sheria, kupitisha Bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali:**

Mhe. Spika, lengo la Programu hii ni kuhakikisha haki na utawala wa sheria unatelekelezwa Zanzibar. Matokeo yanayotarajiwa ni kukua kwa demokrasia na uwakilishi wa wananchi. Programu hii itatekeleza lengo la tatu katika klasta ya tatu ya MKUZA II la kuimarisha utawala wa sheria wenye kuheshimu haki za binaadamu na upatikanaji wa haki za sheria. Huduma zinazotolewa ni kujadili, kurekebisha na kupitisha miswada ya Sheria, kusimamia utendaji wa taasisi za Serikali na kupitisha bajeti ya Serikali.

**Programu ya Pili (C022): Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi:**

Mhe. Spika, lengo la Programu hii ni kuweka mazingira mazuri ya kazi, kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Ofisi ya Baraza. Matokeo yanayotarajiwa ni kuongezeka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa ufanisi. Programu hii itatekeleza lengo la tatu katika *klasta* ya tatu ya MKUZA II la kuimarisha utawala wa sheria wenye kuheshimu haki za binaadamu na upatikanaji wa haki za sheria. Huduma zinazotolewa ni kuwapatia Wajumbe na wafanyakazi wa Baraza huduma na stahiki zao, kuimarisha uwezo wa Wajumbe na watendaji na kuimarisha mazingira ya kazi ya Ofisi ya Baraza.

**Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar:**

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ina Program mbili (2) na Programu ndogo tatu (3)

**Programu ya Kwanza (C031): Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi.**

Mhe. Spika, lengo la Programu hii ni kukuza demokrasia na umoja wa kitaifa. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwa na uchaguzi huru na wa haki na wenye kufuata misingi ya kisheria. Programu hii itatekeleza lengo la tatu katika *klasta* ya tatu ya MKUZA II la kuimarisha utawala wa sheria wenye kuheshimu haki za binaadamu na upatikanaji wa haki za sheria. Huduma zinazotolewa ni kufanya Uchaguzi Mkuu, Chaguzi ndogo na Kura ya maoni, Kufanya Uchambuzi wa Idadi, Majina na Mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi, Kuratibu na kutoa Elimu ya Wapiga Kura na Uandikishaji wa Wapiga Kura na Uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

**Programu ya Pili (C032): Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.**

Mhe. Spika, lengo la Programu hii ni kuimarisha Usimamizi wa mwenendo wa Shughuli za uchaguzi. Matokeo yanayotarajiwa ni uendeshaji bora wa kazi za Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Programu hii itatekeleza lengo la tatu katika *klasta* ya tatu ya MKUZA II la kuimarisha utawala wa sheria wenye kuheshimu haki za binaadamu na upatikanaji wa haki za sheria. Programu hii ina Programu ndogo mbili (2) zifuatazo;

i. **Programu ndogo (C0321): Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.**

Mhe. Spika, lengo la Programu hii ndogo ni kuimarisha Usimamizi wa mwenendo wa Shughuli za Uchaguzi. Matokeo yanayotarajiwa ni uendeshaji bora wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Huduma zinazotolewa na programu hii ndogo ni kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi, kuimarisha maslahi ya wafanyakazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

ii. **Programu ndogo (C0322): Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi Ndogo ya Tume ya Uchaguzi Pemba.**

Mhe. Spika, lengo la Programu hii ndogo ni kuimarisha Usimamizi wa mwenendo wa Shughuli za Uchaguzi. Matokeo yanayotarajiwa ni uendeshaji bora wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Huduma zinazotolewa na programu hii ndogo ni kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi ya Tume ya Uchaguzi Pemba. Kwa

muhtasari wa Programu hii na Programu ndogo za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake **Angalia Kiambatisho Nam. 4.**

**MGAO WA FEDHA KWA PROGRAMU:**

Mhe. Spika, mgao wa fedha kwa Programu za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake ni kama ifuatavyo:-

Programu: Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais. Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Jumla ya Shilingi 625,569,000 zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii.

Programu: Uratibu wa Shughuli za Serikali: Programu hii inajumuisha Idara ya Kukabiliana na Maafa, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali na Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam. Jumla ya Shilingi 2,239,727,000 zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha program hii.

Programu: Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa: Programu hii inatekelezwa na Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Jumla ya Shilingi 714,050,000 zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii.

Programu: Mipango na Utawala. Programu hii inajumuisha Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi Kuu Pemba. Jumla ya Shilingi 1,587,354,000 zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha program hii.

Mhe. Spika, kwa upande wa Baraza la Wawakilishi, mgao wa fedha kwa Programu ni kama ifuatavyo:-

Programu: Kutunga Sheria, kupitisha bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali. Makisio ya fedha kwa program hii ni Shilingi 6,539,295,000 zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha programu hii.

Programu: Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi. Programu hii inajumuisha kazi za utawala kwa Baraza la Wawakilishi Unguja na Pemba. Jumla ya Shilingi 10,223,305,000 zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza program hii. **Angalia Kiambatisho Nam. 5.**

Mhe. Spika, kwa upande wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, mgao wa fedha kwa Programu ni kama ifuatavyo:-

**Programu: Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi. Makisio ya fedha kwa program hii yanaainishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.**

Programu: Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji. Programu hii inajumuisha kazi za utawala kwa Tume ya Uchaguzi Unguja na Pemba. Jumla ya Shilingi 1,404,000,000 zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza programu hii.

Mhe. Spika, jumla ya gharama kwa Programu zote za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Baraza la Wawakilishi na Tume za Uchaguzi Zanzibar ni Shilingi 23,333,300,000.

**UKUSANYAJI MAPATO:**

Mhe. Spika, kwa upande wa mapato kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imepanga kukusanya mapato ya jumla ya Sh. 612,360,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

| | |
|---|---|
| Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali | Sh. 600,000,000 |
| Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | Sh. 12,360,000 |
| **Jumla** | **Sh.612,360,000** |

Mhe. Spika, kabla ya hitimisha naomba nichukue fursa hii kwa kukipongeza sana Chama cha CUF kwa kufanya uchaguzi wao wa ndani wa kuchagua wagombea wake wa Ubunge na Uwawakilishi kwa hali ya amani na salama. (*Makofi*)

Ninawapongeza sana wale wote walioshinda katika kinyang'anyiro hichi na pia ninawapa pole wale ambao kura zao hazikutosha. Ninaamini watajaribu tena hapo mwaka 2020. (*Makofi*)

**HITIMISHO:**

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kunisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawashukuru kwa dhati watendaji na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Khalid Salum Mohamed na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ahmad Kassim Haji kwa juhudi zao katika kutekeleza majukumu yao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na shukrani maalumu kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano, ushauri na maelekezo waliyotupa katika kipindi chote cha miaka mitano iliyopita ambayo yalitusaidia sana katika kufanikisha majukumu yetu. (*Makofi*)

Aidha, napenda kuwashukuru sana Washirika wetu wa Maendeleo wote *(Development Patners)* na nchi marafiki ambazo zinaendelea kuchangia katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Ofisi yangu na ya nchi kwa jumla katika mwaka wa fedha 2014/2015. Miongoni mwao ni: Benki ya Dunia, *Clinton Foundation*, China, *FAO*, Finland, Norway, India, Japan, Marekani, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu, Malaria na UKIMWI *(Global Fund*), Oman, *UNAIDS, USAID, UNDP, UNICEF, UNFPA, WHO, WFP* na *WIPO*.

Vile vile, naishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Tanzania na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano wao mkubwa na Ofisi yangu. Pia, nazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali, Jumuiya ya Wafanya biashara, Wenye viwanda na Wakulima kwa kuendelea kuisaidia Serikali katika kutoa huduma za jamii na kuleta maendeleo katika nchi yetu. Pia, nawashukuru sana wananchi wote ambao wamefuatilia na kusikiliza hotuba yangu hii.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya 23,333,300,000 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake (Tume ya Uchaguzi na Bazara la Wawakilishi). Kwa ajili ya kutekeleza Programu mbali mbali nilizozielezea hapo juu. Mchanganuo halisi wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais | Shs: | 5,166,700,000 |
| ii. | Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | Shs: | 1,404,000,000 |
| iii. | Ofisi ya Baraza la Wawakilishi | Shs: | 16,762,600,000 |
| | **Jumla:** | **Shs:** | **23,333,300,000** |

Mhe. Spika, sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

KIAMBATISHO NAM. 1

MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA KWA KIPINDI CHA JULAI -MACHI 2014/2015

| JINA LA IDARA | MAKADIRIO KWA 2014/15 | KILICHOINGIZWA JULAI– MACHI,2015 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 388,964,000 | 272,067,450 | 70% |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 184,007,400 | 134,207,903 | 73% |
| Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali | 482,066,600 | 392,018,845 | 81% |
| Ofisi ya Faragha | 483,116,224 | 449,644,209 | 93% |
| Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali | 344,638,000 | 231,909,954 | 67% |
| Idara ya Kukabiliana na Maafa | 298,447,800 | 196,518,500 | 66% |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 704,166,316 | 584,539,975 | 83% |
| Idara ya Uratibu wa SMZ Dar es Salaam | 353,178,160 | 181,504,731 | 51% |
| Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 871,615,500 | 1,358,989,917 | 156% |
| **Jumla Ndogo** | **4,110,200,000** | **3,801,401,484** | 92% |
| Tume ya Uchaguzi Zanzibar | 1,314,100,000 | 1,229,926,569 | 94% |
| Ofisi ya Baraza la Wawakilishi | 14,564,000,000 | 13,954,901,100 | 96% |
| **JUMLA KUU** | **19,988,300,000** | **18,986,229,153** | 95% |

KIAMBATISHO NAM. 2

MATUMIZI KWA KAZI ZA MAENDELEO KWA MIEZI TISA (JULAI- MACHI) MWAKA 2014/2015

| VOTE 5 | OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS | BAJETI KWA MWAKA 2014/2015 | KILICHOTENGWA MIEZI TISA(JULAI- MACHI) MWAKA 2014/2015 | KILICHOPATIKANA (JULAI- MACHI)2014/2015 | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|---|---|
| 05/20 | IDARA YA KUKABILIANA NA MAAFA (Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Maafa) | 50,000,000 | 50,000,000 | 25,000,000 | 50% |
| 05/19 | IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ (TASAF III) | 40,000,000 | 40,000,000 | 20,000,000 | 50% |
| | JUMLA KUU | 90,000,000 | 90,000,000 | 45,000,000 | 50% |

KIAMBATISHO NAM. 3

## UKUSANYAJI WA MAPATO KWA MIEZI TISA (JULAI- MACHI) MWAKA 2014/2015

| VOTE 5 | OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS | KILICHOPANGWA KWA MWAKA 2014/2015 | KILICHOPANGWA MIEZI TISA(JULAI- MACHI) MWAKA 2014/2015 | KILICHOKUSANYWA (JULAI- MACHI) 2014/2015 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 05/08 | **IDARA YA UPIGAJI CHAPA NA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI** | 600,000,000 | 450,000,000 | 295,903,000 | 66% |
| 05/05 | **IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI** | 5,000,000 | 3,750,000 | 0 | 0% |
| 05/19 | **IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA** | 3,000,000 | 2,250,000 | 11,940,000 | 531% |
| | **JUMLA KUU** | **608,000,000** | **456,000,000** | **307,843,000** | **68%** |

**KIAMBATISHO NAM. 4**

**Programu na Programu Ndogo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais 2015/2016**

| NAM. | PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO |
|---|---|---|
| **Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais** | | |
| 1 | **Programu C011:** Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | **Programu ndogo C0111:** Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais |
| 2 | **Programu C012:** Uratibu wa shughuli za Serikali | **Programu ndogo C0121:** Kukabiliana na Maafa |
| | | **Programu ndogo C0122:** Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. |
| | | **Programu ndogo C0123:** Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) |
| 3 | **Programu C013:** Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa | **Programu ndogo C0131:** Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa |
| 4 | **Programu C014:** Mipango na Utawala | **Programu ndogo C0141:** Uongozi na Utawala |
| | | **Programu ndogo C0142:** Mipango, Sera na Utafiti |
| | | **Programu ndogo C0143:** Ofisi Kuu Pemba |

| | | |
|---|---|---|
| **Baraza la Wawakilishi** | | |
| 5 | **Programu C021**: Kutunga Sheria, kupitisha Bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali | **Programu ndogo C0211**: Kutunga Sheria, kupitisha Bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali |
| 6 | **Programu C022**: Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | **Programu ndogo C0221**: Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi |
| **Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar** | | |
| 7 | **Programu C031:** Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi | **Programu ndogo C0311**: Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi |
| 8 | **Programu C032:** Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | **Programu ndogo C0321**: Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. |
| | | **Programu ndogo C0322:** Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi Ndogo ya Tume ya Uchaguzi Pemba |

**KIAMBATISHO NAM. 5**

**MGAO WA FEDHA KWA PROGRAMU NA PROGRAMU NDOGO**

| S/N | JINA LA PROGRAMU | JINA LA PROGRAMU NDOGO | IDARA/TAASISI HUSIKA | MAKISIO KWA PROGRAMU NDOGO 2015/2016 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais | 625,569,000 |
| 2 | Uratibu wa Shughuli za Serikali | Kukabiliana na Maafa | Idara ya Kukabiliana na Maafa | 405,775,000 |
| | | Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa | Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 987,260,000 |
| | | Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali | |
| | | | Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam | 846,692,000 |
| 3 | Usimamizi wa Shuguli za Upigaji Chapa | Usimamizi wa Shuguli za Upigaji Chapa | Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali | 714,050,000 |
| 4 | Mipango na Utawala | Uongozi na Utawala | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 780,741,000 |
| | | Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Miango, Sera na Utafiti | 271,792,000 |
| | | Ofisi Kuu Pemba | Ofisi Kuu Pemba | 534,821,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | | **5,166,700,000** |
| 5 | Kutunga Sheria, kupisha Bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali | Kutunga Sheria, Kupitisha Sheria na Kusimamia Taasisi za Serikali | Baraza la Wawakilishi | 6,539,295,000 |
| 6 | Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | | 10,223,305,000 |

[redacted]

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Jumla Ndogo** | | | **16,762,600,000** |
| 7 | Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi | Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi | Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | - |
| 8 | Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. | | 1,214,021,000 |
| | | Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Ofisi Ndogo ya Tume ya Uchaguzi Pemba | | 189,979,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | | **1,404,000,000** |
| | **JUMLA KUU** | | | **23,333,300,000** |

*(Hoja ilitolewa iamuoliwe)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ninakushukuru sana kwa kuwasilisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yako kwa ufanisi mkubwa na makofi mengi, sijui kama imepita bila ya kupingwa au vipi *(Makofi/Kicheko)*

Lakini kuungwa mkono na Waheshimiwa Wajumbe, inamaanisha kwamba sasa mjadala uanze. Nimkaribishe basi Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Hamza Hassan Juma.

**Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

**Mhe. Spika:** Watendaji mpeni maji Mwenyekiti pale.

**Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Spika, kwanza naomba sote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema na kuweza kukutana hapa kuweza kutekeleza majukumu tuliyopewa na wananchi wetu waliotuchagua.

Mhe. Spika, pili nikushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo kwa niaba ya kamati yangu, kuweza kuchangia hotuba hii iliyowasilishwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa utulivu na umakini mkubwa.

Mhe. Spika, pia nimshukuru Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na watendaji wake kwa kuweza kushirikiana vizuri na Kamati yangu, katika kipindi chote cha miaka mitano, mashirikiano hayo naamini yameleta ufanisi mkubwa kwa wizara, pia katika serikali kwa ujumla. Ndio maana leo hii Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameweza kusimama hapa mbele ya Baraza lako Tukufu, na kujinasibu kwa mafanikio makubwa ya serikali katika kipindi chao cha Awamu ya Saba yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa, ambapo hata sisi wananchi tumeridhika na hatua ya maendeleo inayopigwa na serikali yetu, huku nchi yetu ikishuhudia utulivu, amani na mashirikiano makubwa kwa viongozi wetu wakuu na hata sisi tunaofuata, jambo ambalo limeleta hali ya amani kwa wananchi wetu wa kawaida.

Pia tunaomba wananchi wote wa Zanzibar waendelee na utulivu huo hasa katika kipindi hiki kigumu katika nchi yetu, tunapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2015. Kwa hivyo, sote kwa pamoja tumuombe Mwenyenzi Mungu atujaalie na amani yetu hii iendelee kudumu hadi kumaliza kwa uchaguzi mkuu kwa amani na usalama. Amin.

Mhe. Spika, tatu kwa niaba ya kamati yangu naomba niungane na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kumshukuru Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa uongozi wake bora na wenye busara kubwa, kwa kuiongoza nchi yetu hii kwa salama na amani katika kipindi chake chote cha miaka mitano cha serikali yake ya Awamu ya Saba, ambayo imepata mafanikio makubwa katika maendeleo ya ustawi wa jamii, amani na utulivu kwa muda wote wa miaka mitano. Pale ambapo zilipotokea dalili za vurugu, hakuyumba ila alisimamia Katiba na Sheria za nchi yetu katika kukabiliana na changamoto hizo, na leo hii tunajivunia amani na utulivu uliopo katika nchi yetu. Kwa hivyo, iko haja na sisi sote kuweza kuilinda hali hii.

Mhe. Spika, kwa kujua hali ya bajeti ya mwisho ya Serikali hii ya Awamu ya Saba, basi naomba utuvumilie kwa kuchukua muda wako mwingi wa kuwapongeza viongozi wa nchi yetu. Kwa hivyo, nachukua fursa hii adhimu kwa kutoa pongezi maalum, kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa uwezo wake mkubwa aliouonesha kwa kumsaidia Mhe. Rais kuiongoza nchi yetu kwa umahiri mkubwa na ustahamilivu mkubwa. Wakati wote huo wa uongozi wake kwani amekuwa ni kiungo kikubwa, baina ya serikali na Baraza lako la Wawakilishi. Pia amekuwa Balozi mkubwa wa serikali kwa matakwa ya serikali kwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu la Wawakilishi. Hata pale tulipokuwa wagumu, basi alitumia uzoefu wake wa kidiplomasia kutulainisha, na kweli tuliweza kulainika na mambo yao kama serikali yalipita bila ya kupingwa.

Mhe. Spika, hii inatuonesha kuwa kweli Zanzibar ni chimbuko la viongozi mahiri na wenye busara na kuweza kuivusha nchi yetu kwa salama na amani, katika mawimbi na misukosuko ya aina yoyote bila ya msaada kutoka nje. Nadhani somo hili la Zanzibar, iko haja na nchi nyengine za Kiafrika waje Zanzibar ili kujifunza namna ya kuweza kusuluhisha tofauti zao bila ya kumwaga damu, na kuweza kuendesha nchi zao kwa upendo na mashirikiano makubwa.

Mhe. Spika, pia naomba kutoa shukrani zetu za dhati kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuweza kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar, katika kutekeleza majukumu yake ya nchi yetu, pamoja na tofauti zao za kisiasa na wakati mwengine wananchi walipata wakati mgumu kuhisi labda kauli zinatofautiana. Lakini kimsingi au kijumla mambo mengi ya kimsingi wamekuwa wakishirikiana, wakijadiliana na kupanga kwa pamoja.

Lazima tukubali  mfumo wa vyama vingi wa kisiasa, pia tukaongezea mfumo mpya kabisa duniani wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, inabidi tuwe wastahamilivu kwani ndio kipindi cha mwanzo cha mfumo huo, kwa hivyo inabidi tuvumiliane. Hapa kubwa kwa wananchi wetu ni tushukuru kuwa tumeweza kuvuka salama katika mfumo mpya wa kuongoza nchi yetu, kama nilivyosema hapo awali, basi

wenzetu nchi jirani hata wa mbali basi wanaweza kuja kujifunza miujiza hii iliyotokea hapa Zanzibar. Mhe. Spika, kwa hivyo naomba wananchi wote tuige mfano uliooneshwa na viongozi wetu wakuu kwa kutofautiana bila ya kugombana.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila bila ya kukushukuru wewe mwenyewe binafsi, kwa kuendelea kutuongoza kwa kipindi chote cha miaka mitano ya uhai wa Baraza hili la Nane, na kwa umahiri mkubwa na busara zisizo na kifani katika kipindi cha hali ya utulivu Barazani. Na pale ambapo kunapotokea dalili za misukosuko, umekuwa ukiirejesha hali ya utulivu Barazani bila ya kuonekanwa unapendelea upande wowote kati ya pande mbili zilizopo hapa Barazani. Hii inatuonesha ni jinsi gani ulivyokomaa kwenye utendaji na uadilifu katika kusimamia haki, kwa kusaidiana na wasaidizi wako, akiwemo Naibu Spika na Wenyeviti wako akiwemo Mhe. Mgeni Hassan Juma, kama alivyotajwa na Mhe. Balozi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi na kamati yangu naamini pamoja na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, tumeridhika kabisa na uongozi wako jinsi unavyotuongoza.

Mhe. Spika, kama Waheshimiwa Wajumbe wako wanavyoelewa kuwa, serikali imeanzisha rasmi utaratibu wa kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali, kwa mfumo wa kuzingatia program (*PBB*), mfumo ambao kwa Waheshimiwa Wajumbe wameshakuwa waelewa kwa kiasi, kutokana na juhudi za serikali kwa kushirikiana na Baraza letu, lakini wanaowawakilisha bado uelewa wao upo kama zamani, wa bajeti ya mfumo wa vifungu vya matumizi yaani (*Line Budget*).

Mhe. Spika, pamoja na juhudi zilizochukuliwa na serikali, sote tunakubaliana na ukweli kwamba, kumfahamisha mtu aliyetumwa ni lazima kuende sambamba na kumuelewesha yule aliyemtuma, kwani kumuelimisha aliyetumwa bila aliyetuma, ni sawa na kuufanya utumishi usiohitajika kwa wakati huo.

Mhe. Spika, nakusudia kusema kuwa, pamoja na juhudi za elimu ya bajeti ya mfumo wa *PBB* kutolewa kwa Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi, elimu hiyo pia inapaswa kutolewa kwa watendaji katika ngazi za chini za serikali, taasisi, mashirika, pamoja na wananchi ambao ndio waliowachagua na kuwateua Wajumbe wa Baraza hili, kwani mipango yote hiyo inamalizia kwao, kwani ndio watakaopata huduma zilizokusudiwa katika bajeti hii.

Mhe. Spika, kama alivyoelezea Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuhusu hali ya kisiasa hapa Zanzibar kwa hivi sasa ni nzuri, kwani kama nilivyoelezea hapo awali, viongozi na wananchi wanaendelea kushirikiana katika shughuli mbali mbali za

kiuchumi na kijamii. Kwa hivyo, tunamshukuru sana Rais wetu kwa kuweza kuisimamia kikamilifu hali hiyo, na kwa sote tumuombe Mwenyezi Mungu hali hiyo iendelee hivyo hivyo milele, ili kuijenga nchi yetu kiuchumi, kwani huko nyuma tumeshajifunza mambo mengi kuwa vurugu hazikutusaidia chochote ila kututia hasara kwa kujenga chuki baina yetu.

Mhe. Spika, kamati yangu tunaendelea kumuunga mkono Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa kuomba wananchi wote wa Zanzibar, kuwa huko mbele nchi yetu inategemea kuingia katika maamuzi magumu ya kinchi ya kupiga kura ya maoni ya Katiba inayopendekezwa, kwa kupiga kura ya kuiamulia hatma ya baadae nchi yetu, basi ni vyema wananchi wakaendelea kuzitafuta nakala za Katiba hiyo, ili kuzisoma na kuzielewa vizuri ili siku ikifika kuweza kuipigia kura Katiba inayopendekezwa.

Kwa hivyo, kamati yangu tunawaomba wananchi wote kuweza kuitumia haki yao hiyo ya kidemokrasia ya kuamua wanachokitaka bila ya kubughudhiwa na mtu yeyote. Kwani sisi Wazanzibari kwa muda mrefu ndio tuliokuwa tukilalamika kuwa Katiba iliyopo hivi sasa ina mapungufu mengi, wakati umefika kutokana na mabadiliko makubwa ya kisiasa na kiuchumi duniani na katika nchi yetu, basi iko haja ya kuweza kuirekebisha ili na sisi Zanzibar tuweze kutononoka kiuchumi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, sambamba na hilo si muda mrefu nchi yetu inategemea kuingia katika mtihani mwengine wa wananchi kupiga kura ya kuweza kuwachagua tena viongozi wao, ili kuweza kuwaongoza na kuwawakilisha katika kipindi kingine cha miaka mitano na kuiweka serikali itakayowaongoza kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Hapa kamati yangu inawaomba tena viongozi na wananchi kuweza kuilinda amani tuliyonayo na wala tusikaribishe viashiria vyovyote vya vurugu, kwani huu utakuwa ndio mtihani wetu wa mwanzo wa kuanzisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa hapa Zanzibar, kwani tukifeli mtihani huu basi Zanzibar haitokuweko njia nyingine yoyote ya suluhu ya amani, kwani itakuwa vurugu ndio maumbile yetu. Lakini sisi kama ndio viongozi tuliopewa dhamana na wananchi wetu kuwaongoza, basi ni vyema kuweza kuwa mstari wa mbele katika kuisimamia na kuilinda amani kwa maslahi ya wananchi wetu wanyonge.

Mhe. Spika, kamati yangu inaipongeza serikali kwa kupitia hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuwa Tume ya Uchaguzi imeshajiandaa kusimamia kura ya maoni na Uchaguzi Mkuu katika hali ya amani na utulivu, na kupitia kauli mbiu za viongozi wetu mbali mbali, akiwemo Mhe. Rais na leo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuwa uchaguzi utakuwa huru na wa haki, kwa hivyo tunaiomba Tume ya

Uchaguzi kuwa waadilifu katika kulisimamia hilo, ili wananchi wote wa Zanzibar waweze kupata haki yao ya kupiga kura, na waweze kuitumia haki yao hiyo kwa msingi wa kuwachagua viongozi wao wanaowataka, kwa uhuru mkubwa bila ya bughudha ya aina yoyote. Kwa hivyo, kamati yangu inawataka wananchi wote waliotimiza masharti ya kupiga kura wakajiandikishe ili kuweza kuja kuitumia haki yao hiyo ya kikatiba kwa ajili ya kupiga kura.

Mhe. Spika, kamati yangu pia inaunga mkono hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, na kuipongeza serikali yetu kwa kuendelea kuwaonesha moyo wananchi wetu, kwa kuwapunguzia mzigo wa maisha wananchi wetu kwa kufuta ada zote za kiingilio cha skuli, pamoja na kufuta ada ya mitihani yote kuanzia Skuli za Msingi hadi Sekondari.

Mhe. Spika, hili ni jambo kubwa sana hasa kwa wananchi wetu wanyonge ambao hata mlo mmoja kwao ni shida, kwa mtu wa kawaida hili ni jambo kubwa, kwani utakuta katika familia moja wakati mwengine kuna wanafunzi karibu watano mpaka sita kwa wakati mmoja, wote wanahitaji ada ya kiingilio cha skuli na wengine ada ya mitihani, jambo ambalo linampelekea mzazi kuchanganyikiwa wakati inapohitajika ada hizo, kwani uwezo anakuwa hana wakati mwengine na kushindwa kupata pesa na watoto wao kupelekea kukosa haki yao ya kimsingi ya kuweza kupata elimu. Kwa hivyo, tunawaomba vijana wetu kuunga mkono jitihada za serikali yetu, ili kuweza kuwapatia elimu bora, kwa hiyo wajitahidi katika kujisomea ili waweze kufaulu masomo yao, ili kuja kuijenga nchi yetu hapo baadae.

Mhe. Spika, sambamba na hilo tunaipongeza tena serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha vijana wetu waliofaulu mafunzo yao ya elimu ya juu, kwa kupata mikopo kupitia Mfuko wa Elimu ya Juu kwa masomo yao ya ndani na ya nje ya nchi. Hapa kamati yangu tunaiomba serikali kwa mwaka huu pamoja na pesa zitakazotolewa katika Mfuko wa Elimu ya Juu, basi ikiwa wanafunzi wengi watajitokeza watakaohitaji mkopo huu, basi serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza fedha hizo kupitia pesa za kodi ya miundombinu ambazo tuliyoipitisha jana tu. Hii itaweza kuusapoti mfuko huu, ili kuhakikisha kila kijana wetu anayehitaji Mkopo wa Elimu ya Juu basi aweze kupata fursa hiyo. Lakini pia kamati yangu inaiomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambayo ndiyo inayoratibu na kusimamia shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kufuatilia wanafunzi wote waliopata Mikopo ya Elimu ya Juu siku za nyuma, ili kuweza kuanza kurejesha pesa hizo ili ziweze kuzunguka na wenzao na wao waweze kuzitumia kwa ajili ya kujiendeleza kielimu.

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika kitabu chake ukurasa wa 8 kifungu cha 19.0, katika Sekta ya Afya. Serikali imeendelea

kuboresha huduma za afya na hapa tunaipongeza serikali, kwa kutekeleza ahadi yake kupitia kwa Mhe. Waziri wa Fedha pale kwenye bajeti ya mwaka uliopita tulipozuia bajeti ya Wizara ya Afya, kwa kushindwa kukitengeneza chumba cha *ICU*, ambapo hali yake ilikuwa mbaya sana au hata kusema tulikuwa hatuna kabisa huduma ya *ICU*, na kumpelekea Waziri wa Afya wakati ule Mhe Juma Duni Haji, kutaka kutishia kujiuzulu, lakini aliposimama Mhe. Waziri wa Fedha na kuokoa hali hiyo kwa kusema kuwa serikali itahakikisha kwamba *ICU* katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja inajengwa.

Leo hii Mhe. Spika, tuna furaha kusema kwamba zile kelele zetu Wajumbe wa Baraza lako hili Tukufu, kuitaka serikali kujenga *ICU* tunathubutu kusema kwamba tumeridhika kabisa, na tunaamini kuwa hivi sasa huduma hiyo ipo inatumika na inapatikana na wananchi wetu. Tunaipongeza sana serikali Mhe. Spika, kwa jitihada hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sambamba na hilo pia tunaipongeza serikali kwa kusikia kilio chetu cha muda mrefu, cha ukosefu wa madaktari bingwa na wauguzi hapa Zanzibar. Kilio hicho sasa kimeanza kupungua, kwani serikali tayari kwa kupitia Wizara ya Afya, wameweza kuongeza idadi kubwa wa madaktari pamoja na wauguzi katika Hospitali yetu Kuu ya Mnazi Mmoja  na zile kilizoko katika vijiji vyetu. Kwa kweli hivi sasa tunashuhudia tumeletewa madaktari na wahudumu katika hospitali zetu, ikiwemo na ile ambayo imo katika Jimbo langu la Kwamtipura, kwa kweli tunaishukuru sana serikali kwa kupitia Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, sambamba na hilo tunaipongeza serikali kwa kuandaa sheria ya *Condominium*, pamoja na kuanzisha sheria ya kuunda Shirika la Nyumba, ili kuwawezesha wananchi wanaoishi katika nyumba za maendeleo pamoja na zile nyengine za serikali kuweza kumiliki sehemu ya nyumba hizo kwa kushirikiana na serikali. Lakini pia kuanzisha ujenzi wa makaazi mapya ya wananchi kwa bei nafuu, ili kuweza kuleta maisha bora na yenye faraja kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, tunaiomba serikali kuianzisha kwa haraka Mamlaka hiyo ya Nyumba, na vile vile ikabidhiwe watu wenye uwezo na wenye ubunifu kwa kuweza kuandaa mbinu za kupata fedha, na kuweza kujenga nyumba hizo kwa bei nafuu kwa haraka sana, ili lile lengo la serikali la kuwapatia wananchi makaazi yaliyo bora liweze kufikiwa kwa haraka.

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuwa serikali imeguswa sana na suala la udhalilishaji na ukatili wanaofanyiwa wananchi wetu, hasa wakiwemo wanawake na watoto. Kwa kweli suala hili ni kubwa, linakera sana na linauma sana. Kwa kweli hivi sasa Zanzibar imekuwa ni aibu kubwa hasa unapowaona watu wazima wenye akili zao, wanawabaka watoto wadogo wengine hawajafikia hata umri wa miaka 10, hii ni aibu kubwa. Kwa hivyo, tunaungana na

jitihada za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuunda kamati ya mawaziri ili kushughulikia suala hilo. Lakini tunaiomba kamati hiyo bado hatujaona makali yake, kwani kila ukisikiliza habari za mawio asubuhi, utasikia kesi mpya za watoto wanaobakwa na wala huwasikii watu ambao wanachukuliwa hukumu kwa wale waliowabaka. Tunaitaka serikali kuhakikisha suala hili linakoma kabisa hapa Zanzibar.*(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la rushwa kama alivyoeleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, limekuwa ni suala la kusikitisha sana na tunapongeza sana jitihada za serikali, kwa kuanzisha sheria ya kupambana na rushwa, pamoja na Sheria ya Maadili ya Viongozi. Ingawa kuunda sheria ni suala moja lakini tatizo linakuja katika kutekeleza sheria hizo. Kwani tumeona kuna vitendo vingi vya rushwa bado vinaendelea na nyengine ni vya wazi wazi, lakini pia kuna ukiukwaji mkubwa wa taratibu za kisheria katika shughuli nyingi za serikalini. Nadhani wakati umefika tupunguze kuoneana muhali hasa katika mambo mazito ya shughuli za serikali, ili kujenga jamii inayoheshimu sheria na kufuata taratibu zinazowekwa. Vyenginevyo kila siku tutakuwa tunapiga kelele kuwa sheria hazifuatwi, lakini wakosaji pengine ndio sisi. Kwa hivyo, tunaiomba kwanza serikali tuanze sisi viongozi kufuata sheria, ili walio chini yetu waweze kutuiga, vyenginevyo na wao wataiga mifano yetu.

Mhe. Spika, kwa ujumla Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, inahitaji kuidhinishiwa Tsh. 23,333,300,000 kwa matumizi ya kawaida na matumizi ya shughuli za maendeleo, fedha ambazo zinahitajika kwa Ofisi yenyewe ya Makamu wa Pili wa Rais, Baraza la Wawakilishi na Tume ya Uchaguzi. Aidha, kati ya Taasisi hizi tatu kuu, ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pekee ndiyo yenye makadirio ya makusanyo kupitia Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, huku Taasisi zenye makadirio ya fedha za Maendeleo kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwa Kamati, ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pekee.

**OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Makamu wa Pili wa Rais, ofisi hii inatarajia kukusanya Tsh. 612,360,000 kwa mwaka 2015/2016, fedha ambazo zitapatikana kutokana na huduma wanazozitoa Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, fedha ambazo ni Tsh. 600,000,000 kutokana na mauzo ya uchapishaji na Tsh. 12,360,000 zinatarajiwa kupatikana kutoka katika Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, ambapo Tsh. 3,000,000 zitatokana na malipo ya ukodishaji wa vifaa na Tsh. 9,360,000 zitatokana na malipo ya kazi za biashara.
Mhe. Spika, kamati yangu inafahamu kuwa serikali inajaribu kujitahidi kuwa na njia za uhakika za kufanya makadirio ya makusanyo ya fedha mbali mbali kwa

kipindi cha mwaka wa bajeti, hasa kupitia Wizara na Taasisi zake mbali mbali. Bado hufanya makisio ya uzoefu wa mwaka ama miaka iliyopita katika kuamua na kuzielekeza taasisi zake kutafuta mapato kupitia vyanzo mbali mbali vya makusanyo hayo.

Kwa mfano, Mauzo ya uchapishaji ambayo mwaka huu yamekisiwa kuwa Tsh. 600,000,000 ndio hizo hizo zilizokadiriwa mwaka uliopita. Aidha, fedha zilizokadiriwa kwa mwaka 2013/2014 kwa Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga chapa Mkuu wa Serikali, zilikuwa Tsh. 500,000,000 kupitia Mauzo ya Uchapishaji, lakini fedha halisi zilizokusanywa zilikuwa Tsh. 42,776,200 kukiwa na tofauti ama upungufu mkubwa wa Tsh. 457,223,800, na mapato halisi yaliyopatikana ni sawa na asilimia 8.5 tu ya makadirio. Ambapo hali hii kama tunavyoelewa hali iliyokuwa nayo Idara hii ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali hatushangai kuwa kweli walishindwa kutimiza malengo yao, kutokana na uchakavu wa mitambo pamoja eneo walilokuwa wakifanyia kazi lilikuwa katika hali mbaya sana, lakini kwa sasa kamati yangu inajinasibu kuwa zile kelele za serikali kuhamishia Idara ile katika eneo lililo salama ili waweze kufanya kazi zao kwa utulivu mkubwa kama tulivyoanza kuona hivi sasa.

Mhe. Spika, kamati yangu inakubali ni kweli serikali kuwa iliipa idara dhima kubwa zaidi ya makusanyo kwa mwaka 2014/2015, ikizingatiwa kuwa mwaka 2013/2014, Idara hii na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ujumla haikuweza kufikia malengo hata kwa asilimia 10 ya makadirio ya makusanyo. Na ndipo mwaka 2014/2015 kama ilivyo pia kwa mwaka 2015/2016, Idara hii kwa kupitia chanzo hicho hicho cha mauzo ya uchapishaji, kimekadiriwa kukusanya Tsh. 600,000,000. Kiwango ambacho ni kikubwa ukilinganisha na makadirio ya mwaka 2013/2014 na 2014/2015.

Mhe. Spika, kamati yangu kwa mwaka huu wa fedha kupitia vyanzo vya mapato vya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, imeshuhudia tena kuondoshwa kwa vyanzo vya mapato ambavyo vilikuwa vinatumika kwa miaka iliyopita. Kwa mfano, mwaka 2014/2015, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilikadiriwa kukusanya Tsh. 5,000,000 kupitia Ukodishaji wa Ukumbi wa Mikutano *(Hire of Conference/ Seminar Hall),* chanzo ambacho kilianza kukisiwa na kuingizwa katika vyanzo vya mapato vya Idara hii mwaka 2013/2014. Kamati yangu imeridhika kwa mwaka huu kukiondoa chanzo hicho kwani hali ya ukumbi ule uliotegemewa kukusanya mapato hauko katika hali nzuri, kwa hiyo tunaitaka serikali kuweza kufanya maamuzi katika umilikaji wa ukumbi huo wakati ambapo hata Baraza la Wawakilishi waliomba uwe chini yao.

Mhe. Spika, halikadhalika kwa Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, mwaka 2013/2014 ilikadiriwa kukusanya Tsh. 3,000,000 lakini fedha hizo

hazikukadiriwa hata shilingi moja kwa mwaka 2014/2015 na mwaka 2015/2016 chanzo hicho cha fedha hakionekani kabisa katika bajeti ya Idara hii, sawa ilivyo katika Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inakadiriwa kutumia Tsh. 5,066,700,000 kwa ajili ya mishahara ambazo fedha zitakazotumika kwa matumizi haya ni Tsh. 1,967,950,000, Maposho yatatumia Tsh. 703,179,000 na fedha za kuendesha Ofisi ni Tsh. 2,395,571,000. Aidha, kwa matumizi ya maendeleo, fedha zinazohitajika kwa mwaka huu wa fedha ni Tsh. 100,000,000, kwa kuzingatiwa kuwa Tsh. 24,550,000 zitatumika kwa matumizi ya uendeshaji wa mradi na Tsh. 75,450,000 zitatumika kwa matumizi ya utekelezaji wa mradi.

Mhe. Spika, fedha hizo zinatarajiwa kutumika kupitia programu kuu nne ambazo ni Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais, yenye programu ndogo hiyo hiyo. Programu Kuu ya Pili ni Uratibu wa Shughuli za Serikali yenye programu ndogo tatu ambazo ni Kukabiliana na Maafa, Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kuwaenzi viongozi wa Kitaifa na Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, programu kuu ya tatu ni usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa ambayo programu yake ndogo ni hiyo hiyo na Programu Kuu ya Nne ni Mipango na Utawala yenye programu ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, ofisi inahitaji kupatiwa Tsh. 625,569,000 kwa Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Makamu wa Pili wa Rais, ambayo pia ni Programu Kuu fedha ambazo zitatumika zaidi kwa kuwapatia maslahi bora wafanyakazi, kulipia gharama za uendeshaji wa Ofisi, kuimarisha huduma za usafiri za Idara kwa kazi za kila siku, kununua vifaa vya kuandikia, vya usafishaji, samani pamoja na vifaa vyengine kwa matumizi ya Ofisi na kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi na ya muda mrefu, ambayo Kamati yangu imeridhia na naomba Baraza lako Tukufu vile viel na wao waweze kuridhia.

Mhe. Spika, program Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali inahitaji Tsh. 2,239,727,000 ili iweze kutekelezeka, na kwa upande wa Idara ya Maafa ambayo kwa kuzingatia mfumo wa Bajeti ya *PBB*, tunaweza kusema kuwa, shughuli zote za Idara hii zimo katika programu ndogo ya Kukabiliana na Maafa chini ya Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, kwa mwaka 2014/2015 ilikadiriwa kutumia Tsh. 298,447,800 kwa kazi za kawaida, na kwa mwaka huu wa fedha, Programu ndogo hii inahitaji Tsh. 405,775,000, ikiwa ni ongezeko la Tsh. 107,327,200.

Mhe. Spika, tunaipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa ongezeko hilo, lakini tufahamu kuwa, fedha hizo pamoja na kuongezwa kwake na ikizingatiwa maafa yanayoikabili nchi yetu, na fedha kidogo ambazo zinapaswa ziongezwe maradufu. Kwa mfano tu ukizingatia maafa ya mvua zinazoendelea kunyesha, namna ya kukabiliana na maafa haya, kuwasaidia walioathiriwa na mvua, kunahitaji matumizi makubwa ya fedha, pamoja na ukweli wa kutarajiwa kutumika kwa fedha za mradi zinazohusiana na maafa kama tutakavyoeleza baadae. Hapa tunaiomba Serikali sasa kuanzisha rasmi ule mfuko wa maafa ili uweze kusaidia kutoa huduma kwa haraka pale maafa yanapotokea kwani maafa siku zote hayapigi hodi pale yanapotaka kutokea.

Mhe. Spika, programu ndogo ya sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa ambayo shughuli hii mwanzo ilisimamiwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, kwa mwaka uliopita ilikadiriwa kutumia Tsh. 871,615,500 lakini kwa mwaka huu kwa kuzingatia programu ndogo niliyoitaja kabla, fedha zinazohitajika kwa matumizi hayo ni Tsh. 987,260,000, ikiwa kuna ongezeko la Tsh. 115,644,500 sawa na ongezeko la asilimia 113.2 ya makadirio ya mwaka jana. Aidha, Kwa programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, fedha zinazohitajika kukamilisha fedha za Programu Kuu ni Tsh. 846,692,000.

Mhe. Spika, program Kuu ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa ambayo programu yake ndogo ni hiyo hiyo, imekadiriwa kutumia Tsh. 714,050,000 kwa mwaka 2015/2016, ambazo ni nyongeza ya Tsh. 231,983,400. Fedha za programu hii ndogo zinatarajiwa kutumika kwa kuwapatia stahiki na maslahi bora wafanyakazi ikiwa ni pamoja na maposho, mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu (kwa wafanyakazi 7 wa Idara), kuimarisha huduma za uchapaji, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mafuta na vilainisho, kulipia gharama za umeme, kununua vifaa vya usafishaji, vespa, matengenezo ya mitambo na kununua zana na vifaa bora vya uchapishaji, kulipia gharama za matangazo na kuandaa mpango wa biashara, sheria na miongozo.

Mhe. Spika, programu Kuu ya Mipango, Sera na Utawala inakadiriwa kutumia Tsh. 1,587,354,000 kwa mwaka 2015/2016 huku fedha hizo zikielekezwa kwa matumizi ya program ndogo ya Uongozi na Utawala (Tsh. 780,741,000), Mipango, Sera na Utafiti (Tsh. 271,792,000) na Ofisi Kuu Pemba (Tsh. 534,821,000).

Mhe. Spika, ofisi Kuu Pemba, mwaka 2013/2014 ilikadiriwa kutumia Tsh. 452,817,000 na fedha halisi zilizoingizwa hadi kufikia Machi 2014 zilikuwa Tsh. 254,014,050 sawa na asilimia 56 ya makadirio. Kwa mwaka 2014/2015, fedha zilizokadiriwa zilikuwa Tsh. 388,964,000 na fedha halisi zilizoingizwa hadi Machi 2015, zilikuwa ni Tsh. 85,815,350, kukiwa na upungufu wa Tsh. 303,148,650 ya

makadirio. Hali hii bado inaonesha kuwepo kwa tatizo la uingizwaji wa fedha, bila ya kujali tuna mfumo gani wa bajeti.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo sasa ni programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka 2014/2015, kwa kipindi cha Julai hadi Machi, iliingiziwa Tsh. 55,621,903 na makadirio yalikuwa Tsh. 83,289,000 sawa na asilimia 88 ya makadirio.

Mhe. Spika, Tsh. 100,000,000 zinazohitajika kwa matumizi ya miradi ya maendeleo, miradi ambayo imo katika Program Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali katika programu ndogo ya kukabiliana na maafa, ambapo mradi wa Kujenga uwezo wa kukabiliana na maafa unahusika, huku Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga kwa fedha za ndani Tsh. 15,000,000 kwa ajili ya kuandaa michoro na kusimamia Kituo cha huduma za dharura cha kukabiliana na maafa na Tsh. 35,000,000 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya vituo vya kukabiliana na maafa kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kamati imetaka kupatiwa fedha halisi za wafadhili zinazotarajiwa kuchangiwa na washirika mbali mbali wa maendeleo na kuelezwa kuwa ni Tsh. 204,950,000 kwa mwaka 2015/2016. Aidha, kwa mwaka 2014/2015, Serikali ilikadiriwa kuchangia Tsh. 40,000,000 na wafadhili kuchangia Tsh. 1,282,880,000 na hivyo, jumla ya Tsh. 1,322,880,000 zilikadiriwa kwa ajili ya kujenga uwezo na kukabiliana na maafa.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia kuwa mwaka huu serikali itachangia Tsh. 50,000,000 na wafadhili wa maendeleo kuchangia 204,950,000 kunaifanya bajeti inayokadiriwa kwa matumizi ya miradi ya programu ndogo hii ya kukabiliana na Maafa kuwa Tsh. 254,950,000 wakati mwaka uliopita fedha zilizokadiriwa zilikuwa Tsh. 1,322,880,000 kwa upungufu wa 1,067,930,000, huku sote tukijua kuwa, kwa suala zima la kukabiliana na maafa, siku zote fedha huwa hazitoshi jambo linaloipekelea Serikali kuwa na uwezo mdogo sana wa kukabiliana na maafa hayo.

Mhe. Spika, kwa ajili ya utekelezaji bora wa progamu ndogo ya shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyo chini ya programu kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, inahitaji Tsh. 50,000,000 ambazo zitatumika kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF III*) kwa kuzingatia uchambuzi ufuatao:

- Tsh. 7,000,000 kwa ajili ya kusimamia miradi midogo 40 Unguja na Pemba.

- Tsh. 2,900,000 kwa ajili ya kuratibu shughuli za miradi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.
- Tsh. 5,300,000 kwa ajili ya kufanya vikao 8 vya Kamati ya Uongozi.
- Tsh. 13,520,000 kwa ajili kusimamia shughuli za uendeshaji.
- Tsh. 13,160,000 kwa ajili ya kufanya ziara za kikazi, mafunzo na kuandaa kikao cha ujumbe wa Benki ya Dunia.
- Tsh. 3,500,000 kwa kutoa elimu kwa njia ya vipindi vya TV na Redio.
- Tsh. 1,830,000 kwa kusimamia na kufuatilia miradi midogo midogo, na
- Tsh. 2,790,000 kwa kuandaa vikao vinane vya Kamati ya Uongozi.

Mhe. Spika, nimejaribu kuvifafanua vifungu hivyo ili kuonesha ni namna gani serikali inavyotakiwa kuwa makini katika ukusanyaji wa mapato ili kuweza kuingiza kwa wakati hasa katika utaratibu huu wa sasa hivi kwa bajeti inayotegemea programu.

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi nalo limekadiriwa kutumia Tsh. 16,762,600,000 kwa matumizi ya kazi kawaida, fedha ambazo zitatumika kwa mishahara (Tsh. 1,383,160,000), maposho (Tsh. 12,802,363,000) na matumizi ya uendeshaji wa Ofisi (Tsh. 2,577,077,000) ikiwa ni tofatuti na mwaka 2014/2015 ambapo Baraza lilikadiriwa kutumia Tsh. 14,564,000,000 kwa matumizi haya ya kawaida, ambapo kwa mwaka huu kuna nyongeza ya Tsh. 2,198,600,000.

Mhe. Spika, fedha hizo zinazoombwa mwaka huu wa fedha zinatarajiwa kutumika chini ya programu kuu mbili. Ya kwanza ni kutunga sheria, kupitisha bajeti na kusimamia taasisi za serikali ambapo programu yake ndogo ni hiyo hiyo. Programu kuu ya pili ni Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi yenye programu ndogo hiyo hiyo.

Mhe. Spika, programu kuu ya kwanza ambayo bila ya shaka programu hiyo hiyo ni ndogo, inahitaji kupatiwa Tsh. 6,539,295,000, fedha ambazo zinahitajika kwa kujadili, kurekebisha na kupitisha miswada ya sheria; Kusimamia utendaji wa Taasisi za Serikali na kupitisha bajeti ya Serikali. Katika kutumiwa kwa fedha hizo hadi kufikia tarehe 30 Juni ya mwaka 2016, Baraza linaahidi mambo yafuatayo:

- Kufikia asilimia 100 ya uwiano wa miswada iliyopelekwa na kupitishwa katika Baraza la Wawakilishi.

- Kupitisha Miswada 14.

- Wajumbe watakaokuwa wamechangia miswada ya sheria kufikia asilimia 40. Hapa ndio inapohitajika programu ya mafunzo.

- Kamati za Kudumu za Baraza zitakuwa zimeweza kutekeleza majukumu yake mara nne kwa mwaka na pia zimeweza kuwasilisha ripoti zao katika Mkutano wa Machi, 2016.

- Baraza litaweza kupitisha Bajeti ya Serikali katika kipindi cha bajeti ya mwaka 2016/2017. Hiyo ndio ahadi ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, fedha zinazohitajika kwa programu kuu ya pili ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi ambayo pia ndiyo programu ndogo ni Tsh. 10,223,305,000, fedha ambazo zitatumika kwa kuwapatia Wajumbe na Wafanyakazi wa Baraza lako huduma na stahiki zao na kuimarisha uwezo wao; kuimarisha mazingira ya kazi ya Afisi ya Baraza pamoja na kuratibu shughuli za Afisi ya Baraza Pemba.

Mhe. Spika, Wajumbe wako wana haki ya kulihoji Baraza lako na kumhoji Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na kuchukua hatua wanazoona zinafaa kwa mujibu wa Sheria na taratibu za Baraza, iwapo viashiria vifuatavyo vitashindwa kufikiwa hadi tarehe 30 Juni 2016.

- Iwapo asilimia ya Wajumbe na Wafanyakazi wa Baraza hawatopatiwa stahiki zao kwa asilimia 100.

- Iwapo Wajumbe wote na Wafanyakazi 24 wa Baraza hawatopatiwa mafunzo kwa ile asilimia 40 kama tulivyosema.

- Iwapo asilimia ya utekelezaji wa Mipango ya Kazi hautofikia asilimia 90 na huduma pamoja na matengenezo yanayohusiana na mazingira ya kazi yatafikia asilimia 100.

- Iwapo wafanyakazi watapata huduma kwa asilimia 100 na Wafanyakazi watano watapatiwa mafunzo. Hayo yote yanategemea upatikanaji na uingizwaji wa fedha kwa wakati kama Programu inayotegemea bajeti inavyoendelea au bajeti inayotegemea programu inavyohitaji.

Mhe. Spika, mradi wa Maendeleo wa Kuwezesha Mabunge *(Legislative Support Programme (LSP)* ambao mwaka jana ulikadiriwa kutumia Tsh. 710,615,000 kutoka kwa *UNDP* bila ya kuwa na mchango wowote wa Serikali, haukuwasilishwa maendeleo yake mbele ya Kamati na wala hauonekani katika

bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Bila ya shaka inaweza kuwa kunatokana na ule mkakati wa Serikali wa kupanga zile fedha za ndani ama za wahisani wa Maendeleo wenye muelekeo mkubwa wa kusaidia, lakini kwa taarifa tulizonazo, wenzetu *UNDP* bado wana tamaa ya kuendelea kuweza kutusaidia Baraza la Wawakilishi. Kwa kuwa kuna tetesi kuwa wanategemea kuendelea kutusaidia basi ni vyema ukaandaliwa utaratibu za kuuingiza kwenye Bajeti ya Baraza la Wawakilishi katika siku zijazo.

**TUME YA UCHAGUZI**

Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka huu wa fedha wa 2015/2016, Zanzibar tunaingia katika Uchaguzi Mkuu, na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ndio yenye jukumu la kuratibu na kukamilisha uchaguzi huo. Hali hii inaifanya Tume ya Uchaguzi kuhitaji fedha nyingi katika maandalizi ya Uchaguzi.

Mhe. Spika, fungu C.03 la Tume ya Uchaguzi linahitaji Tsh. 1,404,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi zake za kawaida, ambapo Tsh. 501,758,000 zitatumika kwa malipo ya mishahara, Tsh. 630,982,000 zitatumika kwa maposho na matumizi ya uendeshaji wa Ofisi yatakuwa Tsh. 271,260,000 kwa kiwango hiki kilichokadiriwa mwaka huu, na fedha zilizokadiriwa kwa matumizi ya kazi za kawaida mwaka jana ambapo ni Tsh. 1,314,100,000 kuna ongezeko la Tsh. 89,900,000 .

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ina porogramu kuu mbili. Programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi ambapo programu ndogo yake ni hiyo hiyo, na Programu Kuu ya pili ni Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar yenye programu ndogo mbili; ya Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Uchaguzi, pamoja na Uratibu wa Shughuli za Uchaguzi Pemba.

Mhe. Spika, Programu ndogo ya Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Uchaguzi inahitaji kupatiwa Tsh. 1,214,021,000 na Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Uchaguzi Pemba ipatiwe Tsh. 189,979,000 fedha ambazo kwa ujumla wake zitatumika kwa kuboresha maslahi ya wafanyakazi, kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi, kuwajengea uwezo wafanyakazi na kufanya ukaguzi na upimaji uwajibikaji.

Mhe. Spika, Fedha za Maendeleo hazikuonekana katika bajeti iliyowasilishwa kwa Kamati, wakati Kamati yangu inafahamu kuwa mwaka jana, Tume ilikadiriwa kutumia fedha za maendeleo kupitia katika mradi wa *UNDP* ya kuimarisha demokrasia, uliofadhiliwa na *UNDP* kwa makadirio ya Tsh. 1,750,000,000. Ni

vyema Kamati pamoja na Wajumbe wakafahamu mradi wa maendeleo unaotarajiwa kuwa Tume ya Uchaguzi kwa mwaka huu wa fedha wa 2015/2016.

Mhe. Spika, nimejaribu kueleza sana katika eneo hili la Tume ya Uchaguzi hasa kwa kuzingatia kuwa tunaelekea katika uchaguzi, kwa hivyo tunaiomba sana Wizara ya Fedha katika eneo ambalo linahitaji kuingiziwa fedha kwa haraka sana basi hili fungu la Tume ya Uchaguzi, ili kuweza kuandaa mazingira mazuri kuhakikisha kwamba katika uchaguzi unaokuja kusitokee malalamiko yoyote ya ukosefu wa vifaa au posho au huduma mbali mbali kwa ajili ya wafanyakazi.

Mhe. Spika, vile vile kabla ya kumaliza hotuba yangu sasa, naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa usikivu wenu wa kunisikiliza tokea mwanzo wa hotuba yangu hadi hivi sasa.

Napenda pia kwa niaba ya Kamati, kumshukuru Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais; Mhe. Mohamed Aboud Mohamed, Katibu Mkuu Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote pamoja na Makamishna, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kuweza kutoa mashirikiano makubwa na Kamati yangu kwa kipindi chote cha miaka 5.

Mhe. Spika, vile vile nikushukuru wewe pamoja na Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote wakiwemo makatibu wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na wanasheria wetu wa Baraza la Wawakilishi kwa kuweza kutusaidia sana sisi wajumbe wakati mbali mbali katika kutekeleza majukumu yetu. Lakini vile vile Waheshimiwa Wajumbe na sisi tunawasihi kuwaomba watumishi hawa wa Baraza la Wawakilishi kuendelea kutoa huduma bora kwa Wajumbe wote wa Baraza kwa kufuata Sheria na Kanuni za Utumishi kwa mazingira pekee ya huduma inavyotolewa hapa Barazani.

Mhe. Spika, tunamshukuru pia kama nilivyosema nishamshukuru sana Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi pamoja na Makamishna wote, Wakurugenzi, Idara zote za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, shukurani za pekee ziwaendee Wajumbe wa Kamati yangu ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano makubwa na kuaminiana katika kazi zetu. Naendelea kuwaombea Wajumbe hawa kurejea tena katika Baraza hili Tukufu la Wawakilishi linalokuja ili kuweza kutoa uzoefu kwa wajumbe wanaokuja. Kwani waswahili wanasema *isiyo kongwe haivushi*.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu sasa niwatambue Wajumbe wote wa Kamati yangu ambao walinisaidia sana katika kuandaa hotuba hii kama hivi ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe Hamza Hassan Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Saleh Nassor Juma | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ashura Sharif Ali | Mjumbe |
| 4. | Mhe.Shadya Mohamed Suleiman | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Subeit Khamis Faki | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ali Mzee Ali | Mjumbe |

Ambaye ni msaada mkubwa katika Kamati yetu ambaye kwa muda mwingi alikuwa akituwaidhi, akitupa nasaha sisi wajukuu au watoto wake katika Kamati. Tunamuombea Mwenyezi Mungu ampe afya lakini vile vile na yeye aweze tena kurudi katika Baraza hili la Wawakilishi ili kuweza kuchota ule uzoefu aliokuwa nao.

Mhe. Spika, vile vile katika kamati tulikuwa na katibu Ndugu Rahma Kombo Mgeni pamoja na Ndugu Othman Ali Haji ambaye kwa kipindi hiki aliweza kukaimu nafasi ya Katibu wetu Makame ambaye alikwenda kushughulikia masuala yake ya kimasomo.

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza hotuba hii naomba uniruhusu nitumie dakika chache ambazo hazitozidi 5 kama Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura. Naendelea tena kuipongeza Serikali hasa katika Jimbo langu la Kwamtipura, katika miaka 5 hii tumeweza kushuhudia mkono wa moja kwa moja wa huduma za Serikali katika Jimbo langu la Kwamtipura.

Kwa kuanzia nitoe shukurani zangu za dhati kwako wewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kuweza kusikia kile kilio changu cha muda mrefu, kuhusu barabara iliyotoka kwa Abass Hussein kuelekea Mboriborini hadi Kwamtipura.

Mhe. Spika, lile eneo ambalo lililokuwa kadhia kubwa ya wananchi wangu sasa hivi Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu imeweza kututilia lami pamoja kwamba haijafika mpaka mwisho, lakini pale ambapo mlipoweza kututilia ile lami si haba, na tunategemea kwamba ule ndio mwanzo lakini tunategemea, naamini katika awamu hii inayokuja mtaweza kutumalizia barabara ile mpaka mwisho.

La pili Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, naomba niendelee kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kutekeleza ahadi yake ya kutumalizia jengo letu la hospitali ya Mnazi Mmoja, ambalo kwa kweli lilikuwa limetukaa rohoni, tulijenga wenyewe ghorofa ya kwanza, ya pili ikatukwama ikatushinda. Lakini kwa kweli ameweza kutusaidia na alitoa ahadi yake yeye mwenyewe, na sasa hivi tunashukuru Serikali baada ya kumaliza ujenzi ule sasa

tumeweza kuhamishia kituo cha matibabu ya macho pale katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Bila ya msaada wenu Serikali kwa kweli kituo kile kingelishindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Vile vile, tunaipongeza Serikali kwa kuongeza muda wa kufanya kazi kutoka asubuhi mpaka saa 8 na sasa hivi kinafanya kazi mpaka saa 3:00 ya usiku. Kwa kweli Mhe. Spika, wananchi wa Jimbo la Kwamtipura pamoja na majimbo jirani lakini tunashukuru sana kwa huduma ambazo tunazozipata katika Jimbo letu la Kwamtipura. Lakini kubwa zaidi Mhe. Spika, pamoja kwamba halijatekelezwa, lakini tunaamini kama alivyoeleza Mhe. Haji Omar Kheri, mwalimu, kwamba ule mradi ambao umekuwa ni kadhia kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Kwamtipura pamoja na Jimbo la Chumbuni, mradi wa ujenzi wa mtaro wa maji machafu kutoka Daraja Bovu mpaka Saateni, kwamba sasa hivi tunashukuru wataalamu wameshaanza kuja, wameanza kukutana na masheha na kujadili mambo mbali mbali na kuweza kuandaa mazingira ya kuweza kujenga mtaro ule.

Mhe. Spika, kwa imani yangu kama alivyoeleza Mhe. Haji Omar Kheri kwa kuwa Jimbo la Kwamtipura na Jimbo la Chumbuni kuna Watumbatu wengi ambao ni jamaa zake, basi ninaamini kabla ya kumaliza bajeti hii basi alau zile harakati za kuhakikisha kwamba ule mtaro ambao unaanza kuchokolewa chokolewa na kuanza kusogezwa vifaa, kwa ajili ya ujenzi utaanza kukamilika.

Mhe. Spika, nategemea mradi huo ukiweza kukamilika hata ile kadhia ya maafa ya mwaka huu ya mvua kubwa iliwapata wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, pamoja na majimbo jirani, basi tunaamini mvua nyengine zitakazokuja za masika za mwaka ujao, basi sitegemei tena wananchi wangu wataweza kuzama pamoja na nyumba zao.

Kwa kweli Mhe. Spika, bila ya kusema hayo kwa kweli ningekuwa sikuwatendea haki wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, kwa kuishukuru Serikali yao kwa yote mema ambayo mliweza kutufanyia. Kwa hivyo tunaomba sana yale mambo mengine madogo madogo yaliyobakia, Serikalil iwe karibu na wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, lakini vile vile iwe karibu na wananchi wa majimbo mengine ili kuweza kupata huduma iliyo bora.

Sasa kwa kumalizia kabisa kabisa ninawaomba Wajumbe hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ni hotuba mtambuka, kwa sababu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yeye ndiye anayesimamia shughuli zote za Serikali, kwa hivyo mnaweza mkamshauri, mnaweza mkamuuliza katika maeneo yote ya Wizara, kwa sababu yeye ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali. Kwa hivyo, naomba tuitumie fursa hii ya kuiuliza Serikali na kuielekeza Serikali ili wananchi wetu waweze kupata ile huduma bora inayofaa.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, kwa kuwa juzi nilipokuwa nikitoa hotuba yangu kupitia Kamati ya Wenyeviti, niishukuru Serikali pamoja na wajumbe wote kwa kuweza kunifariji katika yale maafa, kwa hivyo sina haja kurejea tena, lakini kwa kweli ninawashukuru sana kwa mashirikiano yote mlionipa katika kipindi chote cha miaka 5.

Mhe. Spika, baada ya hayo sasa baada ya kunywa maji naomba kuwasilisha hotuba yangu hii kwa niaba ya Kamati. Ninakushukuru sana, ahsante sana.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanallahu Wataala* alitujaalia mchana huu kuwa katika hali ya uhai, uzima na afya inaturuhusu. Pia nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba yake mwanana ambayo ameitoa hapa na tumeifahamu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu katika hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais katika ukurasa wa 4 kifungu cha 9 naomba ninukuu kwa ruhusa yako;

"Mhe. Spika, hali ya kisiasa Zanzibar imeendelea kuwa shwari amani na utulivu, hali ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta maendeleo kwa kutoa fursa za uwekezaji, kufanyika kwa shughuli za biashara na mengineyo".

Mhe. Spika, ukikisoma kifungu hiki ni kizuri, mimi nitakubaliana nayo kama hali ya kisiasa sasa hivi ni nzuri lakini katika hali hii nzuri ni ya wananchi wenyewe ndani ya mioyo yao, tunaiomba Serikali hali hii iisimamie vizuri kwa kutenda haki, bila ya kufanya haki basi shwari hii itaondoka. Na tunamuomba Mwenyezi Mungu asiiondoe shwari hii kuwe na utulivu wa kutosha na amani. Nasema hilo kwa sababu ya msingi, vyama vya kisiasa vimeruhusiwa kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa Katiba yetu. Lakini *sometimes* kunakuwa na upendeleo wa kutosha, wengine wana haki wengine hawana, hili si jambo zuri, tunawaomba watu wote watendewe haki kwa mujibu wa sheria tulizojiwekea. Ukianza kupendelea upande mmoja basi kunakuwa na mkongamano mbaya sana, kwa sababu ukila na kipofu usimkamate mkono atajua huyu ananidhulumu.

Kwa hivyo, tunawaomba wasimamizi wa shughuli hii wasimamie vizuri hasa katika shughuli ya kuelekea katika Uchaguzi Mkuu na Kura ya Maoni. Nchi inapokuwa katika Uchaguzi Mkuu inakuwa katika mtihani mkubwa hamjakuwa na amani mpaka mtakapomaliza salama uchaguzi wenu na mkapata matokeo mkawa katika salama. Tunawaombeni sana Wazanzibari ni wamoja, na wataendelea kuwa wamoja, ila viongozi tusiwape tabu wananchi. Mimi naamini katika moyo wangu

wananchi hawana tabu hata kidogo, lakini tunawatia tabu, viongozi tuwe makini tuhakikishe kama nchi hii ni yetu wenyewe sote, wala hakuna mtu mwenye hati miliki ya nchi hii. Tutakwenda kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea, tutapishana mpaka mwisho wa dunia ndio hivyo hivyo tuyazingatie sana.

Mhe. Spika, Uchaguzi Mkuu umezungumzwa na imezungumzwa tumeambiwa wananchi waende kujiandikisha ili waingie katika daftari la kudumu la wapiga kura.

Itakumbukwa Mhe. Hamad Masoud Hamad alileta hoja binafsi hapa ya kupata hivyo vitambulisho vya *Zan-ID* ili kuingia katika daftari baadae. Mimi mwenyewe nilitoa ushahidi wa vyeti 103, siku hiyo kikao hiki kikiongozwa na Mhe. Naibu Spika, nikamkabidhi tukaambiwa katika majimbo kuna vyeti feki, mimi sikatai lakini vyote ni feki na watu hao hawajapata haki zao.

Mtu unapomnyima haki akitambua haki yake, na haki inataka kupiganiwa, inadaiwa mwisho inapiganiwa. Sasa kama mtu utamdhulumu siku zote hizo akirevuka wewe mwerevu utapata tabu. Naomba sana tutende haki katika shughuli zetu, hizi ni fursa zote zimetoka kwa wananchi wote wa Zanzibar. Nazungumza tena kama wananchi wa Zanzibar hawana tabu, tusiwatie tabu. Haki ikitoka upande huu na upande mwengine iende, ukimdhulumu huyu hapo ndio patapotokea matatizo.

Mhe. Spika, ni ushahidi tosha siku ya tarehe 29 tulikuwa na mkutano Makunduchi wa Chama cha *CUF*, baada ya kurudi kuna watu waliofanyiwa vurugu na wengine kutolewa macho, hii ni hatari, mahali kama pale huwezi kusema patakuwa na amani. Lakini jambo la kusikitisha kabisa na la huzuni, sijapata kusikia mimi sijui wenzangu mpaka leo hii kama kuna watuhumiwa waliokamatwa na tokeo lile. Lakini nasema kitendo kile kama kilifanywa upande wa CCM, hata kama hakuna watuhumiwa basi wangekamatwa watu kama 200 wakawekwa ndani, hili linatokezea na ndio ninavyosema haki itendeke pande zote mbili.

Naomba lizingatiwe sana wasimamizi mnaopewa mfanye kazi zenu kwa uadilifu, umepewa dhamana na wananchi, hujapewa dhamana kuwatesa wananchi ni dhambi kubwa unaowafanyia. Naomba twende kwa utulivu na amani kama ulivyotaja, tusitaje amani na utulivu katika makaratasi tu, twende kwa vitendo hapo ndio tutapofikia katika malengo ya amani na utulivu. Imezungumzia kama wananchi wa Zanzibar amani na utulivu imo ndani ya mioyo yao na wamezaliwa nayo amani na utulivu tusiwachafue.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa 8, sekta ya afya imezungumzia katika sekta ya afya. Hapa niipongeze Serikali na Wizara yenyewe,

imezungumzwa *ICU* mimi nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, nikiongozwa na Mwenyekiti wangu Mhe. Mgeni Hassan Juma tulipata kutembelea hospitali ya Mnazi Mmoja, kweli tuliona *ICU* ya zamani yenye vitanda 4 na *ICU* mpya yenye vitanda 8. Hapa ninawapongeza *ICU* ya kisasa na inahitaji mahitaji mazuri sana hapa Serikali imefanya vizuri, lakini pamoja na uzuri huo kuna changamoto za kutosha ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Moja, mgonjwa anapokwenda hospitali anakwenda kupata huduma na kama sio mgonjwa au kwenda kumjuilia mtu huwezi kwenda katika maeneo yale na mtu hataki aende kabisa, lakini Mwenyezi Mungu keshakujaalia kufika pale lazima upate huduma. Lakini kuna wahudumu wetu wengine hawawapi maneno ya faraja wagonjwa baada ya uchungu walionao wa magonjwa wanazidishwa magonjwa. Kwa hivyo, tunaomba serikali isimamie vizuri wahudumu wetu wapewe maelekezo ili mgonjwa akienda pale apate faraja, asijute kutoka nyumbani kwake akaenda maeneo yale.

Mhe. Spika, vile vile Hospitali ya Mnazi Mmoja ina maeneo inavujisha, wagonjwa wanapata shida kweli kweli hasa katika wodi ya wagonjwa wa kisukari. Halafu vitanda ni vichakavu vya kutosha vyengine vimewekewa mwega wa mawe, nilipata kushuhudia kwa macho yangu.

Mhe. Spika, jambo hili lichukuliwe hatua na ni jambo zuri sana mgonjwa akajisikia kama amefika katika sehemu ya huduma.

Vile vile,  katika mambo ya usafi tuko nyuma sana, maana yake hata *dettol* ya kusafishia pale wanatwambia hawana, *gloves* za kuvaa wakasafisha hawana, mambo madogo madogo kama haya yanaitia aibu serikali yetu. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika jambo hili lisimamiwe kwa nguvu zote na tupate afya nzuri kwa sababu wananchi ndio wanatoa kodi zao, na wakitoa kodi zao wakipelekwa pale wajue kwamba tunapata huduma kutokana na kodi zetu.

Mhe. Spika, katika hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais imezungumzia katika mambo ya sekta ya maji. Pia mimi nawapongeza sana katika sekta ya maji kwa kusambaza maji mijini na vijijini. Lakini pamoja na hayo kuna changamoto kubwa sana, mimi nawaonea huruma watu wa Jimbo la Kikwajuni la Mhe. Mahmoud wana dhiki ya kutosha katika mambo ya maji, watu wale kama Zanzibar hii sio pao. Mtu analazimika kununua dumu moja la maji shilingi mia tatu mpaka mia nne, madumu mangapi utahitaji? Una watoto wangapi ili asubuhi ukoge, jioni ukoge na ukilala ukoge, fedha inayotumika ni kubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba pamoja na huduma hizo zinazotolewa za maji lakini waangaliwe kwa jicho la huruma watu wa Jimbo la Kikwajuni pamoja na maeneo mengine.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu kuna udhalilishaji kijinsia wa wanawake na watoto, jambo hili linashamiri siku hadi siku, kila tunavyokaza ukanda kudhibiti jambo hili lakini siku hadi siku linakuwa, ni sababu gani zilizopelekea hivyo? Tunaomba serikali ichukue hatua na mambo haya kufanyiwa usimamizi mzuri na yapungue sio yazidi.

Itakumbukwa miezi mitatu iliyopita Sheha wa Shehia ya Majenzi Wilaya ya Micheweni alithubutu kumuingilia mtoto wake, mtoto tokea ana miaka tisa mpaka akashindwa akatamka dhahiri hatujui kesi ile inaendelea vipi.

Mhe. Spika, jambo hili ni baya, mimi nasema basi Mwenyezi Mungu atuepushie lakini ni kama laana, wewe mwenyewe unamzaa mtoto wako una hamu naye kiasi gani, watu wamejaa kibao wakubwa, warembo, unakwenda kumuingilia mtoto wako, hilo ni tatizo. Tuombe dua Mwenyezi Mungu atuepushie lakini na serikali ichukue juhudi ya kusimamia, mambo haya yanatia aibu hasa Kisiwani Pemba kila ukiletewa ripoti imezidi.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa ni mdogo niishie hapo lakini mambo haya niliyoyazungumza ni muhimu sana yazingatiwe na kufanyiwa kazi. Ahsante sana nakushukuru.

**UTARATIBU**

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Spika, hapa tunachangia bajeti kuu ya serikali na bajeti tuliyoanza nayo tunaanza na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini kuna yale matabu ya kuweza kuoanisha na kulinganisha kitu gani tunataka kuja kukikubali na kukichangia hatuna mpaka sasa. Sasa tunaomba muongozo wako katika hilo.

**Mhe. Spika:** Sikuwa nimeelewa hilo kama vitabu havipo, lakini kimsingi vitabu vipo kuna kazi moja ndogo sana ambayo labda pengine isingekuwa muhimu kukosa hivi vitabu. Tuna kawaida kuvitia majina ili kuhakikisha kila mmoja amepata, ni kazi hiyo tu, nimeelekeza kama hiyo kazi ya kutia majina haijamalizika basi vitabu viletwe kama vilivyo. Lakini vitabu kimsingi vipo, maana hata mimi cha kwangu hapa nimeshakipata kuonesha kwamba vipo hapa. Vitabu vinaletwa sasa hivi.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Spika, vitabu tunavyovizungumza ni vile vitabu vya kupitisha hizo *programmes* zenyewe.

**Mhe. Spika:** Ah! *Okay*, tutatoa majibu maana hapa sina majibu.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kabla sijaanza kuchangia niunge hoja ya Mhe. Mwenyekiti wangu Mwakilishi wa Kikwajuni kwa sababu Mheshimiwa hii ndio ripoti, lakini lengo hasa ilikuwa tunakwenda katika lile buku lenyewe ambalo buku hilo Mheshimiwa ndio lenye ule mfumo wa *PBB*. Sasa Mheshimiwa ninapotaka kuangalia katika maelezo ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na bajeti yenyewe husika nakosa.

Kwa hiyo, hapa mimi naona nitakuwa na-*support* hewa, hivyo natoa ombi langu ikiwezekana na kanuni kama inanilinda kwa hoja yangu kwa kuwa suala hili na vitabu vipo, na hata ukisema vigaiwe na mimi nikiendelea nitakosa haki. Naomba Mheshimiwa tuweke kanuni kando tuahirishe Baraza lako Tukufu tuje tena jioni kwa kuendelea. Naomba hapo kwanza jibu nisikie Mheshimiwa. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Nafikiri ni jambo la msingi kuona kwamba hasa kwa wale ambao wanataka kuingia kwenye programu kubwa na ndogo na wakawa na masuali kuhusu *activities*, huduma zenyewe ni jambo la msingi.

Sasa nikiahirisha kikao hivi punde ambayo nakubali hivyo tuhakikishe tumechukua hivi vitabu. Sasa tunayo nafasi ya kuvichukua nyumbani lakini tuhakikishe kwamba vinarudi kuja kufanyiwa kazi, maana mara nyingi inakuwa ni tatizo na ndio maana ilikuwa wanaweka majina ili kuhakikisha kwamba kila mmoja amepatiwa kitabu chake. Nafikiri ni jambo la msingi wala halina haja kuwekewa hoja, ni jambo muhimu na tangu hapo muda uliobakia ni wa wachangiaji wawili, basi tupate nafasi ya kugawa hivyo vitabu mimi nikiwa sipo hapa kitini. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, suala ambalo limejitokeza ni la msingi. Mhe. Mahmoud nakushukuru nilikuwa sikufahamu, nilifikiri vitabu vya hotuba, lakini kweli ni vizuri Wajumbe mkachangia sambamba na ule mgawanyo wa fedha, haidhuru humu umo lakini humu umo kwa kifupi mule ndio umo kwa ukamilifu wake, na pale ambapo Mhe. Mjumbe anataka kuweka hoja juu ya jambo ambalo Mhe. Waziri au Mheshimiwa mwenyewe Makamu wa Pili wa Rais aje atoe maelezo ni vizuri akawa anakwenda sambamba na hicho kitabu.

Basi nichukue nafasi hii kukiahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni lakini wakati huo huo tuone kwamba kila Mhe. Mjumbe hicho kitabu amepata ili kufanya marejeo kwa kile ambacho anataka kuja kukisema. Kikao kimeahirishwa hadi saa 11:00 jioni.

*(Saa 6:07 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea nina majina ya wachangiaji wawili waliobakia asubuhi. Kwa hivyo, wale wenye nia ya kuchangia walete ili tuweze kujipanga vizuri, kwa jioni hii tunaanza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk akimaliza ataingia Mhe. Asaa Othman Hamad.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nishukuru sana kwa Mwenyezi Mungu tangu asubuhi mpaka muda huu tunaokwendanao Mwenyezi Mungu katupa muda wa kuendelea na afya na tungali hai. Hilo kwanza nishukuru sana na *Insha Allah* Mwenyezi Mungu atujaalie atupe mwenendo huu huu wa uhai wenye afya na uzima bora.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuwapongeza wataalamu wa Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa sababu wataalamu ndio wapishi, ndio miundombinu, kama hatuna wataalamu waliobobea basi wizara au serikali inaweza ikaterereka. Kwa hilo niwapongeze sana kwa taaluma yao waliyokuwanayo.

Mhe. Naibu Spika, watu wengi sana hawaelewi nini utendaji wa Makamu wa Pili wa Rais, na niseme hivi kwa makusudi watu wafahamu. Kwa sababu Mhe. Makamu wa Pili ni kiungo wa wizara zote hapa Zanzibar. Leo mimi nimefurahi sana na nimefurahi kwamba kwanza na mimi nimekuja na sheria yangu mkononi, na ile dhana yangu mimi *wallahi* ningesema, sitaki nitumie lugha ya kuwa niseme ni malaika lakini niseme binadamu tu Mwenyezi Mungu alinipa ule moyo wa kufikiri jambo na Mwenyezi Mungu akalileta lile jambo ambalo nimelifikiria.

*Wallahi* nilifikiria siku moja nitoe hoja Mhe. Makamu wa Pili aweze kukaa katika kiriri na kuweza kusoma hii Hotuba ya Bajeti, nilikuwa na hamu hiyo Mhe. Naibu Spika, lakini ile hamu haikuwahi kutoka Mwenyezi Mungu akaileta *automatically* pale, *Wallahi laadhim*, nakwamba ni jambo ambalo nimefarijika na siku zote mimi hapa Barazani huwa nachelewa kuja lakini leo nimekuja mapema sana kutokana na kuwa na hamu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nilijaribu kutafuta sheria au kanuni lakini nimeona hamna hilo jambo ambalo nataka kulisema. Namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu anisikilize kwa makini sana, kwa sababu ya kukwambia ile hiba ya leo tuiendeleze iwe ndani ya sheria. Nilikuwa naomba sana ikiwa ndani ya katiba au ndani ya kanuni tuwe na uwezo wa kuweza kumuuliza maswali papo kwa papo Mhe. Makamu wa Pili ningefarijika sana. Ndio maana leo lile jambo alilosoma pale basi ile dhana ya kusema sheria hiyo naona kama imepita, niliona katika mawazo hayo.

Sasa kuna mtu hapa anapiga mimi simfahamu kitu gani. Mimi naomba au natoa hoja kwa ushauri wangu kuwa katika marekebisho ya katiba kama alivyosema Mwenyekiti wangu hapa kuna mambo ambayo lazima tuyafanyie marekebisho na kuweza kuyaleta ili yaweze kutusaidia katika sekta za uchumi na halikadhalika, hilo amesema Mwenyekiti wangu. Sasa mimi ningeomba sana ili tuweze kuitambulisha sheria hii, ili Mwanasheria aweze kuona jambo hilo lina umuhimu wake, kwa sababu kuna raha zake kuweza kumuuliza Mhe. Makamu wa Pili maswali papo kwa papo. Kuna raha zake, ustadi wake, umahiri wake. Kwa hiyo hili suala ninaomba sana watakaokuja walitengeneze hili ili wajisikie raha, kiongozi wao anakuwepo katika membari pale na wanaweza kumuuliza na akajibu kwa ufasaha. Mhe. Naibu Spika, hilo moja nimeona nilieleze hivyo.

Mhe. Naibu Spika, la pili niingie katika ukurasa sasa, mimi kwanza nikubaliane kabisa na Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa bado tungali tuna utulivu wa hali ya juu. Ningeomba sana kuwa hizi kero ndogo ndogo tusizisababishe zikawa kubwa, lakini *topic* kubwa tuseme tungali tuna usalama na amani yetu sasa hivi. Hilo niombe sana nilipongeze kwa hali ya juu kuwa bado Mhe. Makamu wa Pili ana uwezo wa kuweza kutuliza hali halisi, ana maelezo mazuri, basi naomba na sisi tuyakubali hayo maelezo yake mazuri ili tuendelee na amani yetu na utulivu tusigombane, tusifarikiane, haileti maana, haitotuletea uchumi endelevu kwa wananchi wetu, tutawasumbua wananchi wetu. Kwa hiyo, mimi naunga mkono kitabu chake hiki kwa lugha hiyo aliyoitoa hapa naipongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, niingie ukurasa wa 7. Ukurasa huu hapa wanaleta masikitiko hasa katika mambo ya Wizara ya Afya na hasa katika ukurasa wa 18, nimeambiwa kuna *ICU*. Mimi nasema ni mdau mkubwa wa Wizara ya Afya, kwa kweli hali ya hospitali hairidhishi, *ICU* tumeijenga kubwa sana na ni ya kileo lakini mpaka leo haijafanya kazi kwa nini? Hiki kitu najiuliza serikali imejitutumua kwa uwezo wote Mhe. Mwenyekiti wangu kasema hapa kwa ufasaha kabisa, kaeleza mambo yote na kila kitu mpaka kusema wakati ule Mhe. Waziri alikuwa Babu Juma Duni kutaka kujiuzulu akatoa mfano huo, lakini Mheshimiwa wetu hakujiuzulu, akaambiwa fedha zipo Waziri wa Fedha akajitutumua akasema fedha zipo na *Alhamdulillahi* tumeona, lakini *ICU* mpaka leo haijafanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, natoa angalizo tuwe na upendeleo wa kutembea, na nimesema hapa kuwa Mhe. Makamu wa Pili ni kiungo wa wizara zote, hebu jamani tuwe tunafanya mapenzi ya kutembelea kwenye wizara hadi wizara kuna matatizo, wafanyakazi wanataka kumuona kiongozi wao katembea na wanamsikiliza nini cha kusema na ndio maana nikasema sheria nyengine apewe Makamu wa Pili aweze kuwa na meno, awe na rungu la kuweza kuwawajibisha watendaji, sheria hiyo haipo na kama ipo basi tunaifumbia macho, apewe kwa sababu yule ni mtendaji na kama ipo kwa nini asiwajibishe watu mpaka leo iko *silence* haitumiki.

Mimi sijasikia Mhe. Makamu wa Pili akasema Katibu Mkuu huyo hafai, ondoa, sijamsikia hata siku moja. Sasa sina maana kusema kwamba Makatibu Wakuu wanavuruga hapana, nimetoa mfano tu kwa sababu mdomo wangu uko karibu na makatibu wakuu nawapenda sana, lakini wanisamehe sikuwa na maana hiyo ya kusema wao ndio wanaoharibu kuendesha serikali.

Mhe. Naibu Spika, lakini hilo ni moja na watendaji wengine na wengine, kuna wakurugenzi wengine wana matatizo, kuna wengine mtu anapewa uongozi wa *department just* ile kuambiwa wewe ni *coordinator* tu hapa basi anapenda kudhalilisha watu. Lakini utakuta Makamu wa Pili akipelekewa kesi ya yule mtu anashindwa kumuwajibisha, tumeambiwa jamani tusifanye kazi kwa kuangaliana, tuwe na utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, naona sasa ukumbi upo mara mbili, ndio maana nikasema hili suala kuwa Mwanasheria Mkuu aliangalie sana, wala asione tabu kwa kuwa kasema Makame Mshimba aweke *history* hiyo, mambo mawili ya sheria hayo Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria yupo anasikia ili aweze kuangalia zile hatua, tusione tabu kabisa kumpa hayo meno. Inawezekana ikawa mimi na mimi nikaja nikatumia sheria hiyo, ikaleta manufaa mazuri sana, inawezekana mwengine yeyote, inawezekana Waziri wa Fedha akapanda na yeye akapewa kitu kama hicho ikamsaidia sheria hiyo, halikadhalika na wengine. Sasa mimi naomba hiyo waiangalie vizuri Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lazima aweze kupewa sheria hiyo.

Kwa hivyo, *ICU* mpaka leo haijafanya kazi sababu kitu gani, sielewi. Lakini ninachosikitika kimoja mimi niseme ni bajeti tu hatujawa *serious* kuwekeza katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika, juzi moja nilimuona Rais alikwenda kutembelea sehemu ya kumbukumbu ya kuweka ile historia ya mtu anayetoka hospitali, mpaka leo hii mafaili yako chini ya meza mavumbi matupu, kumbukumbu ya mgonjwa huipati. Mimi miaka ya nyuma sana niliwahi kupelekwa operesheni wa *appendix* lakini leo hamna, sasa *reference* yangu, hebu katizame kama ipo na kama ipo mimi niko tayari kumdhamini mtu, hakuna ile kumbukumbu kwa sababu hatuna *space* iliyokuwa nzuri.

Niwashukuru sana watu wa *Mental*, wale *standard* lakini hawana wafanyakazi tu, lakini wameweka vitu vyao kwa *discipline* kabisa. Ukienda kumwambia tu mgonjwa wangu fulani anajua rafu gani yenye 'A' rafu gani yenye ''B', rafu gani yenye 'C', leo katizame pale hospitali hizo rafu zenyewe zote haziko *discipline*, mafaili hayako mazuri. Mheshimiwa inasikitisha na mwenyewe Rais kaona, sasa

leo tukimpa sheria hiyo Mhe. Makamu wa Pili wakati Rais ameshaona, Rais ametoa agizo atafanya nini, hukumu itatoka.

Kwa hivyo, mimi ningeomba sana tuangalie na bajeti, labda ukosefu wa bajeti na ndio maana tulisema mwanzo tuliangalia tulete buku, ndio maana nikakwambieni kwamba hili buku lilikuwa na uzito wake. Nimeangalia kwa ghafla tu hapo kumbe humu Mhe. Makamu wa Pili ameshatengeneza programu yake ya *PBB* vizuri tu. Humu mimi simpati kumpiga, huku nitasema kwenye kitabu, humu simpati hata siku moja, buti langu halipigiki, ndio maana nimekuja na viatu vya champali, haipigiki kwa sababu ameniwekea mwenendo wa *cash*. *Inshaallah* nikirudi huko kesho ndio nitapambana na buku hili, ndio iko wazi hii wala sipotezi muda wangu nitasema tu imepita hiyo. Kwa sababu ameniwekea malengo ambayo huko mbele mimi nitakufanyia hili na hili, sasa hilo nishukuru sana kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea hospitali nilisema juzi kwamba kuna mashine, mashine hiyo imetolewa fedha na Mfuko wa Afrika ya kufanya *full blood picture.* Mashine hiyo inachekesha sana, mashine nzuri nilijaribu kuzungumza na watu wa Muhimbili walisema mashine zile walizikataa. Kwa sababu mimi tatizo langu siishii hapa tu naishia hata huko karibu karibu kunakotengenezwa huko, mashine hiyo sasa hivi ni mbovu kwa sababu kifaa chake huwezi ukakipata hapa mpaka China, ni bora ununue mpya, mpaka leo hili suala. Mhe. Makamu wa Pili atapokuja anipe jawabu na huyu mtu aliyefanya kitendo hicho ameshatumia sheria ya utawala bora? Hakuna kuoneana haya hapa, sasa hivi ukweli tuambizane, hakuna kumezeana kwa sababu mashine hiyo ya *full blood picture* hebu nenda nje *full blood picture* ukitaka kufanya mtu kiasi gani, leo mnaleta vitu kama hivyo tena iko *laboratory* kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nimeshindwa kuja nazo picha nimezisahau, kawaida yangu huwa na picha nimeangalia mifukoni kumbe hazimo, lakini ninazo mpaka picha mashine hiyo inasikitisha sana. Hii hospitali ya rufaa si kitu cha mchezo Mheshimiwa, kwa kweli inasikitisha.

Halafu nataka kusema Mhe. Waziri wa Fedha wajitahidi jamani wakatafute maeneo mengine. Jana nilikuwepo hospitali vigodoro vyembamba kabisa vimekaa wagonjwa watatu, niambie nani atapona hapo, utapona au utazidi maradhi. Nimelia mgonjwa wangu aondoshwe, mama yangu mwanamke nakwambia! Nimelia machozi nasema mgonjwa aondoshwe ataendelea kupata maradhi mengine. Inasikitisha sana tena sana, ningeomba kwa kuwa serikali ina mambo mengi basi Mheshimiwa afanye harambee, wafanyabiashara jamani hamtaki hata sadaka hii? Wenzetu kule Bara wanatoa vifaa kusaidia Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, nataka niwaombe sana tusingojee serikali jamani, nawaombeni sana hali ngumu hebu nendeni kule hospitali nawaombeni, haki ya Mungu inasikitisha kweli nakwambieni. Ukienda kwa wazazi kitanda kimoja watu wawili, mzazi ana uchungu na unajua uchungu mzazi anataka ajifarague katika uchungu, sasa hebu nambie huyu ana uchungu na huyu ana uchungu ngoma inakuwaje? Mtajibu wenyewe kina mama, huyu ana uchungu na huyu ana uchungu kitanda kimoja, nambie sasa tumbo kama hili mimi nabiringita huku na huyu anabiringita huku tutagongana matumbo hatimaye tunaanguka chini. Mgonjwa unampa raha aendelee na uchungu vizuri ni moja katika tiba ya kumpa *relief* mgonjwa.

Sasa hii nayo inasikitisha sana, naomba sana afanye ziara tena Mhe. Makamu wa Pili ni shujaa anakwenda tunagongana mimi na yeye. Siku moja tuligongana yeye hakuniona tu mimi, yeye yuko juu mimi niko chini nikasema *yes*. Sasa na hii aende halafu aje kunambia kama mimi nasema uongo, mimi sisemi uongo kwa kutaka faida gani, lakini nina uchungu na nchi, nina uchungu na hili jambo la fedha za wavuja jasho hatari.

Leo hospitali dawa hamna operesheni watu wanalipa shilingi 40,000 wanaambiwa waende wakanunue nyuzi, zile fedha wanazochangia zinakwenda wapi.

Mhe. Naibu Spika, *CT Scan*, nina mgonjwa nimempeleka *CT Scan* tumelipa shilingi 150,000 lakini picha sikupata naambiwa hamna picha halafu rufaa hiyo. Jamani tuiwekeze, naomba sana Mhe. Makamu wa Pili, namuomba Mhe. Rais tuache yote tuwekeze fungu kubwa sana katika Wizara ya Afya Mheshimiwa hatari kubwa, dawa nje hazinunuliki.

Tuna mgonjwa nimekwenda kununua dawa za shilingi 90,000 alipata *fructure* ya kichwa *internal* ana-*bleed* ndani ya *brain*, mwisho na mimi nitakuwa *specialist* karibu, maana yake nimeshakuwa najua *internal* na *abdomen* nitakuwa dokta na mimi nishaona ishara hizo, kwa sababu ni vitu ambavyo unaambiwa. Mimi nauliza *problem* nini, nashukuru wananihadithia, nashukuru tunashirikiana kwa kufanya maendeleo hayo ya kusaidiana. Lakini ninachoomba Mheshimiwa asione tabu, hakuna mtu kusema jambo lenye kheri kwa kumwambia mtu kuwa jamani ee tuchangie jambo fulani si vibaya jamani, wenzetu tunawapa mzigo mzito.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii ni kubwa sana pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha kuwa kapunguza mambo mengi ya safari. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha tuangalie wenzetu hali ngumu, kule *mental* ukienda hali ngumu hata karatasi ya kutoa *photocopy* ya kupata yale maelezo ya mgonjwa wa akili haipatikani, naomba sana hili suala liweze kufikiriwa na liweze kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije suala la rushwa, rushwa imekithiri kweli na kama alivyosema Mhe. Waziri wa Fedha usimuonee mtu lakini vile vile nataka kutoa shule hapa Mwanasheria naomba aniangalie sana. Unajua tusidanganyane si rahisi mtu kumkamata na rushwa hiyo tusidanganyane, lakini mtizame Makame Mshimba tangu asubuhi yake anakula muhogo na likitua anakula shelisheli, leo mimi na-*change* ghafla nakula mbeya asubuhi mchana nakula pishori, sijui unakula katlesi, hebu jiangalie hujiulizi na wakati yule mtu umeshaambiwa anakula rushwa. Sasa unangoja nini hapo, mtie pingu. Sasa *sausage* yake anakula, hebu niambie.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba tupewe semina, wala usione tabu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wasomesheni hawa, wapeni semina Majaji, kuna mambo unaweza ukahukumu kinadharia, kihistoria, Mwanasheria nikatalie hili kama hivi haliwezekani, unaweza ukamuhukumu mtu kinadharia, ukaona tu ile *ground* yake halisi katika akaunti yake mtu ana *two hundred millions* hujui kaipata wapi, hana kiinua mgongo, hana shamba alouza. Sasa wewe hujui na tayari huko nyuma kuna *absent* kubwa katika *department* yake. Sasa mimi naomba hili suala tujaribu sana kuweza kufuatilia.

Jambo jengine ni ukatili wa kijinsia. Mhe. Naibu Spika, suala la kudhalilisha watoto na unyanyasaji. Mhe. Naibu Spika, niseme ukweli Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hatujawa *serious* na suala hili, *wallahi laadhim* hatujawa *serious*. Inatia uchungu, aibu!

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Tume. Mimi ninasema *wallahi* mimi sililii, utasema kama mimi nalilia, mimi sililii lakini anawachagua Mhe. Rais watu siyo hawana imani. Eeh! niseme ukweli, siyo, hawana imani. Leo kama kweli Tume hebu mimi nimejiundia Tume kesi ngapi nimeshazipeleka Mahakamani sasa hivi na aje aniulize mimi nitamwambia, nimejidhamini mwenyewe, nimejitolea mwenyewe. Simu yangu ipo wazi niiteni popote ninakwenda. Ninayo timu nzuri ya Kaskazini B wakiwemo akinamama na wengine tunashirikiana nao Mhe. Naibu Spika. Tumeifanya kazi, unyanyasaji huu umekuwa mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais usione tabu, mwambie Mhe. Rais anachagua watu siyo, wapo watu maana yake unajua kitu kutumikia siyo kizuri mimi mheshimiwa, bora ujitumikie mwenyewe. Mimi ninajitumikia mwenyewe, niiteni sitaki kupewa pesa mimi, nisilipwe, wala mafuta mimi sitaki. Lakini hili suala tulikomeshe, na *wallahi* linakomesheka hili, ninaamini sana.

Ninasema leo iwe basi unyanyasaji, imekwisha leo. Kwa hivyo basi na nyinyi Wawakilishi ninakugeukieni mushiriki, tusifanye mchezo. Kila mtu ana jimbo lake hapa, hebu tuwe wamoja tukamataneni, tuisaidie hii Ofisi ya Makamu wa Pili wa

Rais, tusiwe sisi tu, na sisi tuna matatizo vile vile, tugeukeni kwa kwenda kushirikiana ili tumpe nguvu Mhe. Rais aone, muone kama hamjarudi majimboni, mutarudi tu! (*Makofi*)

Zipo sababu nyingi za kumfanya mtu arudi jimboni, kwa sababu ukiwa unatetea jamii, unashiriki kuliondosha hilo tatizo kubwa, wananchi watakurudisheni. Hebu tushikamane hili suala tuone kama hatukurudi sote hapa, *wallahi laadhim*. Kwa sababu ni jambo linaumiza, lina kashfa, hulali, mwanangu Mtume Yarabi Salama atarudi saa ngapi, hatobakwa. Hebu tuwe *serious*, naomba sana jamani hili tusifanye mzaha tuwe *serious* na hili suala tulikomeshe. Tumuunge mkono Dkt. Ali Mohamed Shein kwa suala kama hili kwa kila njia. Naomba sana suala hilo Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, niendeleze katika suala ambalo ninaomba sana mheshimiwa kuna mambo mengine Serikali sasa hivi lazima ni suala la maafa. Mhe. Naibu Spika, hapa nataka niwapongeze sana, shujaa Katibu wako Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Mhe. Waziri ni Dkt, sijui *PhD* sijui mutasema wenyewe, maana mimi nikisema sana mutasema labda jamaa yangu.

Mhe. Naibu. Spika, nilikuwa ninamuona halali usiku na mchana, ile mvua yote imemuishia mwilini pamoja na Waziri wake na Makamu wake. Si kitu cha mchezo, lakini watu hawafahamu wanafikiria Wizara hii au hii Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndiyo yenye maafa peke yao, Wizara nyengine hizi hawazioni. Kitu kama hichi kinasikitisha. Kwa kweli hicho kifungu kidogo imekuwa nongwa. Kwa kuwa wamekuwa wanapewa vile vifungu vidogo kuna hii *special* Idara ya Maafa tena imekuwa sote hatuhusiki. Haiwezekani, kwa sababu pale panatakiwa kuna njia, kifusi akabebe Mohamed Aboud wakati siyo wizara yake. Hatukutoa mashirikiano, mimi ninasema wazi wala siogopi. Niseme kuwa hatukushirikiana nao vizuri, hatukuwasaidia katika masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, ninashukuru sana Mhe. Balozi Seif Iddi alipokuja tu alianza kuingia kwenye maji, hakuona tabu, hakujua kuwa pale atapata malaria. Lakini katembelea sehemu zetu pamoja na Makamu wake wa Kwanza pamoja na Rais mwenyewe, wameonesha ujasiri. Sisi tunangoja nini. Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, hii Wizara tusiitupie mzigo, ni lazima tuwasaidie katika mambo ya maafa, tuwe kitu kimoja.

Lakini leo unakuta mwenyewe Katibu, leo unamkuta mwenyewe Waziri, kesho unasikia king'ora charara, unamsikia mwenyewe Makamu wa Pili wa Rais, kesho kutwa unamsikia nani, hawa wapo wapi jamani. Kwa hivyo mimi ninaomba sana kwa mashirikiano yenu mazuri, na kwa kupitia Wizara yenu ya Fedha, kwa sababu fedha na wao walikuwa wakichombeza, wakipeleka fedha ambazo za kuwasaidia

na nini. Lakini *tools* za kufanyia kazi hawana hawa. Hawa Waziri utawapa pesa bure, watakuwa nazo pesa lakini magari na nini yatakuwa wapi ya kupeleka kifusi, wanapata matatizo.

Kwa hivyo, mimi nishukuru na zile njia na nimefurahi sana, nimekuta sasa *alhamdulillah* kumbe kusema kusaidia dawa Mhe. Naibu Spika, nimezikuta sasa zimetengenezwa zipo safi. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hayo ndiyo tunavyosema kuwa fungu bado la maafa haliwezi kutosheleza kabisa. Ninaomba mimi sana hili suala liweze kufikishwa pahala pazuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea zaidi niseme kuwa hivi sasa tunataka kuleta wawekezaji. Mhe. Naibu Spika, wawekezaji lazima tuangalie na kuangalia kwetu lazima tuwatafute wawekezaji waliokuwa wenye historia nzuri na wenye uwezo madhubuti, kwa sababu leo nchi yetu hii hatuna wawekezaji waliokuwa *strong* kabisa, hakuna kabisa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi nilisema juzi hapa, na leo ninarejea tena. Mhe. Naibu Spika, kuna ubadhirifu na hii Makamu mwenyewe yupo, Waziri yupo naomba sana Mhe. Waziri na Mhe. Waziri wa Katiba *registration* zako pale haziangalii utaratibu, zinafanya sisemi kama rushwa lakini itakuwa kwa sababu kuna *registrar* huwezi kusaini kampuni mbili kwa pamoja, kaangalie Mheshimiwa uje unitajie baadae hapa Mheshimiwa Abukabar Khamis Bakary, hili haliwezekani!

Mheshimiwa Mwanasheria fuatilia hilo suala, mutuletee kitu kilicho kizuri kisiingizwe katika matatizo, Ofisi yangu ya Makamu wa Pili wa Rais isiingizwe kwenye matatizo. Lazima tufuatilie jambo *completely* kabisa tupate kitu cha uhakika. Mimi naomba sana Mheshimiwa tuwe waangalifu sana katika masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea kumalizia sasa hivi ninataka kutoa *alert*. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi niwashukuru sana watu wa *Immigration*. Watu wa *Immigration* sasa hivi wanakamata watu wenye vyeti bandia. Nimeshuhudia mwenyewe, sisemi kwa uongo, nimeshuhudia mwenyewe. Wengine wamekimbia *Immigration*, wengine walikamatwa. Mtandao huo upo sasa hivi mkubwa sana wanatoa vyeti vya bandia vya kuzaliwa. Sasa mimi ninafikiria hajawa *serious*, ninadhani Serikali hatujawa *serious* katika mambo mengine.

Kwa sababu watu wanavitumia hivi kwenda kutafutia *passport*, watu wanavitumia hivi kwa kutafutia vitambulisho, almuradi imekuwa sasa haileti sitofahamu nzuri, kutumia vyeti vilivyokuwa ni vya bandia, na hivyo vipo na vimekamatwa. Nendeni *Immigration* mukavione, nendeni kule vitambulisho vikaonekane. Hata mimi

walikuja watu katika kampuni *Zanzibar Life Opportunity* pale, tukagundua watu wana vyeti vya kuzaliwa feki, tukasema hivi hatuna haja navyo.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi naona hili suala liangaliwe kwa umakini kabisa, kwa sababu hii hatari kwenda kumpa vyeti. Kumbe sasa una-*forge* tena unajua kinachofanywa *forgery* kwenye *serial numbers*. Itakuwa *serial number* yangu mimi kapewa Mlinde, munafikiri ni kitu gani. Ni hizi namba tu pale kinachotumiwa lakini hawa watu inavyoonesha wanatoka Wizara hii husika ya usajili, ninafikiri wanatoka huko, haiwezekani, *serial number* mtu hawezi kupata kibandia bandia, au tuseme labda iwe Mlinde aniuzie mimi *serial number* yake, hiyo kitu haiwezekani kutokea.

Mhe. Naibu Spika, nije masuala ya unyanyasaji kwenye mahoteli. Mhe. Naibu Spika, leo nimeletewa barua bahati mbaya nimesahau mkoba upo nje, barua ya Hoteli ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, naomba sana jamani hizi sheria zipo *weak*. Mhe. Naibu Spika, wananchi wa Tanzania wanadhalilishwa, hii tuseme ukweli tusione haya, tutungeni sheria jamani tufuateni hizi sheria, kwa sababu sheria hizi nimekwambieni, mimi nikikwambieni zimepitwa na wakati muamini. Kwa sababu mimi ninafuatilia sheria, nikikaa nyumbani ninaangalia mitandao, wenzetu wana sheria gani sasa hivi. Na hivyo ni kweli kabisa, kwa sababu leo twende katika nchi ya Kenya, kamtizame pale huyo Mtanzania kama ni *manager* katika hoteli yoyote, nendeni katizameni basi hamumuoni, hamwendi muka-*quote* na ukienda na nchi nyengine halikadhalika.

Lakini leo katizameni hapa, anaanzia Joyce nani kutoka Kenya, kutoka wapi asimnyanyase Mtanzania hapa. Sisi wenyewe tumekaa tu. Aah! *wallahi* Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana, inanisikitisha sana. Maana yake inanisikitisha na saa nyengine hukaa nikafikiri hasa nani nikapigane naye hili suala alisawazishe, kwa sababu ninasema na ninasema hapa lakini sheria haichukuliwi. Tutungeni sheria jamani tuwaambie Watanzania wenyewe, Jakaya Mrisho Kikwete siku ngapi anasema suala hili, alikemea alikuta huyu kutoka wapi, akaambiwa huyu anatoka Kenya, anatoka Kenya? Hakuna mtu ambaye anaweza kufanya kazi hii, alikomesha Jakaya alikataa kitu kama hichi.

Sisi tunaogopa nini, au ndiyo rushwa yenyewe tunakula viongozi, sisi tunaogopa nini. *Wallahi* Mhe. Naibu Spika, tunaogopa nini sisi, sheria tunatunga wenyewe hatupo *serious*, sijui kwa nini.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hebu siku moja fanya ziara, unafanya ziara *sometimes*, hebu nenda kafanye ziara, *wallahi* nenda kaseme *full management* hapa ndani ya hoteli hii, utaona haya Mheshimiwa. Ukimuuliza yeye, tena ukifika waombe *certificates*, halafu linganisha na mwananchi huyo baada ya

*certificate* hiyo, utarudi shingo upande kama ulivyoiweka sasa hivi hapo. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa wizara yako kubwa, mimi sipendi niitupie mabomu kwa sababu wizara yako kubwa na wewe ndiyo mtendaji, nimekupa cheo hapa nimesema upewe meno. Ninaamini tatizo lako linalokusumbua Mheshimiwa hujapewa meno kwa mujibu wa sheria, ninaamini hilo. Lakini nimeshasema Baraza linalokuja Mhe. Naibu Spika, Katiba itakapobadilishwa au Kanuni, sasa safari hii tunataka upewe meno.

Sasa Mhe. Naibu Spika, asiyekubali kufuata sheria Mhe. Naibu Spika, mtoe nje usimuonee haya, au si hivyo niweke Waziri wako, niambie tu kamtoe fulani, nitakwenda kumtoa tu mimi simuonei haya mtu. Kwa sababu tumo katika kujenga nchi. Wananchi ndiyo maana hawaoni uchumi kwa sababu hawapati zile kazi ambazo munazozisema nyinyi, munaotoa milango wazi ili watu wawekeze, hatukatazi watu wasije kuwekeza, sheria zifuatwe za nchi. Tukimpa mmoja *okay*, sisi tumpe mmoja tu, tutampa mmoja pale kama *chief* anamjua mwenyewe aliyesomea tumekubaliana naye na mtu mmoja wawili watatu. Lakini *department* yote, sehemu ya kufua, sehemu ya bustani, sehemu nini, unamkuta mtu Bazungu, unamkuta mtu nikisema Muhindi wengine wanisamehe, utamkuta nani mtu wa Kenya, utamkuta mtu wa Burundi na kila mtu pale, ati kusimamia bustani.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana, bustani basi! Leo watu wanafukuzwa kwenye hoteli ya Melia pale kwetu Kiwengwa wamefukuzwa watoto wadogo kabisa. Mhe. Naibu Spika, wakati ndiyo huu tunataka kura sisi kwa wananchi wetu. Ninaomba sana Mhe. Naibu Spika, kipindi cha *break* hapa fuatilia hayo ninayokwambia, na uje hapa utwambie mheshimiwa. *Wallahi* tunasikitika sana.

Halafu kuna hichi kitu kinaitwa niseme labda hii kwamba Mhe. Haroun Ali Suleiman, kidogo nimeona miwani yangu imenipotea Mhe. Naibu Spika, sijui *DNA* bwana! Mhe. Naibu Spika, nimeisahau kidogo. Kuna sehemu kama ni Mahakama, labda nitoe *example* yake.

Mahakama hiyo inahukumu mtu pesa yake kwa siku anatumia milioni mia mbili kwa siku. Lakini msimamizi wa kesi ile ana mshahara wa shilingi laki mbili, aliyeonewa amedhulumiwa hakupewa mshahara wake wa shilingi laki mbili, kitandawili.

Mhe. Naibu Spika, unafikiria vipi, sisemi kama wanakula rushwa, *no*, ninatoa mfano kwa sababu na wale nao watu, mshahara wanaopewa ni mdogo na wanahukumu kesi zinazoanzia *two hundred millions*. Sasa unafikiri mpaka leo kesi zile zinang'ang'anaa hazijesha.

Watu wa Kiwanda cha Sukari pale nilisema sana na hili ninakuomba sana Mhe. Naibu Spika, Kiwanda cha Sukari kiwe *serious,* hebu twende. Mhe. Naibu Spika, nenda pale wakawaulize wananchi wasikilize juzi wamekuja kwa makundi wanafukuzwa watu wana mikataba wameshafika miaka minane, miaka mitano watu wanafukuzwa tu, hakuna haki yao wanayopewa katika nchi yao hii ya Zanzibar, tumekomboa, wanafukuzwa, kiwanda kile pale wanateswa.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nenda ukaone, halafu njoo uwaambie Baraza kama mimi ninasema uongo. Jamani tuumwe na masuala kama haya Mhe. Naibu Spika, naomba sana tuumwe na sheria hizi. Hili jambo hatuwakatai wawekezaji lakini wafuate sheria, kwa nini wasifuate sheria. Leo mtu ana miaka minane vitoto vidogo na watu wazima, mtu unamwambia toka nje kazini, hataki kumpa haki yake, wewe nchi yako hii?

Mhe. Naibu Spika, mimi hapana bwana! kama mutaninyima mara hii musinipe kura potelea mbali lakini ukweli nitausema, wananchi wenyewe wanajua vya kusema, lakini siwezi nikawaacha wananchi wangu ndani ya ardhi hii, wakati wazee wamegomboa wametoka jasho. Halafu huku ni kutawaliwa kisayansi, ukisikia kisayansi ya kutawaliwa ndiyo kama hivyo kwa sababu ardhi yako mwenyewe unanyanyaswa. Aah! ukoloni kweli mambo leo *wallahi*.

Ni mtu tu tena Muafrika, ni Muafrika *just* anafanya vitendo kama hivi vya kunyanyasa watu. Unakwenda uungane nao, wale wanasema hapana, hawana lazima uwalipe twende kwenye sheria, inasemaje sheria ya kazi, ipo hii. Halafu leo kwa nini hatufuati Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, ninapita rasharasha sina haja ya kumpiga yeye Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini ninatoa *message*. Kila wizara niliyoigusa hapa nimetoa *message,* wakati huo huo wizara zao siwapigi kwenye buku hili kwa sababu siwapati *too late*. Hapa anakwambia Waziri wa Fedha, bora nikupe hongera *wallahi*, hii *master* yako ya Uingereza *fantastic* kweli, hii bwana siyo ya kughushi. Waziri wa Fedha kapata *pure masters* ya Uingereza. Sasa nimekuwa ninakuogopa kwa sababu *professor* ninamuogopa mtu mwenye *master* si ajabu hiyo, lakini lazima niseme ukweli, hapa umetuweka wewe kiza na aje mtu anioneshe hapa kama atakupingeni hii, hata siku moja, labda awe ni mtaalamu, huyo atakwenda mafamba tu. Kile kifungu kimekubaliwa, ndiyo, tunakwenda zetu, hakuna ile buu! hamna Mhe. Naibu Spika, hamna kabisa!

Mhe. Naibu Spika, mheshimiwa nikushukuru sana kwa hilo. Mhe. Naibu Spika, nimalizie sasa kwa kumuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kazi tunayo kubwa, na kazi tunayo kubwa ya ufuatiliaji, kwa sababu tumekuwa tuna-*delay* sana.

Halafu la mwisho nimelikumbuka Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ufanye ziara katika Jeshi la Polisi. *Wallahi* ninakuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ufanye ziara, halafu uniite mwenyewe kisiri, utasema duu! umeona nini wewe. Ninakuomba sana Mheshimiwa lakini nitafurahi sana hata zile *radio calls* sasa hivi wanazo tayari, kwa sababu walifika hata *radio calls* wakawa hawana Jeshi la Polisi, wanatumia simu tu wanataka kufanya *exchange* ya jambo unaambiwa simu hii *is not reachable*. Aah! wakati mtu yupo kwenye msafara ingekuwa ajali.

Ninashukuru sana Mhe. Rais amefanya jambo la msingi sana kuhangaika pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tumepata *radio calls* ambayo ni moja kati ya kiungo cha kuonesha jinsi gani Rais atafika wapi sasa hivi, Rais kabadilisha na nini, hilo moja lakini simu tungesababisha ajali na viongozi wetu tunawapenda.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hilo moja niseme lakini hii ninamalizia kwa Polisi Jamii. Mhe. Naibu Spika, sijaona jitihada zako za kuipenda Polisi Jamii, munaidharau hii Polisi Jamii. Hebu fanya kwa makusudi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais waite, kwa sababu Polisi Jamii Zanzibar imekufa, leo Tanzania Bara Polisi Jamii ni nzuri, wanavaa nguo vizuri huwezi kuamini na Jakaya kawapa fedha. Waaambie hawa wafanyabiashara Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Polisi Jamii jamani inatusaidia kwa Zanzibar.

Leo kaondoka Kamishna Mussa kaichukua Polisi Jamii yake. Tizama Tanzania Bara anavyoeneza, tumemuondoa Kamishna Mussa tumempeleka Bara, tizama Bara sasa Polisi Jamii ilivyoshamiri si mchezo, tizameni taarifa ya habari nyinyi. Huwezi kuona taarifa ya habari ya kwanza, ya pili unaoneshwa kwenye kaya ya Polisi Jamii wamo katika foleni wanataka kujipanga kwenda kwenye kazi zao. Sisi leo Mhe. Naibu Spika, watu wamefanyiwa *trainee* ya polisi jamii hapa tumewaondosha. Tulikuwa naye kijana mmoja anaitwa Majura na yeye alikuwa mmoja katika mwalimu wa masuala hayo na yeye tukasema kwa kuwa ni rafiki yake Mussa hatuna haja naye. Haa!

Mhe. Naibu Spika, hii ni tabia moja ambayo sio nzuri jamani. Mimi niliposhinda katika Jimbo la Kitope, wale wote ambao niliwakuta wenzangu sikuwanunia, na ndio demokrasia. Lakini sisi tuna tabia mbaya. Tabia yetu mtu unakuja kumkomoa. Wa nani huyo, wa fulani huyu. Usimpe kitu. Wa nani wa fulani huyu. Mrembee huko. Hatuendi hivyo, utawala bora haufanyi hivyo, hii ndio tabia tuliyokuwa nayo. Sasa mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, kuwa hebu tuwaite wale polisi jamii waliokuwa na uzoefu tuwaulize mmenasa wapi ili tuwasaidie. Mhe. Naibu Spika, naomba sana *credit* hiyo ukiifanya ukaita polisi jamii Zanzibar viongozi wao, pamoja na mapolisi wao, mheshimiwa utakuwa umejenga mustakabali, tena hawatakusahau maisha. Kwa sababu uzuri wa kiongozi ukiondoka kwenye

madaraka weka kitu kieleweke, kila watu wakikaa Mhe. Balozi, Mhe. Balozi, hawaimbi nyimbo nyengine, kwa sababu kile kitu kakiweka cha msingi na chenye maana.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, watafute hawa uwaite. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana leo kwa kunipa muda mrefu sana, ili na wengine wameshapata *view* ya kuweza kuchangia, namuona Mhe. Subeit Khamis yuko tayari. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**Mhe. Asaa Othman Hamad:** Nashukuru Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia jioni hii kufika tukiwa na idadi ile tuliyoanzia asubuhi bado tuko salama. Ni neema zake yeye Allah Inshaallah tumuombe atujaalie tuikamilishe shughuli hii kwa kipindi hiki na awamu hii ya mwisho tukiwa salama.

Mhe. Naibu Spika, kitabu hiki cha Ofisi ya Makamu wa Pili tumekipata hivi asubuhi. Nimejitahidi kukipitia sina budi niwapongeze sana waandaaji. Dhana iliyoandikwa humu Mwenyezi Mungu aibariki, kwa mara ya mwanzo *asaa kher* tukafika mahali stahiki.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze hapa kwenye huduma za jamii. Nimefarijika sana kabisa. Imepangwa hapa elimu, afya, maji na nikaona upande wa elimu kuondolewa zile kero ambazo wananchi wakizipigia kelele. Katika hili naipongeza serikali. Moja imekumbuka sasa kumuenzi Al-Marhum Mzee Karume. Mzee Karume alitangaza afya bure, elimu bure. Hapa katikati pakaingia kidudu mtu, tukaambiwa tunachangiwa, kubabaishwa tu maneno ili lengo lifikiwe. Lakini lugha iliyotumika leo inafuta.

Hongera sana Mhe. Balozi. Mzee Karume alisema *be, wau, re,* bure, akijilabu kusudi vijana wa nchi hii wapate elimu bila ya malipo. Sio kwamba ni bure haina thamani, alijua wananchi wa nchi hii ni wakulima na wakwezi. Hawa sio wakulima wa Marekani ama Vietnam, uwezo wao ni duni, hawataweza kulipa matibabu wala elimu. Maneno haya ndio maana alisema *be, wau, re,* walikuwa wanamfahamu Wazanzibari siku hizo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba amenifilisi sana kwenye sekta ya afya. Lakini haitakuwa vibaya nikisema kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ndiyo inayosimamia sekta zote tulizonazo. Inalazimika ama kuwajibika kuona mambo yanakwenda vile ambavyo anatakiwa yaende. Kwenye afya tunasema Mnazi Mmoja ndipo tunaita ni rufaa, lakini bado tunasua sua sana, haiba ya Hospitali ya Rufaa haijafikiwa Mnazi Mmoja.

Mhe. Makame Mshimba vile ambavyo nilikuwa nimeviweka mfukoni kavifichua. Lakini niseme kwamba bado Mhe. Balozi hapa mahali panahitaji jicho la karibu sana, kwa sababu ndipo penye maisha ya watu. Ukiwacha vile vyombo ambavyo ndivyo hivyo vinachunguza kumurika na kujua tatizo, hutopata tiba kama tatizo halijajulikana. Lakini vyombo vyenyewe ama mashine yenyewe kama hiki hakipo kimeletwa nusu na nusu hapana, kipo pale hata vile vilivyoletwa na vyenyewe vinakufa pale pale, hatujafanya kitu. Ni ukweli usiofichika wagonjwa wengi wanaojiweza wanasafiri kwenda Dar es Salaam ndio India ya wengi. Lakini ni wangapi wanaweza kwenda Dar es Salaam.

Mhe. Spika, Sasa turudi kwenye ile dhana iliyokusudiwa ya Mapinduzi ya nchi hii. Watu wanateseka sana, wanasumbuka sana magonjwa haya. Maana tuna mabadiliko ya tabia nchi, lakini kuna na mabadiliko ya maradhi yanatusumbua mno. Waheshimiwa Wajumbe mnaweza kusogea wengi mnakwenda Dar es Salaam, wengine mnakwenda China, wengine Uingereza na kwengineko.

Lakini wananchi wetu huko hawafiki, serikali ijitahidi sasa kuboresha hii Mnazi Mmoja kama ni rufaa, lakini ibaki kuwa ni rufaa kwa kuziboresha hizi Kivunge, Mnazi Mmoja, Wete, Chake Chake, Mkoani, Micheweni na kwengineko, ili mgonjwa hata akija Mnazi Mmoja kweli anastahiki rufaa. Tunaisifia *ICU* hii itachukua wangapi. Ukenda asubuhi Mnazi Mmoja robo tatu wanahitaji *ICU* kwa macho tu. Bado afya inahitaji nguvu za ziada.

Mhe. Naibu Spika, natoa pongezi tena kwenye sekta ya elimu. Hizo tozo serikali imezifuta, lakini nitaomba itajwe. Kama jana Mhe. Waziri wa Fedha alituambia itaanza tarehe 01/07/2015. Hii nayo nitaomba itajwe itaanza lini, kusudi walimu wakuu kule mashuleni wasije wakajenga hoja nyengine kwamba hawajapata barua, hawajapata muongozo, hawajapata hiki na kile. Kwa hivyo, tungeomba itajwe kwenye chombo hiki ili kila mmoja asikie na walimu wakuu, taratibu nyengine tena ziendelee.

Mhe. Naibu Spika, jengine kwa haraka haraka. Mheshimiwa Zanzibar ni visiwa viwili vikubwa na vimezungukwa na visiwa vingine vidogo vidogo. Nazungumzia ile Idara ya Maafa. Idara ya Maafa tusiitizame upande wa bahari tu. tungejitizama tukajipima hata hizi siku mbili hapa au tatu ambayo mvua ilikuwa inanyesha kwa wingi, ni kiasi gani tumeathirika. Mengine ni uzembe wa wazi kukosa usimamizi, kukosa uwajibikaji na tunasababisha wenyewe kupata maafa ambayo hayakuwa na sababu.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wanajenga ovyo, lakini nani anawapa vibali vya kujenga. Mtaro wa maji unajengewa ghorofa juu, maafa yatakuja tu. Lakini pia

maandalizi ya kukabiliana na haya maafa au majanga yakitokea bado ni hafifu mno sio yale ya baharini wala ya nchi kavu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kujua kwamba sisi tunaishi mazingira yetu ni ya visiwa, tunahitaji matayarisho ya ziada yaweko baharini na hapa nchi kavu, tukizidiwa huku nchi kavu tutaelekea wapi. Yakitokea baharini tunafanya nini, vyombo vinazama sote ni mashahidi. Watu wa Nugwi hawalali, vikosi vyetu ndio hivi vinavyofanya hiyo kazi, lakini unaiona ile hali haipendezi kabisa, hakuna matayarisho wala hakuna chochote kilichopangwa. Mwenyezi Mungu yuko ndio tunachokifanya hicho na anatusaidia na ataendelea kutusaidia. Lakini Mwenyezi Mungu anahukumu nia za waja wake wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba serikali katika maeneo haya, hebu tujipange sasa tujuwe moto ukiingia mahali gari litapita wapi, tuitizame hali yetu. Boti likizama ni chombo gani kinakwenda kusaidia. Wavuvi wamepotea wanatafutwa na kitu gani, hayo ndio mazingira ya visiwa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na yote hali ya uchumi imesemwa imeboreka na takwimu zimetajwa, kama mambo ndio hivi basi tuwapongeze wenzetu wanaoshughulika na sekta hii. Lakini bado Mhe. Naibu Spika, mimi nashindwa kuelewa, itakuwaje hali ya uchumi iwe imeboreka kiasi hiki, lakini hali za wananchi wetu bado ni duni kupita maelezo. Mhe. Naibu Spika, umaskini unarindima Mzanzibari anakula mlo mmoja ama hali kabisa, hana pesa ya kwenda matibabu, tunaishi maisha mabaya mno.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningesema hivi, ukuaji wa uchumi huu, kuboreka kwa hali ya uchumi huku kungekwenda sambamba na hali za maisha ya wananchi wake, hapa mimi ningesema *Alhamdulillah*. Lakini hii kuboreka kwa hali ya uchumi kwenye nambari na maandishi ya namna hii, bado sipati uelewa na nitahitaji maelezo ya kina ili niweze na mimi kusema kwamba kweli hali ya uchumi imeboreka.

Mhe. Naibu Spika, nimeambiwa hali ya kisiasa iko tulivu ni amani, wananchi na viongozi washirikiane kudumisha amani. Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida huwa hutakiwi kuwa na mashaka na mtu yeyote, ila mashaka yanakuja kutokana na vitendo. Lugha hii inayoandikwa kwenye kitabu hiki ingekwenda sambamba na hali halisi ya mwenendo mzima wa kisiasa, mimi ningesema naam. Lakini ishara ama dalili hazioneshi hivyo. Tumeshuhudia kipindi hiki watu wamepigwa hapa, wameumizwa, watu wamepoteza viungo vyao hapa na sababu ni siasa na vyombo vyetu vya ulinzi bahati mbaya, badala ya kusimamia amani ya watu wenyewe ni vishawishi wakubwa wengi wao kuleta balaa hili.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nyinyi ndio mafya matatu mlioko huko juu, umma huu unawatazama nyinyi, lakini na dunia inashuhudia. Lakini zaidi ya yote Mwenyezi Mungu mwenyewe anaona na anajua nafsi zetu. Hili sisi tutasema kwamba tunawaombeni tunataka amani, tunataka utulivu ndani ya nchi hii, hapa tumezungukwa na bahari hatuna pa kwenda chonde chonde tumekubaliana kwa hiyari kabisa, tutabadilishana madaraka ya nchi hii kwa kupiga kura moja mtu mmoja, inakuwaje tena kutoa meli za mafuta zikibeba watu kuleta hapa inakuwaje na kwa nini. Tunaongeza nguvu, kutoka wapi. Meli inashuka Kizingo, Meli inashuka kule kwenye *ranch* ya ng'ombe. Nayasema haya Mhe. Naibu Spika, nikijua nasema nini, atakayetaka kunisuta asimame anisute. *(Makofi)*

Sasa kama kweli tunahubiri amani na utulivu, tuwe ni wakweli.

## UTARATIBU

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Naibu Spika, nimesimama kutokana na kifungu 63 juu ya utarabu huu ninaouona. Mzungumzaji aliyepita amezungumza jinsi ya kuletwa watu kutoka sehemu mbali mbali kwa meli. Ningemuomba tu Mheshimiwa alete ushahidi wake ili jambo lake lionekane kwamba liko sahihi.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Asaa Othman Said, twende kwenye uchangiaji wa hotuba yetu na hayo hayamo kwenye hotuba, uchangie hotuba, tafadhali sana. Haya tuendelee.

**Mhe. Asaa Othman Said:** Mhe. Naibu Spika, najadili hotuba niko kwenye hali ya kisiasa. Sasa ninayoyasema ili hali hii iende sambamba na maandiko mule tunamoleta kujikwaa kwenye siasa mwaka huu iwe basi. Hawa watu mnaosema labda iwe wamekufa mchana huu, lakini Mheshimiwa nimesema chombo hiki hapa sio cha kupiga blaa blaa, ukisimama hapa unasema unasikika na dunia. Mimi ni mwakilishi wa wananchi niliyechaguliwa kwa kura nyingi mno, waliniamini sijaugua kichaa nina akili timamu hadi sasa.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema kama mwananchi wa nchi hii Mzanzibari menyu sina dowa miye. Mimi ni Mzanzibari pyuwa naipenda sana nchi hii na wananchi wake.

Ninachokisema Mhe. Naibu Spika, kama kuna chama cha siasa ambacho ndani ya moyo wangu sitokisahau mpaka kufa kwangu ni *Afro*-Shirazi ndicho kilicholeta utu wetu na heshima ya nchi hii. Lakini hatutoendelea kubaki na *Afro*-Shirazi vimezaliwa vyengine, lengo na madhumuni ni kuendeleza pale tulipoachiwa na *Afro*-Shirazi sio kuja kufikichana hivi tena, kuomba ubia huku na kule kwa

madhumuni. Tumekubaliana twendeni hivyo, atakaeshindwa ampe mwenziwe mkono hongera. Aanze kijiti aongoze wananchi wataona akishindwa na yeye wananchi watamuacha pembeni.

Mhe. Naibu Spika, maana yangu ni moja tu, tunataka haki itendeke na haki itasimamiwa na Tume ya Uchaguzi iwachiwe ifanye kazi yake bila ya kutiliwa mikono hapa na pale. Nayasema kwa sababu ishara Mhe. Naibu Spika, hazioneshi kwamba zinakwenda sambamba na mtiririko wa maandiko ya kitabu hiki, natoa tahadhari ni hilo tu.

Wananchi wetu sisi ndio mas-ul. Mhe. Naibu Spika, nimesema kwa sababu kila mmoja hapa tuliona ataulizwa na atatakiwa kujibu alivyowaongoza hawa watu. Mimi nasimama najitoa toka asubuhi nitasema nilisema. Siku hiyo *TV* zipo zile za ukweli hasa sio hizo *man made*, hazikufanywa na mtu ni zake Mwenyewe *Allah* (*S.W*). Nitaoneshwa nilivyosimama hivi nasema nini, walionisikia watasikia, waliokuja na yao tena bahati mbaya. Lakini ninachoamini sote tunajenga nyumba moja, naamini kabisa hakuna atakaedharau kiasi hicho, kujikwaa ni binaadamu tutajikwaa. Lakini ninachokisema tunahitaji amani ya ukweli, kauli hizi ziwa ni thabiti, tunataka tufike mahali stahiki ili tuwarithishe watoto wa nchi hii kwenye amani na utulivu mapenzi na mshikamano.

Mhe. Naibu Spika, jengine bado tuna tatizo la uchumi, tunahitaji kujipanga na kwenye kujipanga ningeshauri miye kufuatana na wenzetu tunaowaona wanaishi kwenye visiwa kama sisi. Mhe. Naibu Spika, watu wa Singapore wamepiga hatua kubwa sasa hivi ya kiuchumi na maendeleo hasa ya mtu. Ili na sisi tufikie pale kusema Juma, Mariyamu, amepiga hatua, tusiseme tu kwamba tukahesabu majengo sijui huduma za jamii lakini ukenda dawa hakuna, kiti mtoto anakaa chini shuleni, barabara ndio ile, *stand* imekwenda kuwekwa pale Michenzani.

Bado, tujipange wataalamu wapo Zanzibar. Wanasiasa wawaachie wataalamu wafanye kazi zao na wana sisasa wafanye kazi za siasa, lakini tunapowabana mwanasiasa analazimika. Hivyo kweli Michenzani ndio *stand*, hapana, tuwekeze kwenye elimu. Wenzetu wamekomboka hapo na wao wanatumia bahari Mwenyezi Mungu katupa bahari hii ya Hindi hebu tuitumieni. Tusivutane kwa mambo madogo madogo.

Mhe. Naibu Spika, Baraza lako Tukufu Baraza la Wawakilishi nilipopitia hapa naona kuna mambo, kuna programu hizo zimetajwa, mambo manne haya, lakini ningeshauri kamati zako za kudumu za Baraza, imetajwa kwamba watapewa taalamu, lakini tunapata taaluma nimeona. Mhe. Naibu Spika, lakini waliotutawala Waingereza wanasema kuona ni kuamini Kamati zetu za Baraza la Wawakilishi ni bahati mbaya hadi sasa sijaona, imetoka mekwenda Makurunge, imetoka Arusha,

imetoka Mwanza, tunachobadilisha huku tunaona bahari, kule tunaona maji pepo ni pale pale.

Mhe. Naibu Spika, hizi kamati ili zijifunze zitoweni ziende zione wenzetu wanafanya nini. Lazima kuwe na bajeti kila Kamati lazima itoke nje ya Afrika hii, nje ya Tanzania hii waende Botswana wakaone ng'ombe anafugwa vipi, waende China wakaone samaki wanafugwa vipi. Leo mtasema tu utalii wote, utalii kwa wote. Lakini mtu hajajua atashauri nini huyu mwakilishi. Jimbo kwake huyu atafundisha nini yeye mwenyewe hajui. UNDP wanatufadhili wanatufundisha tunakaa kama ni shule lakini sisi kwa umri huu na capteni huyu lazima aone, akiona ndio atakuja hapa kufundisha na ataishauri serikali vuzuri kabisa na pale ambapo bado atasema hapa bado wenzetu wanafanya hivi.

Mhe. Naibu Spika, wala sio matembezi yale ni masomo, wanarudi hapa timu ya Baraza wamejifunza kitu cha kusaidia Taifa hili. Yenye mwenyewe sio kwamba atakuwa mtu wa Baraza maisha, anapostaafu yupo kijijini kwake anajua afanye nini, wananchi wake awaelekeze nini. Lakini kwa mtindo huu wa sasa badom bado nasema, kamati hizi mnazifunga sana zinahitaji wigo mpana ziweze kutoka, wasafiri wakajionee mambo, wajifunze huko, wabadilishane na wenzao ili waje hapa na mawazo yatakayoweza kujenga maisha ya watu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi *Inshallah* Mwenyezi Mungu atatupa kila la kheri tumuombeni. Tumekabiliwa na mambo mawili makubwa kama kitabu kilivyoeleza; kuna kura ya maoni, katiba pendekezwa, wenyewe Wazanzibari wanajua wamependekeza nini watapiga. Kuna kura ya uchaguzi mkuu wa kuwachagua viongozi wao muhula unaokuja tujitahidini, tujitahidini kudumisha amani ya nchi hii.

Tafadhalini sana tusiwe sababu ya kusababisha maafa na majanga na kuhatarisha maisha ya watu. Damu ya kiumbe aliyemuumba Mwenyezi Mungu haimwagwi ovyo ovyo. Tusiyachanganye ya dunia tukajisahau tafadhalini sana, kheri itakuja, lakini kheri hiyo itatafsiriwa sambamba na imani zetu.

Viongozi sote tumo humu na viongozi wetu wakubwa wamebeba dhima hiyo, tuwasaidieni *Inshallah* tutafika bandarini salama na amani. Mwalimu wangu mmoja alitwambia darasani tulikuwa somo lake tumefeli wengi robo tatu ya darasa, kelele mtindo mmoja, lakini akatwambia *be cool, I want all of you to live in peace and not in pieces!* na hakuna aliyefeli. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

**Mhe. Shadya Muhammed Suleiman:** Asante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia machache katika hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kutuwasilishia hotuba hii kwa vizuri sana. Vile vile, nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mashirikiano yao wanayotupa wakati wa Kamati.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii sitokuwa na mengi ya kuzungumza isipokuwa nimesema sitotenda haki ikiwa sitoyazungumza haya, ambayo wananchi wangu wa Mkoa wa Kusini Pemba wamekuwa na kero kubwa na kwa vile leo tunaona tunazungumzia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndio Kiongozi Mkuu wa chombo hichi cha Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niendelee na pongezi zangu naomba tena nichukue nafasi hii kumpongeza Afisa Mdhamini Pemba pamoja na watu wake wote wa Ofisi ya Makamu wa Pili Pemba, na wao, kwa mashirikiano yao wanayotupa wakati wote wa Kamati tukwa katika Kisiwa cha Pemba.

Baada ya kumpongeza Afisa Mdhamini, pia nichukue nafasi hii kuipongeza Idara ya Maafa hususan kwa upande wa Kisiwa cha Pemba kwa juhudi na busara kubwa na kazi nzito waliyoifanya wakati tulipopata maafa yale katika Kisiwapanza.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitochukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Profesa Mnyaa Waziri wa Sayansi na Teknolojia kwa msaada wake mkubwa na moyo wake wa huruma baada ya kutokea tukio lile na kufika Kisiwani Pemba kuiyona hali ile na tukashirikiana naye, na yeye tunampongeza kwa dhati.

Baada ya pongezi hizo Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niangalie ukurasa wa 8 kwa ruhusa yako naomba ninukuu;

"Mhe. Spika, serikali pia imechukua hatua za kuongeza madaktari na wahudumu wengi wa afya kwa kuwasomesha na kuwapatia uzoefu. Hivi sasa nchi yetu ina madaktari wazalendo wapatao 44 na madaktari bingwa wazalendo 13. Hii ni hatua kubwa sana kufikiwa na nchi yetu."

Mhe. Naibu Spika, sitaki niseme uongo au niseme namkanusha kiongozi wangu kwamba si kweli. Ila nataka niseme tu hali halisi ilivyo hususan katika kisiwa cha Pemba na hususan katika hospitali ya Chakechake.

Mhe. Naibu Spika, nina masikitiko sana kusema kwamba hao madaktari wazalendo waliokuwemo humu kwenye kitabu katika hospitali ya Chake Chake hakuna daktari mzalendo hata mmoja.

Mhe. Naibu Spika, hakuna kitu kizuri kwa mgonjwa kama maneno matamu, unapokwenda pale hospitali ukapata faraja basi pekee unaona ni nusu ya tiba. Lakini leo Mhe. Naibu Spika, unatoka unakwenda hospitali unajuta kwa nini umekwenda kufanya nini pale, lakini huna jinsi lakini unajiuliza kwenye moyo wako.

Nasema hayo Mhe. Naibu Spika, kwa ushahidi kamili, juzi tu mie nilikuwa nina mtoto wangu alikuwepo pale alilazwa akafanyiwa operesheni, mengi nimeyaona kwa macho yangu. Lakini hapa sio wakati wake nasubiri Wizara ya Afya, lakini kuna mambo haya muhimu wakati tunasema tunazungumza hotuba ya Makamo wa Pili wa Rais ambaye ndiyo kiongozi wa serikali basi nilisema kwanza niliseme.

Mhe. Naibu Spika, hospitali ya Chake Chake kuna mgomo, ukenda pale mtu anaweza akafanyiwa upasuaji akaa siku tatu hajapitiwa pale na mambo mengine. Lakini kubwa zaidi Mhe. Naibu Spika, sijui niseme Waziri aje anieleze, naomba waziri aje anieleze. Hiki kifaa cha *HIB* cha kupima ule wingi wa damu katika hospitali ya Chake Chake pale hakuna, ni aibu. Sasa nilikuwa nataka nijue kifaa hiki kinathamani ya shilingi ngapi mpaka tukakosa kipimo kile mgonjwa yupo mahututi anataka kufanyiwa upasuaji haijulikani damu yake ikoje ana kiasi gani, ina mudu au haimudu, wewe uhangaike. Kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hebu anieleze hichi kifaa hiki ni kiasi gani?

Nikitoka hapo Mhe. Spika, niende ukurasa wa 9 kwa ruhusa yako vile vile naomba uniruhusu ninukuu, masuala Mtambuka;

"Mhe. Spika, utunzaji wa mazingira ni suala muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Nchi zote duniani zinatoa kipaumbele katika suala hili kwa maendeleo endelevu na kupunguza umasikini. Kwa kutambua umuhimu huo, serikali imekuwa ikihimiza wananchi kupanda miti kwa wingi na kuachana na tabia ya kukata miti ovyo na uchimbaji wa rasilimali zisizorejesheka kiholela."

Mhe. Spika, ni vyema ni maneno mazuri na ni kweli, lakini kama hivi ni sawa Kisiwa cha Pemba sote tunakifahamu, hebu nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze, Kisiwapanza jamani inakwenda zake. Kisiwapanza Mhe. Makamo wa Pili inakwenda zake na sio Kisiwapanza tu lakini tunasema ile hali halisi ipi iliyomzidi mwenziwe, Kisiwapanza hatunayo tena. Tukenda Makombeni na sehemu nyengine nyengine lakini hususan leo hapa nitalizungumzia suala la Kisiwapanza. Hali ni hatari kwa wananchi wetu Mhe. Makamu wa Pili.

Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze kama serikali ina mpango gani imejitayarisha vipi, kuhusiana na suala hili zima la wananchi wetu wa Kisiwapanza ili kunusuru maisha yao.

Nikimaliza ukurasa wa 9 Mhe. Naibu Spika, nakuja ukurasa wa 10, mapambano dhini ya ukatili na udhalilishaji wa jinsia. Tatizo la ukatili na udhalilishaji kwa jinsia dhidi ya wanawake na watoto bado lipo na kila siku tunazungumza humu ndani tunasema lakini kila tukiamka mambo ndio yanazidi. Vile tukizungumza naona kama tunawatia kasi hao mabwana huko nje lakini tatizo hili Mhe. Naibu Spika, linakuja kwa nini, adhabu zetu kwanza ni ndogo, hatimaye wewe utakwenda pale wewe utaambiwa hakuna ushahidi.

Leo utamkuta mtoto ushahidi wote uko wazi mtoto mdogo leo unaambiwa ushahidi haupo sijui unatakiwa ushahidi upi Mhe. Naibu Spika. Kwa kweli jambo hili sisi kama wanawake kama wazazi linatuumiza hatulali hatuwazi, mtu ukitoka kidogo tu unakuwa na wasiwasi na watoto wako, jamani nikirudi wanangu wako salama, unaelekeza kama huna akili vizuri. Tuiombe jamani Serikali iliangalie kwa makini suala hili, suala bado hili lipo tena kwa kasi linaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mimi sitokuwa na mchango mkubwa, kabla ya kumaliza Mhe. Naibu Spika, kuna suala moja nimelisahamu naomba nilizungumzie kuhusu maafa. Maafa ni makubwa na maafa sote tunayajua na tumepata maafa Mhe. Naibu Spika, hatutoyasahau maisha. Kwa vile leo tunazungumzia hii Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndio Kiongozi Mkuu wa Serikali, Mhe. Naibu Spika, tuliambiwa meli ya Serikali itafika mwezi wa tano, mwezi wa tano unamaliza hebu Mhe. Waziri akija anieleze hii meli ya Serikali itafika lini?
Wananchi wa kisiwa cha Pemba tunaumia, juzi wananchi wameingia kwenye *M.V.* Maendeleo wamekwenda kuwekwa kule mtihani, inatusikitisha hatulipendelei suala lile. Tunamuomba Mhe. Waziri atueleze atakapokuja hapa hii meli ya Serikali itafika lini, mtu wa Pemba ukilala una safari kuja Unguja unafikiria meli. Ndege wengine hawana uwezo, huyo mwenye uwezo sasa hivi ndege inatisha ukiangalia uwanja wetu wa Pemba. Hatusemi mengi Mhe. Naibu Spika, tunasubiri hizo wizara husika zifike hapa patachimbika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache kwa niaba ya wanawake wa Mkoa Kusini Pemba ninaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Abdi Mosi Kombo:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichangie hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Naanza ukurasa wa 5 kifungu 13.0 kinachosema kwamba hali ya uchumi wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, kwa *item* zinazoonesha kwamba hali ya uchumi Zanzibar imekua na desturi ya uchumi unapokuwa wananchi wake wanakuwa hali nzuri.

Mhe. Spika, nikenda katika huduma za jamii nchi yetu ina wananchi wengi sana kuna wakulima, kuna wafanyakazi, kuna vijana, kuna wanawake na kuna wanaume. Nikenda katika huduma za ukulima hivi sasa hali ya ukulima Zanzibar imekuwa duni kwa sababu wakulima wetu hawapati vifaa vya kulimia. Matrekta yamekuwa kidogo, madawa shida, mbolea shida.

Kwa hivyo, ninaiomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ihakikishe kwamba inaiambia Serikali pamoja na Wizara yake husika ya Kilimo kuhakikishia wananchi kuwapatia wananchi vifaa kama matrekta kwa uhakika kwa sababu wakati inapofika *season* ya kulima matrekta inakuwa hakuna, madawa yanakuwa shida, mbolea matatizo. Kwa hivyo ninaiomba Wizara husika iwahakikishie wananchi kilimo cha uhakika wakati unapofika.

Mhe. Naibu Spika, nikenda katika huduma za jamii, katika huduma za jamii nchi yetu ina vijana wanahitaji elimu kusomeshwa nyanja ambazo za kuweza kuleta maendeleo kama vile sekta za viwanda, vijana wakasomeshwe sekta za viwanda ili wakati wanapomaliza masomo yao wawe na uhakika kwamba wanafanya kazi za kimaendeleo.

Katika huduma za jamii nchi yetu imeleta sekta moja ya utalii, sekta ya utalii sasa hivi tunayo ni ya kupunguza matatizo ya ajira katika vijana wetu wa Zanzibar. Kwa hivyo ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba vijana wa Zanzibar wanapata huduma katika sehemu hizi za utalii. Nchi nyingi katika dunia zinaangalia wazalia kwanza kuliko wageni kwa sababu wazalia ndio wanaojenga nchi. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ningeiomba Serikali iangalie hasa na Mhe. Waziri anayehusika atembelee katika mahoteli ya Zanzibar kuhakikisha kwamba, je, vijana wa Zanzibar wapo na wanaajiriwa kiuhakika ndani ya sekta hii ya utalii.

Nikenda huduma za jamii ninaishukuru Serikali katika bajeti hii ninamshukuru Waziri wa Fedha kutenda fedha za kuwasaidia wazee kuwapa pencheni wazee wanaofikilia miaka 70 Zanzibar, kwa hivyo ninaipongeza Serikali pamoja na Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kulihakikisha jambo hili katika nchi yetu ya Zanzibar ili kupunguza makali ya kasi ya umasikini kwa wazee wetu wanaofika miaka 70, kwa hivyo napongeza.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika sehemu ya maafa, ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba inaangalia matatizo ya maafa. Kwanza tuna maafa tuliyokuwa

nayo katika nchi yetu hasa maafa ya njia za barabarani na magari, magari yetu hivi sasa Zanzibar yamekuwa mengi na yanakwenda kwa kasi. Utazikuta daladala hivi sasa zinazokwenda sehemu ya mashamba zimepakia watu na wengine wanani'nginia kwa hivyo ni moja katika maafa. Kwa hivyo ninaiomba Serikali kupitia Wizara inayohusika iangalie magari yanayopakia watu waliokuwa wanani'nginia na madereva wale wachukuliwe hatua.

Gari imepakia ndani ya gari mna watu kuliko maana yake kile kiwango kilichokuwa ndani ya gari ni kikubwa na wale wanaoninginia ni wengi na barabara zetu mbovu. Ukipita barabara yetu hii kutoka mjini kwenda huko Mkokotoni, sasa ukiangalia hiyo barabara yenyewe na watu wanaopakiwa katika magari ni maafa kamili.

Kwa hivyo Serikali iwe macho kuangalia madereva wanaopakia watu namna ile, yale ni maafa makubwa sana, njia zenyewe ni mbovu madaraja mabovu sasa na *speed* ya gari tunayokwenda ni kubwa na magari yenyewe ni mengi. Kwa hivyo ninaiomba Serikali ihakikishe kwamba wanaopakia watu kama wale wanaojaza *over limit* wachukuliwe hatua.

Mhe. Naibu Spika, katika maafa yanayotokea kila mara ndani ya nchi yetu, mafuriko ni rehema ya Mwenyezi Mungu lakini na binaadamu tumepewa akili tuzitumie. Mwenyezi Mungu katupa akili tuitumie. Sasa wenzetu wengine wanajenga nyumba ndani ya mto kwa sababu Mwenyezi Mungu kaumba kila kiumbe kakiwekea sehemu yake, mwanadamu kamuwekea sehemu yake, mnyama kamuwekea sehemu yake na maji yamewekewa sehemu yao.

Kwa mfano mwanaadamu anapokwenda porini kwenye mbuga za wanyama, basi wale wanyama hustaajabu kiumbe hiki kimefika vipi kwa hivyo tukile, unaliwa kwa sababu si *position* yako ile ni *position* ya wanyama. Sasa na maji yana *position* yake Mwenyezi Mungu aliyoyaweka, unajenga ndani ya mto unagombana na maji, maji yatakuuliza wewe umekuja kujenga hapa kwa nini pako?

Sasa utakuta haya ni maafa, wakati mwegine maafa tuyaangalie kwa kiakili kujenga nyumba ndani ya mto ni kutafuta maafa. Kwa hivyo ninaiomba Serikali inapopimia watu viwanja iwapimie sehemu ambayo inahakikisha hapa hapaingii maji.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuheshimu wakati wako mimi namalizia hapa Serikali ihakikishe kwamba tunajikinga na maafa kwa kuwapimia wananchi viwanja sehemu ambazo inastahiki kupimiwa viwanja. Ahsante.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Ninakushuru sana Mhe. Naibu Spika, jioni hii ya leo kunipa fursa na mimi kuchangia mawili matatu katika hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2015/2016. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa na mimi kwa sababu ni mjumbe wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, basi mchango wangu utakuwa sio mkubwa. Lakini pia naomba samahani kidogo kifua changu kina makwaruzo ruzo kidogo kwa hivyo nitakapokuwa nakohoa kohoa itabidi munisamehe tu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa na mimi nataka nianze hapa kwenye hali ya kisiasa kwa kweli hali ya kisiasa katika nchi yetu kama walivyosema kwenye kitabu kama ni nzuri, mimi nakubali kama ni nzuri. Lakini uzuri wake unahitaji kutiliwa nyenzo na nyenzo zitapatikana kwa sisi viongozi vya kisiasa tusiangalie mbele zaidi, maslahi ya kisiasa kuliko kuwaangalia wananchi wetu katika hali ya nchi yetu ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, juzi nilikuwa ninaangalia Burundi, niliona hali ya waburundi wanavyoihama nchi yao wanavyokimbilia Tanzania kutokana na mgogoro wa kisiasa ulioko Burundi. Waheshimiwa amani ina ila moja, amani inakuwa ni nzuri kwenye nchi pale ambapo ipo imedumu, lakini amani mkiichezea maana ikivurugika hiyo amani kuirudisha kwake ndio inakuwa na gharama kubwa sana.

Kwa hivyo ninawasihi sana viongozi wetu tusiangalie tu maslahi ya mbele ya kisiasa tuangalie na amani na matatizo ya wananchi wetu. Wenzetu wa Burundi wao ni Bara wana maeneo ya kukimbia mara moja na kuingia kwenye nchi nyengine. Lakini Zanzibar ni visiwa tuangalie tu wakati wa mwaka 2001 wakati kulipovurugika kwa maandamano Pemba, wananchi wangapi walikufa baharini kwa kukimbilia Mombasa.

Kwa hivyo wazee wangu, viongozi wangu ninawasihi sana tusichezee amani kwa kusema kwa midomo tu lazima amani tuidumishe kwa vitendo. Nawaomba sana panapostahiki kukaa mkazungumza pazungumzwe, panapostahiki kufanywa pafanywe lakini tusichezee amani tuliyonayo tukaja jilaumu baadae, maana kuirudisha ndio kazi.

Waheshimiwa katika nchi yetu tulikuwa tuna matatizo mengi tulikuwa hatuzikani, hatusali pamoja, hatuli pamoja, hatuchezi pamoja, hata katika Baraza la Wawakilishi, Baraza la Wawakilishi Kongwe ndio nimewahi nikiwa kule tulikuwa hatukai kama hivi. Ilikuwa upande na upande mwengine tunaangaliana hivi kama majogoo. Waheshimiwa ile ilikuwa ni tabu kwa sababu ilikuwa hapana anayemuamini mwenziwe.

Mimi ilikuwa siwezi kumuamini mwenzangu rafiki yangu alikuwa Mhe. Naibu Spika, lakini hivyo nikenda kwake yeye basi nilikuwa ninajificha. Kwa sababu nikenda nikionekana nikirudi nitaambiwa tayari keshachukuliwa yule. Waheshimiwa ninawaomba sana, tukumbuke nyuma tulikopita na tulipo sasa.

Tulifanya Serikali ya Umoja wa Kitaifa nchi zote zinastaajabu kutokana na hali tulivyo, kwa hivyo tusije tukarudi nyuma kwa kuchezea amani hii. Kwa hivyo tusije tukarudi nyuma kwa kuchezea amani hii. Kwa hivyo tusiisifu kwenye vitabu tu, lazima isimamiwe iwe ya kweli na kusimamiwa kwake ni kuwa wakweli sisi wenyewe tukafanya mambo ambayo yanastahiki kufanywa yasiwe yale ya kuichezea amani na tukaibomoa amani tukawa tunasoma kwenye vitabu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nilikuwa nataka nilizungumze ni suala hili la maafa. Kama walivyozungumza wenzangu, waheshimiwa tumeshuhudia katika mvua hizi zilizopita za karibuni wananchi wa Zanzibar wamepata matatizo walio wengi nyumba zao zimeingia maji, mafuriko ya majumbani yamechukua vifaa vya watu, yamechukuwa mali za watu, wengine walikuwa hawamo kwenye majumba yao wakija kwenye majumba yao maji tayari yashachukua kila kitu.

Sasa waheshimiwa maafa haya mtu hujifunza kutokana na kosa ambalo amelifanya nyuma. Na waswahili wanasema ukiona mwenzio ananyolewa basi wewe tia maji.

Sasa waheshimiwa mimi ninazungumzia bwawa lilioko Kwerekwe, katika suala ambalo limesababisha maafa makubwa katika nchi yetu kwa sababu hizi mvua zinazopita moja ni bwawa la Kwerekwe lile limeua watu wawili. Lakini hata hivyo barabara zote zimefungika kwa bwawa lile la Kwerekwe, imebidi sasa sisi tunaokaa Fuoni hatuna njia ya kupita ilikuwa tunatumia kibarabara kimoja uchochoro ambao ni hasara tupu, huo uchochoro wenyewe sasa hivi umevurugika mashimo matupu hakuna hata ile njia ya kupita.

Sasa basi ninaiomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliangalie lile bwawa liliopo pale Kwerekwe na kama kuna ushauri wowote ule wa kitaalamu, basi wapeleke wataalam ili pashauriwe tuliangalie lile bwawa kama ni kuchimbwa chini zaidi maji yaingie lakini yasiwe vile yakaziba barabara lichimbwe. Ama ni kuhamishwa kwa mitaro lakini lihamishwe, almuradi Serikali ielekeze nguvu zake katika bwawa lile la Kwerekwe, ni tishio. Kwa sababu njia inayokwenda Makunduchi, Fuoni na kuna vyuo, kuna Ofisi ya Bunge, kuna vyuo vyetu lazima watu wanataka njia ya kupita. Sasa njia kama ile haipo ni matatizo makubwa na ilikuwa ni matatizo makubwa yaliyotupata, kwa sababu ilikuwa mtu kama anakwenda Fuoni kwamba muda wa robo saa basi alikuwa anakaa zaidi ya masaa sita kwenye foleni hajafika. Kwa hiyo, naiomba sana serikali iliangalie suala hili, na ikibidi kama kuna njia nyengine ya kitaalamu ya kupata barabara nyengine basi

iangalie, lakini pale bwana ni tishio kubwa na tumeona pamesababisha maafa makubwa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambao nataka nilizungumzie ni suala la Ofisi ya Faragha ya Makamo wa Pili wa Rais. Mheshimiwa sisi zamu hii tumefanya safari ya kwenda Dar es Salaam katika kamati yetu, madhumuni ya kwenda Dar es Salaam ni kuangalia ofisi au makaazi ya viongozi wetu. Mheshimiwa kwa kweli naomba sana serikali kwanza nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais anayoishi Dar es Salaam hailingani kabisa na hadhi yake. Kwa hiyo, naiomba serikali iliangalie kabisa kwa macho mawili kama nyumba ile ifanyiwe matengenezo makubwa ili iendane na hadhi ya kiongozi wetu. Kwa sababu kama kiongozi wetu akikaa makaazi ambayo kuwa hayastahiki ni aibu kwa nchi yetu yote.

Pili, Makamo wa Kwanza wa Rais na yeye kule Dar es Salaam anakaa kwenye nyumba za kukodi, kwa hiyo na hili naomba sana viongozi wetu watafutiwe nyumba ambazo watakaa kwa sababu kama hakuna makaazi ni aibu kwa viongozi wetu. Kama ninavyozungumza Mheshimiwa hili suala naiomba serikali ilipe kipaumbele na iliangalie, ili viongozi wetu wapate wakae kwenye nyumba ambazo wana hadhi na wanafanana na kukaa katika nyumba hizo.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala la Ofisi ya Wapigaji Chapa. Mhe. Naibu Spika, ofisi hii imerekebishwa na tunashukuru kama wanafanya kazi vizuri kikamilifu. Kama tulivyoelezwa kwenye kitabu, vitabu vyote vya bajeti wanachapisha wao, miswada ya sheria wanachapisha wao na kazi nyengine wanafanya. Mhe. Naibu Spika, lakini tunaomba serikali pia iangalie kama ile ofisi ni muhimu kwetu haiwezekani sasa hivi kama kuna magazeti yaende yakatiwe rangi Dar es Salaam. Kwa hiyo, serikali ifanye kila aina ya njia lakini mambo haya yafanyike pale kwenye Ofisi yetu ya Mpiga Chapa. Ni aibu kwa serikali yetu kuwa magazeti yaende yakachapishwe Dar es Salaam kwa ajili ya kutiwa rangi magazeti, ni aibu.

Kwa hiyo, na hili serikali ione kama ifanye jitihada ya kuwa kama kuna magazeti yanayotaka kuandikwa, yanayotaka kutiwa rangi iwe ni hapa hapa kwetu. Kwa sababu hii itakuwa inasaidia mapato katika nchi yetu leo fedha ngapi zinakwenda zikitumika Dar es Salaam ambazo zinapatikana hapa kwa wapiga chapa wetu. Kwa hiyo, naomba na hili serikali ilione na ilifanyie kazi, Waziri wa Fedha yumo humu anasikia.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nataka nizungumze nimalizie kama nilivyokwambia mimi masuala yangu kwa hili itakuwa ni suala dogo ni suala la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, suala la Baraza la Wawakilishi mimi nataka nizungumze kitu kidogo kwa masikitiko, kwa sababu Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi tumeshapiga kelele sana kule. Mimi sitaki hata niseme humu maana nikisema naona kama mtu akifunua sana funga zake atakuwa yeye mwenyewe ah bora naona mimi niache tu maana nikisema naona itakuwa kama najikashifu mimi mwenyewe, najidhalilisha kwa hiyo, basi naona bora niache.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja hizi zote.

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:** Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii nikiwa mzima wa afya.

Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kusimamia ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, pia nimshukuru Makamo wa Pili wa Rais kwa kutuwasilishia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Pia, nimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili pamoja na watendaji wake wote kutuandalia hotuba hii yenye malengo mazuri na serikali.

Mhe. Naibu Spika, nipongeze Ofisi ya Makamo wa Pili kwa kusimamia wizara zote za serikali hasa kwa upande wa kupata pato la Taifa. Mhe. Naibu Spika, kusema kweli wizara ya Makamo wa Pili inasimamia vizuri wizara zake zote na inastahili sifa nyingi. Mhe. Naibu Spika, pamoja na kusifu kupanda kwa pato la Taifa mimi Mheshimiwa kwa dhati ya nafsi yangu mpaka tumefikia hapa kusema kweli hotuba hii nimeipokea kwa mikono miwili na ninastahili sifa nyingi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije katika huduma za jamii, pia nipongeze serikali kwa kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha huduma ya elimu, afya, maji safi na salama pamoja na makaazi ili kuleta ustawi mzuri wa jamii.

Mhe. Naibu Spika, niende katika sekta ya elimu, ni kweli sekta ya elimu imejitahidi kama ilivyojieleza hotuba ya Makamo wa Pili kuwa hatua nzuri iliyofikia ya ujenzi wa skuli wa madarasa mapya kwa skuli mbali mbali pamoja na ununuzi wa samani na vitabu kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli sekta hii imejitahidi inastahili sifa, mimi leo kila panapokuwa pazuri itabidi nisifu. Mhe. Naibu Spika, sekta hii ya elimu imejitahidi kwenye ujenzi kusema kweli mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Ustawi nimeona majengo mapya, ni kweli majengo mazuri na kweli majengo yapo lakini

ninachoomba hapa mapendekezo yangu baada ya kujenga ujenzi wa chini sasa tubadilike tujenge ujenzi wa ghorofa. Pia kwenye samani hapa pia maoni yangu naona kwenye samani baada ya kuwapa watu binafsi kwenye kuchonga, mimi naona serikali isimamie hapa kama Wizara ya Elimu inayo Chuo cha Mikunguni, chuo kile ni kizuri na uwezo wanao kwa sababu kwenye Wizara ya Elimu tayari wameshawakopesha kwa hivyo uwezo wa kutengeneza samani upo.

Kwa hivyo, baada ya kwenda kupeleka tenda kwa watu wa nje kwa hivyo tutumie idara zetu hizi za serikali kuona tunapungukiwa kidogo na thamani ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye sekta ya afya. Sekta ya afya nayo pia niipongeze kwa kazi nzuri inayofanya mimi pia nikiwa Kamati yangu inahusiana na mambo ya afya kusema kweli imefanya vizuri inastahili sifa tena sifa, kwa sababu mimi nimepata bahati kipindi chote tangu nilipoingia Barazani nilikuwa kwenye Kamati hii ya Ustawi wa Jamii. Kusema kweli Wizara ya Afya imejitahidi sana kila mwaka tunapokwenda kwenye kamati tunaona utekelezaji unavyotekelezwa.

Kuhusu *ICU* kwenye chumba hiki cha *ICU* kusema kweli Mhe. Naibu Spika, tumekwenda kukiona chumba ni kizuri lakini tatizo lilokuwepo pale tatizo la madaktari bingwa. Mhe. Naibu Spika, muda huu chumba hiki hakiwezi kufanya kazi kwa sababu hapana madaktari bingwa wanaoweza kuhudumia *ICU*.

Kwa hivyo, hili ni tatizo kwa sababu chumba kilichokuwepo kina vitanda vitano, lakini hiki kilichokuwa tayari kilichokuwa kipya ni kikubwa, ni kizuri kina kila kitu kusema kweli sekta hii imejitahidi.

Mhe. Naibu Spika, pia niipongeze sekta hii kwa kuwa na kitengo cha upasuaji vichwa na uti wa mgongo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Naibu Spika, kusema kweli jengo lilokuwepo ni zuri na tayari kazi wameshaanza kufanya, naipongeza sana sekta hii.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije katika Ofisi ya Faragha, mimi nilikuwa najiuliza ofisi hii kipindi kilichopita bajeti iliyopita tulileteWa taarifa kuhusu ofisi hizi kuimarisha Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kusimamia makaazi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa kuzifanyia matengenezo nyumba za Mazizini, Dar es Salaam na Dodoma.

Bajeti iliyopita pia ililetwa kama hivi lakini leo pia hotuba imeeleza kama ilivyo sijaona maendeleo kutoka mwaka jana imefikia wapi. Kwa hivyo, utakapokuja kutoa majumuisho nipate taarifa kwamba ofisi hizi kipindi kilichopita walikuwemo kwenye bajeti limefanyika lipi na lipi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije katika Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, niipongeze tume kwa kazi zake nzuri inazofanya kwa kupanga malengo yao ya kazi mbali mbali hasa kwa kuzingatia mwaka huu tuna uchaguzi. Mhe. Naibu Spika, mimi naipongeza sana Tume ya Uchaguzi kwa mipango yao mizuri waliyokuwa wamejipangia, naomba dua isimamie vizuri kipindi hiki tunachoingia cha uchaguzi tufanye uchaguzi kwa salama na amani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi naunga mkono hoja mia juu ya mia.

**Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza hatuna budi sote sisi tuliokuwemo humu ndani kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wa pumzi ambaye ametupa mpaka muda huu.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kazi kubwa yenye uvumilivu, usikivu na busara kupitia kiongozi wetu mpendwa kwa Baraza hili mzee wangu Mhe. Balozi Seif Ali Iddi pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kaka yangu Mohammed Aboud pamoja na watendaji wake wote wa Wizara ya Makamo wa Pili wa Rais, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa uvumilivu na kwa hekma na busara mpaka wakatuletea kitu kama hiki.

Naomba nichukue nafasi hii kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Uzini kuishukuru na kuwaunga mkono kwa kazi ambayo yenye machofu makubwa sana, lakini wakawa wastahamilivu.

Mhe. Naibu Spika, nashkuru kitabu hiki ameeleza mambo mengi sana na hasa katika suala la mapambano ya rushwa. Mhe. Naibu Spika, Baraza lote ambayo yenye kuwakilisha wananchi duniani kote katika hasa mapambano ya rushwa, Baraza hili la Wawakilishi, Bunge wananchi ambao tunawakilisha wanakuwa na matumaini makubwa sana hasa kuangalia ni kitu gani ambacho lengo ni kuwaletea faida wananchi, kwa upande wa Zanzibar.

Sasa Mhe. Naibu Spika, tunaposema mapambano ya rushwa sote tunatakiwa tukiwemo sisi viongozi tuliokuwa humu ndani tunapoamka sote huwa tunajitizama kwenye kioo kabla hujatoka. Sasa Mhe. Naibu Spika, Baraza hili ni uzuri tukawa na maadili ambayo ikaonesha mfano kwa watendaji ambao tunakwenda kuwatumikia na kwenda kuwafanyia kazi.

Maana yake Mhe. Naibu Spika, Baraza hili Wawakilishi sisi tuna majukumu mengi sana, sasa kama maporomoko ya maadili kwa utendaji wetu si mzuri matokeo yake

hata hizo kamati za kuwatumikia wananchi na kwenda kufanya kazi, hatutopata yale mambo ambayo tuliyotakiwa kuyafanya kwa wananchi.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi ningeliomba kwamba hili Baraza linatutizama kwa nyanja zote za Zanzibar na Tanzania, kwa hivyo ni vizuri tukajenga jambo la kupendana, jambo lenye ukweli lakini jambo si la ubinafsi umimi, umimi, umimi. Lakini tuifanye kazi hii ili kuwapelekea matumaini wananchi ambao waliotufikisha hapa tumefika.

Mhe. Naibu Spika, hiki ni kipindi cha lala salama Mwenyezi Mungu akitujaalia kwa upande wangu kiti hiki ninachokizungusha nimekuja kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi, sikuja kama Raza wala Kampuni *Hassan and Sons* na ikifika muda kama wenzangu walioingia na wakatoka nitarejesha kiti hiki kwenye Chama cha Mapinduzi. Sasa Mhe. Naibu Spika, katika vitu hivi tunatakiwa sote kwa pamoja ili tukimaliza muda wetu au kila mtu muda wake ni uzuri Mwenyezi Mungu alitujaalia kwamba tukitoka tukumbukwe kwamba kulikuwa na nini.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nikija kutokana na hali ya siasa ni sisi wenyewe nafsi zetu kujiuliza, na kwa sababu tuko kwenye ushindani, na kwenye ushindani tunatakiwa uvumilivu tujadiliane, tuvumiliane, tuheshimiane. Sasa ni vizuri tukatoka sote kwa pamoja kwa kujenga mashirikiano kwa faida ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba kutoa tahadhari kwamba vyama vya siasa vinavyohubiri siasa ni vizuri wakahubiri maendeleo na faida namna ya kukosoana. Tumekuwa ndani humu tunakosoa mawizara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mfumo Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sasa ni vizuri tukaendesha utamaduni wetu kama tulivyo ndani.

Mhe. Naibu Spika, lakini suala la madhehebu, dini tusilifanyie mzada katika mambo ya siasa ni zito halivumiliki wala halikamatiki, suala la madhehebu ni suala zito sana. Kuna mfano wa karibuni hapa kuna wenzetu wa nchi moja ya Ulaya walikwenda vijana au kikundi kikafanya kikatuni cha Mtume wetu *(S.A.W)*, mimi nakilani sana. Lakini mimi kama Raza naweza kuwa mstahamilivu kwa sababu yule ni Mtume wetu wa mwisho ambaye ameletwa na Mwenyezi Mungu hasemi isipokuwa wahai, sasa unapoanza jambo kama lile mimi naweza kuwa mvumilivu lakini mwenzangu akasema potelea mbali kwa sababu unagusa dini, siku nyengine unagusa madhehebu na matokeo yake mnayaona yanavyotokea.

Sasa kuna vitu hivi uvumilivu wa kusema, wa kuhubiri, na wa kusimamia kila jambo na uvumilivu wake na kila jambo lina mipaka yake. Mimi ningelimuomba Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mzee wetu Dokta Ali Mohammed Shein kusimamia hii sheria, sheria, sheria. Hili nampongeza Dokta

Shein kwa kweli ameweza kuifanya tukafika hapa tulipofika pamoja na wasaidizi wake. Sasa vitu kama hivi tukiviacha vinaweza kuleta vitu ambavyo havisaidii, tumekuwa na amani, tumekuwa na utulivu, tumekuwa na mshikamano. Mwenyezi Mungu atujaalie mwezi huu leo mwezi mosi Shaabani kwetu sisi ni mwezi mkubwa sana Mhe. Naibu Spika, tuna siku kama 24 nyengine kuelekea Ramadhani.

Kwa hivyo, matumaini kwamba sote tuna uvumilivu wa kukaa pamoja kujadiliana, kupendana kama tulivyo hivi tukitoka tuweze kujenga Zanzibar yetu imara.

Mhe. Naibu Spika, nitakuja katika suala hili la maafa. Mimi niipongeze kwa dhati kabisa Kamati ya Maafa ambayo inasimamiwa vile vile na Mwenyekiti wake na inasimamiwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Kwa kweli suala la maafa ni mitihani ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu anatwambia atatuletea mitihani kila aina mali, ugonjwa, maafa, vitu vingi lakini mwisho anatwambia wapeni habari nzuri wanaosubiri.

Vile vile,  suala la maafa na sisi kama wananchi tunatakiwa tuwe na usikivu serikali inavyotwambia, viongozi wanavyotueleza. Lakini sehemu pana mtaro wa maji sasa huu unapita unakwenda baharini nakuja mimi Raza nakwenda kujenga nyumba yangu kwenye mtaro wa maji. Sasa kuna vitu vyengine ni mitihani ya Mwenyezi Mungu lakini serikali inakuwa inabeba lawama haitizami kwamba tatizo lile limetokana na nini na matokeo yake tumemsikia juzi Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipozuru Kinondoni kule, kwamba yale maji yalikusanyika kwa sababu kuna nyumba zilijengwa ndani ya mtaro wa maji ambao wa kusukuma kupelekwa baharini matokeo yake sasa aliyekuwemo na asiyekuwemo.

Janga lile Mwenyezi Mungu awasaidie limekuja matokeo yake imebidi serikali sasa kwa huruma inagharamika mara nne ambapo haina kwenye bajeti, haipo kwenye makisio matokeo yake yameingia vile yalivyoingia. Kwa hivyo, mimi nasema serikali ni wananchi sasa sisi kama wananchi lazima tuwe wasikivu katika vitu kama vile.

Mhe. Naibu Spika, vile vile suala la watendaji vitu hivi kuna Diwani, Sheha, kuna vyombo vingi vinavyohusika. Sasa mimi nafikiri tuanze kutoa elimu ya kutosha ili kuepukana na maafa haya.

Mhe. Naibu Spika, Mwenyezi Mungu anapoleta mtihani utakuta nchi imezolewa. Kathmandu juzi nusu ya nchi imekwenda zake India, ni mitihani ya Mwenyezi Mungu mtikisiko wa ardhi ambapo hakuna mtu aliyekuwa amejua. Kwa hivyo,

kuna vitu ambavyo vinatakiwa wananchi wawe wasikivu wakati serikali inapokuwa inatoa taarifa za maji, habari ya mvua za masika na taarifa zake, lakini tunapokaa tukasema aa sasa ndio matokeo yake hayo tunakuja kuilaumu serikali.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka kutoa mawazo kwa kamati hii ya maafa. Kamati ya Maafa inakuwa na bajeti yake lakini wakati mwengine inaishiwa inatokea mtihani. Sasa mimi naiomba kamati tutoe mashirikiano, serikali ni sisi wananchi sasa kila mwananchi ajiulize kaifanyia nini serikali yake. Sasa katika hili Mhe. Naibu Spika, mimi ningeliomba kamati nzima hii inayosimamia haya maafa yanapotokea sisi tuna wahisani, sisi wengine wafanyabiashara.

Kwa mfano, mimi nimekuja hapa kwa niaba ya Uzini lakini vile vile ni mfanyabiashara ninao ushawishi mzuri kwa Mwenyezi Mungu kuwashawishi wenzangu waliokuwa ndani ya nchi, nje ya nchi Wazanzibari kusaidia haya mambo. Sasa vitu kama hivi kamati imeshakaa, niliiona kamati inakaa lakini kama tuna *problem, what is the solution, what is next*. Kamati hii imekaa imejadili, imeona lakini sasa pale tunahitajia vianzio vya kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano yalipotokea Kisiwapanza Mwenyezi Mungu alipoleta mitihani yake maana yake ile ni mitihani ya Mwenyezi Mungu kuamini kwamba sisi sote tunaringa na pumzi, sote tumezaliwa na mchanga tutazikwa na mchanga, *we are all transit.* Lakini Kisiwapanza mfano imekuja mitihani mimi nilizungumza na Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, kwa bahati nilikuwa simjui nilipewa nambari nizungumze naye nikampigia simu Mkuu wa Wilaya ya Mkoani Pemba, nikamwambia bwana mimi ndugu yako Raza, mfanyabiashara, mwananchi na kwa sababu mitihani hii ni yetu sisi bila ya kuchagua rangi, kabila ndio utamaduni Mwenyezi Mungu aliyotujaalia. Zanzibar *is the cosmopolitan* basi nikamwambia hebu niambie sisi kama Wazanzibari wafanyabiashara na wenzangu wako nje tusaidie nini Kisiwapanza na nasikia kuna taarifa hali si nzuri ya umasikini kwa ndugu zetu wa Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati katika kuzungumza akanambia vile vile kuna ukosefu wa madawa Kisiwapanza. Mimi nikamwambia orodhesha kila kitu katika vitu hivi tuambie mahitaji yako, hawa wenzangu pesa *cash* hawana wana vifaa kama saruji, nondo, mabati, chakula, madawa tuelezee na sisi tutakwenda kwa utaratibu kama madawa tutashirikiana na hospitali.

Mhe. Naibu Spika, ninashukuru mwenzangu kanipokea na hivi sasa bado nilimwambia nakupa zaidi ya siku sita, kwa bahati nzuri ni kijana mzuri na nafikiri analifanyia kazi. Lakini sasa hii inaingia wiki ya pili bado nafikiri kuna tatizo la mawasiliano. Kwa hivyo, inawezekana Mwenyezi Mungu kamjaalia ni kijana

mzuri Mwenyezi Mungu ampe imani nimeambiwa ana mkakati mzuri, anafanya kazi, lakini vile vile anatakiwa awe na wasaidizi.

Sasa ningeliomba hii Kamati kwamba mambo haya yanapotokea tuitwe wananchi sisi tunaipenda nchi yetu, tuna uchungu na nchi yetu tuitwe. Bwana kuna hili la maafa serikali ndio sisi, kwa hivyo hapa kuna tatizo moja, mbili.

Hivi karibuni niipongeze *ZBC*, kwa bahati mbaya nilikuwa nyumbani usiku basi nikaifungua nikakuta mitihani ya wenzetu Mwenyezi Mungu aliyowaletea, Pita na zako Mkoa wa Kaskazini. Kwa bahati nzuri siku ya pili asubuhi nikamtuma dereva nilipomtuma bahati nzuri na wenzangu wote wengine kwa sababu ni suala letu basi yule dereva aliporudi akanambia kuna tatizo moja, mbili, tatu na bahati nzuri nikawasiliana na Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa ambaye vile vile ni bosi wetu kwenye Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu tulikuwa kwenye semina nikawasiliana naye Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nikamueleza kwamba bwana nina ziara ya Kaskazini, Pita na zako ndugu zetu walipata mtihani ninakwenda huko.

Mhe. Naibu Spika, ninachomshukuru angelikuwa kiongozi mwenye ubinafsi, umimi umimi angesema subiri twende pamoja, lakini akanambia nenda kaifanye hiyo kazi halafu utuletee taarifa. Lakini unajua huu ndio uongozi, hii ndio mtu kuwa na uchungu angelikuwa kiongozi tu mwengine akasema usiende huko ngoja na mimi nikapate kuonekana, lakini hakujali kitu hicho akanambia mwanangu Raza nenda kaifanye kazi hiyo uikamilishe inatosha hiyo. Sasa hao ndio viongozi tunaowataka wenye uchungu na nchi.

Kwa hivyo, mimi ningeliomba bado hatujachelewa vitu kama hivi vinatokea mitihani vinakuja vingi na wananchi tunataka tuwasaidie. Mimi pamoja na wenzangu bado azma yetu pamoja na wenzangu waliokuwa nje kwenda Kisiwapanza, kwenda Micheweni na sehemu nyengine kuona mazingira tuliyokuwanayo. Tunasaidiana, tunashirikiana letu pamoja Pemba/Unguja, Unguja/Pemba. Hiyo ndio lugha yetu sisi na hicho ndicho tulichopewa na Mwenyezi Mungu hakuna mtu aliyekuwa hajachanganya katika nchi hii ndio maana nikasema *we are all cosmopolitan.*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka katika hili niingie katika suala la waandishi wa habari. Ni kweli *Alhamdulillah* kiongozi wetu msimamizi wa humu ndani ni mwenyekiti wetu, ndiye ambaye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mimi naamini Dokta Ali Mohammed Shein hakubahatisha hata kidogo kumteuwa Makamu wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wake wote, pamoja na wizara yote na serikali nzima ambayo yeye ndiye anayeongoza chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema tumeingia tena kwenye bajeti kuna mengine kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kwa nia nzuri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilisimamia suala la ahadi za Wawakilishi kupitia majimbo yao. Masuala mengine yamesimamiwa na baadhi ya mawaziri kuchukua dhamana.

Mhe. Naibu Spika, lengo ni zuri lakini mimi nilichokuwa nataka kuomba *communication is very important*, tukiwa na mawasiliano ya majimbo panapotokea jambo ni vizuri tukaitana. Kwa mfano, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alisimamia suala lile la barabara za ndani za Jimbo la Uzini lakini uzuri wa mawasiliano akanikutanisha na watendaji wa Idara ya Barabara. Unajua hakuna kitu kama *communication* na kufahamu mambo, kuna usemi unasema: "Ushamba si kuzaliwa shamba, kutofahamu mambo".

Kwa hivyo, nilipokuta nikaambiwa ehee bwana Raza hii hapa, Wizara ya Miundombinu kwa kweli niliwaelewa, mwanzo nilikuwa sijaelewa niliona kama kuna vikwazo, nilielewa kuniambia kwamba Bwana Raza kweli umefanya majukumu hayo, kweli umechangia, serikali imeshafanya mambo mengi kama barabara, kilimo, utalii, mengi sana sisi tunajaliza tu baadhi ya vitu lakini Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye kuwatumikia wananchi ishafanya mambo mengi sana na inaendelea kufanya mambo yake chini ya Dokta Shein. Lakini baada ya kukutana na wataalamu wale wa Idara ya Barabara wakaniambia, Raza sisi hatuna tatizo lakini tatizo letu ni zana za kufanyia kazi hatuna za kutosha na thamani yake hii hata tukiagiza inakaribia dola milioni tano, lakini kila tutakachojaaliwa tutakuwa tunafanya.

Mhe. Naibu Spika, *this is very good* ni *communication,* lakini unatoka mtu una kiburi hutaki kujibu, *that is a problem*. Kwa sababu *we are here for the people power* sasa vizuri ni usikivu. Mimi nampenda sana simsifu kwa sababu yuko pale Mhe. Waziri wa Fedha ni mtu msikivu, ni mtu ambaye ana busara, ni mtu ambaye akikufahamisha unafahamu. Kwa sababu mimi nilimfuata nikamwambia kaka yangu Mhe. Omar Yussu Mzee kuna skuli ile ulisimamia wewe katika buti lile ukasema utakwenda kuimaliza, lakini akanielimisha akanambia kweli jambo hili lipo nimelifanya moja, mbili, tatu. Sasa vitu kama hivi vinaleta mambo ya mshikamano, lakini kufika pale ukasema *you don't care* halafu tuje hapa hakuna haja hiki chombo ni cha wananchi ni chombo ambacho tunalenga kwa faida ya wananchi ndio maana nikasema chombo hiki hakuna wapinzani humu, wapinzani katika chombo kama hiki wako Dodoma humu kuna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, hata hizi bajeti zote zinazokuja hapa zimepita kwenye Baraza la Mapinduzi akiongoza Mhe. Rais, ambalo lina Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili na Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mfumo wa

Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa hivyo, mimi ningeliomba kiongozi mkuu wa serikali, Makamu wa Pili wa Rais kama mawaziri hawatakuwa waangalifu katika hili maana sio kila anayepepesuka ni mlevi na maporomoko ya maadili ambayo dalili ya mvua mawingu tunaiona, tutawapelekea salamu sio nzuri wananchi waliotuteua. Kwa hiyo, *they are not the losers*, *we are the losers*.

Mhe. Naibu Spika, Baraza lako hili waandishi wa habari ni watu muhimu sana hasa wa Zanzibar. Mimi nawasifu sana waandishi wa habari wa magazeti ya Zanzibar Leo na *ZBC* kwa uzalendo, kwa udugu, kwa kupenda nchi yao. Mheshimiwa waandishi mafao yao ya hapa na wanaofanya kazi Bara *Wallahi* Mbingu na Ardhi. Sasa nashangaa vitu vidogo *overtime* yao mtu anatoka asubuhi nyumbani kwake mpaka saa tatu akirejea hata huo mgongo na kiuno vinauma hawezi hata kukaa kitako.

Sasa tuwafikirie tuwe na huruma, wizara inayohusika ipunguze matumizi yake, lakini leo utamkuta mwandishi Zanzibar Leo, *ZBC* anadai shilingi laki nane halafu kuna wakati tunaonekana tunakwenda kufanya sherehe tunatumia shilingi milioni tano. Sasa tuwe ni watu wasikivu na kiongozi wetu ndiye Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lazima tutizame maslahi ya hao waliokuwa wanyonge ndugu zetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, siku nyengine mtu hana hata vespa, baiskeli anatoka hata akifika daladala ng'ambo huko Fuoni ndani au Mfenesini saa tano halafu aje kuripoti na akichelewa matatizo makubwa.

Sasa mimi nilikuwa nasema hawa ndugu zetu tuwatizame kama tunavyotizamwa sisi bila wao hii *message* haifiki kwa wananchi. Mheshimiwa hakuna suala la kupendelea wala hakuna suala la umaarufu, nyanja zote tuna wenzetu upande wa skuli walimu, upande wa wizara zote wale watu ambao walimu wamefanya *overtime* kuna wengine mafao yao Mheshimiwa mambo madogo.

Mimi naamini serikali inapenda hivyo lakini unapopandisha mishahara ujue mafao nayo yanakuwa yanazidi, kama umepanga shilingi bilioni mbili na tayari mishahara imepanda *it means* usitegemee shilingi bilioni mbili inabidi Waziri wa Fedha Mwenyezi Mungu ampe nguvu na watendaji wake aanze kutafuta zile ambazo zimepungua zijalizwe, kwa sababu zile zinazidi tena. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi ningeliomba hii Wizara kusimamia kazi na mawasiliano, hili litasaidia katika yote haya.

La mwisho, Mhe. Naibu Spika, suala letu la Muungano. Mhe. Naibu Spika, *alhamdulillahi* Muungano wetu ni imara na Muungano wetu uliounganishwa kati ya Hayati Mzee Mwalimu Nyerere (Baba wa Taifa) na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu amlaze pahali pema.

Lengo la viongozi wawili hawa kuunganisha Muungano wetu ilikuwa ni kuwaleta wananchi matunda, ilikuwa kuwaletea upendo na ilikuwa kuwaleta wananchi faida katika maendeleo. Lengo ilikuwa ni hilo tu na kuwaweka watu wote sawa na malengo yao kuwasaidia wananchi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hata mapinduzi yetu matukufu ya Zanzibar tulipoyafanya, tulifanya kuwaletea wananchi maendeleo, tukafanya mapinduzi, tukasema tujiamulie mambo yetu wenyewe. Ndugu zetu wa Tanganyika wamefanya uhuru wao kwa kusaidia taifa. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nchi mbili hizi zimeungana huru katika njia ya kuheshimiana, kupendana na trust zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini ninasema hivi ninatanguliza haya. Mhe. Naibu Spika, mimi ningelimuomba Waziri ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye msimamizi wa muungano Mhe. Mohammed Aboud. Kidonda tulichokipata Mhe. Naibu Spika, sisi kwa Zanzibar ya *ESCROW* ni kubwa sana na tumefanya mapinduzi Zanzibar. Mmoja alijiona bora.

Sasa ikiwa watu wanne ambao hawahusiki muungano, hauna muhimili kwa sababu Mhe. Naibu Spika, zinaweza kufika lakini hii si shida. Watu wamejichukulia pesa wanne, watano. Nchi nzima Zanzibar bajeti imeathirika, *it is not Union matter*. Sasa Mhe. Naibu Spika, ningelishauri kwa Mhe. Waziri na watendaji wake wakenda kumuona mwenziwao Waziri Mkuu, ni msikivu sana hata Mhe. Rais Jakaya Mrisho Kikwete ni msikivu, ana hekma, busara na huruma, tukajua *what the solution.*

Mhe. Naibu Spika, hii imeathiri inawagusa wananchi wote hasa waliokuwa chini maskini za Mungu. Mhe. Naibu Spika, tunaposema au tunapotafuta uongozi tunasema tunatafuta uongozi uliokuwa wa kusimamia haki. Sasa leo mapambano ya rushwa, viongozi wanachota mabilioni ya pesa. Mhe. Naibu Spika, hakuna mwananchi hata kama anaipenda nchi yake anaweza kuja kuwa kiongozi kipindi kama hichi, kama hana mabilioni; maana siku hizi milioni hazitajwi, inaitwa vijisenti tu mamilioni. *What is next* Mhe. Naibu Spika?

Kama tutachukua watu katika sehemu mbali mbali, katika Baraza katika Bunge kuwaingiza watu ambao wenye utajiri wa kuweza kutumia pesa, halafu yule mnyonge wa mapinduzi matukufu ya Zanzibar juu ya uwezo wake, usomi wake, kukaa kwake, kufundishwa mapinduzi akashindwa hata kuwa Katibu Tarafa. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba Serikali hili ilione na mimi ninaamini Serikali yetu zote mbili ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano haitomuonea mtu kwa

rangi, sura au kwa dini. Yeyote atakayefanya makosa ataonewa na makosa yake. Ndivyo ilivyo.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hili limeathiri na siyo jambo ambalo la kawaida. Mimi ninashukuru sana na ninarejea tena kupitia Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kumshukuru Rais kwamba angalau Mwenyezi Mungu katupenda bei ya mafuta imeshuka bei. Ninaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeondosha ushuru wa chakula.

Mhe. Naibu Spika, *it could be crisis*, watu wanne, watu watano, hawapo katika mjadala. Mtu hata kama baa yake imefungwa anachukua ndege anakodi gari anakwenda nayo. Sasa kuna John, kuna Jecha, kuna Pandu. Mhe. Naibu Spika, ninataka hili tulione sote na Serikali ilione na hivi vitu vinakwenda. Tumepata mkasa wa *Richmond* tumeumia, *EPA* tumepelekwa *sanction*.

Sasa kuna vitu hivi Mhe. Naibu Spika, mimi ninasema bora tule ugali au sembe lakini tuweze kujiamulia mambo yetu wenyewe, hasa Zanzibar na kwa upande wa nini, hasa Zanzibar bora tule ugali, tule sembe tujiamulie mambo yetu wenyewe na tunaweza hilo Mhe. Naibu Spika, hakuna lisilowezekana kwa Zanzibar. Tumepiga hatua kubwa sana. Serikali ya Dkt. Ali Mohammed Shein imepiga hatua kubwa sana, imekusanya mapato ya kutosha, ina madini ya kutosha. (*Makofi*)

Serikali hii mimi ninaamini ya Dkt. Shein haimdhulumu mtu. Kwa hivyo mimi ninaamini, mimi ninashukuru. Ninamshukuru Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad, ninaishukuru Serikali, ninamshukuru Makamu wa Pili wa Rais, ninawashukuru Mawaziri wote na watendaji wote kwa namna ya kuweza kuungana na kuuleta umoja wetu. Mimi matumaini yangu kwamba hivi vilio na hali hii ya ESCROW ninazungumza kwa kitu ambacho kipo, hali si nzuri.

Mhe. Naibu Spika, leo Dola za Kimarekani ni elfu mbili na arobaini na tano. Bado *sanction* tunayo. Sasa mimi hili na mimi ninaamini hakuna kitu kama dola. Mheshimiwa Kikwete na Serikali yake ni watu wastaarabu, wanaipenda. Mimi ninafikiri kipenzi cha huyu ni Mheshimiwa Mohammed Aboud kijana mzuri sana, anakubalika hata kwetu sisi kwa wafanyabiashara, hata ukiwa na kelele gani, anakwambia bwana njoo hapa hebu kaa kitako, tatizo nini. Sasa hii ndiyo raha yake ya Mawaziri wetu hawa, akina Mhe. Haji Omar Kheir, wote Mawaziri hao, wanakwambia hebu kaa kitako nini tatizo. Sasa hiyo ndiyo raha yetu tunajuana.

Mhe.Naibu Spika, naipongeza Serikali, naipongeza Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ninaiunga kwa asilimia 199 bajeti hii ipite na matumaini yangu viongozi wote Wawakilishi wote kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu hapatakuwa na ile paa! paa! hapatakuwa na buti.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kumpa heshima Makamu wa Pili wa Rais. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Mohammedraza. Sasa tunamalizia na mchangiaji Mhe. Marina Joel Thomas.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi kuchangia hotuba ya Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, kwanza shukurani zangu za pekee nipende kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake mahiri na usimamizi mzuri wa shughuli zake za Serikali anazozifanya kwa kuzingatia Katiba na sheria ya nchi.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Rais wa Zanzibar amekuwa mstahamilivu mkubwa, asiyeteteреka na kuwa mstari wa mbele katika kuhimiza uwajibikaji, uadilifu katika utendaji wa shughuli wa shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, chini ya uongozi wake nchi imepiga hatua kubwa ya kimaendeleo katika nyanja mbali mbali za kiuchumi, kijamii, kisiasa. Hapo pia ninamuomba Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu, ampe afya njema yeye na familia yake azidi kutuongoza kwenye kipindi kijacho kinachoendelea. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze tena Makamu wa Pili wa Rais kwa kuwasilisha hotuba hii na kuweza kusimamia vyema shughuli za Serikali mbali mbali kwa manufaa ya nchi na wananchi wetu kwa jumla. Pongezi nyengine Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza kwa masuala mbali mbali yanayohusu maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nitaanza katika hali ya kisiasa kwenye *page* ya 4 hii. Kwa upande wa hali ya kisiasa Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru Mungu amani na utulivi inatawala, lakini pia tukiangalia na hii imepelekea hata kuleta maendeleo katika nchi yetu kwa fursa mbali mbali zimeongezeka kwa wawekezaji na hii imepelekea kuleta kuinua hali ya uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kusema sasa hivi tumekabiliwa na mambo mawili makubwa ya kura za maoni pamoja na uchaguzi. Lakini nilikuwa ninaiomba Serikali pindipo ikitokea watu wote ambao wanaashiria uvunjifu wa amani kipindi hiki chote, Serikali iwachukulie hatua za kufaa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika huduma za kijamii na hapa nitalenga katika mambo ya elimu. Mhe. Naibu Spika, pia hapa ninapenda nimshukuru tena Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kufuta ada zote za mitihani ya elimu ya msingi na sekondari pamoja na suala zima la msaada kwa wazee kutoka shilingi arobaini elfu mpaka sitini elfu na achanganye kabisa Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuwataka wale wazee kuanzia umri wa miaka sabini na kuendelea kuwajengea mazingira mazuri ya kupata maslahi ya kila mwezi ambayo yatasaidia katika kuendeleza maisha yao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda kwenye afya. Sekta ya afya imepiga hatua nzuri, hatua mbali mbali za maendeleo, mambo ya ujenzi, mambo ya huduma mbali mbali ya maradhi mbali mbali lakini pia katika suala lake, kuna suala zima la jengo la *ICU*. Jengo ni zuri, wenzangu wamesema baadhi ya Wawakilishi lakini kunahitaji madaktari mabingwa. Kwa hivyo naiomba Serikali ilizingatie hili, kwa sababu bila ya madaktari bingwa hata hii *ICU* itakuwa haina sifa kama sifa ilivyokuwa nayo hivi sasa. Kwa hivyo, ijitahidi ilete madaktari bingwa ili wagonjwa wetu wasisumbuke.

Pia ninaipongeza kwa jengo jipya ambalo la matibabu ya upasuaji wa kichwa pamoja na uti wa mgongo. Ninaipongeza Serikali kabisa katika suala hili imepiga hatua nzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika mapambano dhidi ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Suala hili Mhe. Naibu Spika, lipo na linaendelea kukua siku hadi siku, watoto wetu wananyanyasika, wanawake wanadhalilishwa. Na pia hapa nimpongeze Rais wa Zanzibar kwa kufungua kampeni mnamo tarehe 6 Disemba, 2015 ili kupiga vita udhalilishaji wanawake na watoto. Kauli mbiu imetoka ni udhalilishaji wanawake na watoto Zanzibar basi na ninaamini itakuwa basi kama tutafuata sheria, taratibu zilizopo. Yakitokea masuala kama hayo ya udhalilishaji ya watoto na wanawake, sheria ikichukua mkondo wake, watu wakachukuliwa hatua, ninaamini hili suala hili litatuka siku hadi siku na hatimaye kumalizika kabisa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, suala zima la kukabiliana na maafa. Katika *page* ya 22 mpaka 23 imeeleza malengo ya Idara hii na imesema katika moja ya malengo imesema Idara ilikuwa na lengo la kuifanyia matengenezo maghala mawili na kununua vifaa vya kukabiliana na maafa kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji imeelezwa kama imefanyia matengenezo mahala lakini suala la vifaa halijaoneshwa katika ripoti hii. Mhe. Naibu Spika, naomba nipate maelezo kwa sababu huku alisema watanunua vifaa lakini katika

utekelezaji wameeleza suala la matengenezo ya maghala, lakini ununuzi wa vifaa haijaonesha pahali popote.

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika Ofisi ya Uratibu. Mhe. Naibu Spika, imeelezwa hapa katika suala zima la ufuatiliaji wa miradi midogo midogo ya wananchi kupitia mfuko wa maendeleo wa jimbo. Lakini katika ripoti hii Mhe. Naibu Spika, wameeleza kama kuna majimbo manane ambayo yamerejesha marejesho. Nayo ni Donge, Kitope, Matemwe, Dimani, Makunduchi, Mtoni, Koani kwa Unguja na Pemba ni Chambani. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia Idara ya Uratibu inafanya kazi kubwa na inapata changamoto nyingi katika kufuatilia shughuli hizi. Kwa hivyo, ili kurahisisha Idara hii ifanikiwe vizuri katika kazi zake, niombe tu hizi fedha zinazotiwa katika majimbo zifanyiwe kazi na marejesho yarejeshwe, ili Idara hii ya Uratibu iweze kuratibu shughuli zake kwa uhakika kabisa. Na pia tutawapunguzia changamoto ambazo zinawakabili katika ugumu wa kukusanya kufanya marejesho hayo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika suala zima, kuna ukusanyaji wa mapato hapa na katika Idara ya Uchapaji na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni mia nne hamsini hadi kufikia mwezi wa Machi, 2014.

Ofisi imekusanya jumla ya shilingi milioni mia mbili na tisini na tano, mia tisa na tatu sawa na asilimia sitini na sita ya lengo. Hapa ninataka kujua tu Mhe. Naibu Spika, labda kwa nini halijafikiwa lengo, labda kuna changamoto zozote ambazo zimeikabili zifikiwe lengo hili.

Pia kuna Idara ya Uendeshaji na Utumishi pia ilipangiwa kukusanya shilingi milioni tatu laki saba na hamsini kwa makusanyo ya kodi katika jengo la Baraza la Wawakilishi la zamani, lakini hadi kufikia mwezi wa Machi, 2015 hakuna fedha yoyote iliyokusanywa.

Mhe. Naibu Spika, kumeelezwa changamoto ambayo kutokupatikana mapato hayo. Wamesema hali hii imetokana na ukumbi huo kukosa kukodishwa kwa vile upo katika hali isiyoridhisha na unahitaji matengenezo makubwa na kuwekwa vifaa vya kisasa.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa ninaiomba niishauri Serikali kwa sababu hili ni jengo na likifanyiwa matengenezo litatumika na pia litaingiza mapato katika nchi yetu.

Kwa hivyo, ninaishauri Serikali ilifanyie marekebisho, ukarabati ili iwe kama ni chanzo kimoja cha mapato ambacho kitasaidia Serikali kuendesha shughuli mbali mbali za maendeleo katika nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naomba nishukuru kwa sababu ya sherehe za mapinduzi kwa kufanikiwa kwa kiasi kikubwa sana zaidi ya asilimia 100. Na ninapenda niipongeze Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kulisimamia hili na kamati mbali mbali ambazo zimetekeleza shughuli hii.(*Makofi*)

La mwisho, Mhe. Naibu Spika, nimeona suala zima la kujengwa kaburi la Dkt. Abdulwakil Rais Mstaafu. Ninataka niipongeze sana Serikali hili ni utekelezaji mzuri, kwa sababu huyu ni kiongozi wetu, alikuwa ni Rais wetu kaitumikia nchi hii. Kwa hivyo ni jambo jema kabisa limefanywa na naomba niipongeze Serikali kwa dhati kabisa.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Marina. Waheshimiwa Wajumbe hivi leo tulipata wachangiaji 21 na tayari wachangiaji 10 wamekwishakuchangia, wamebakia wachangiaji 11 nitawataja ili kesho tukija tukijaaliwa mapema asubuhi baada ya maswali tuweze kuanza kuchangia. Nao ni:-

1. Mhe. Fatma Mbarouk Said
2. Mhe. Panya Ali Abdalla
3. Mhe. Omar Ali Shehe
4. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
6. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
7. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
8. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
9. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma
10. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
11. Mhe. Mgeni Hassan Juma

Naomba Waheshimiwa hao kesho waje mapema ili tuweze kujipangia vizuri, tunategemea kwamba bajeti hii ifanywe majumuisho jioni na ipitishwe kesho tukijaaliwa.

Kwa hivyo, ninawashukuru kwa mashirikiano mulionipa na sasa naahirisha kikao chetu hichi hadi kesho siku ya Alhamis tarehe 21/05/2015, saa tatu barabara za asubuhi.

*(Saa 1.34 usiku Baraza liliahirishwa hadi*
*tarehe 21/05/2015 saa 3.00 asubuhi)*